# Nipashe

Alhamisi Machi 19, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580183

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US







## Maalim Seif aeleza Lowassa alivyouvunja moyo upinzani

UKURASA 4

UKURASA 13

# Makali corona yazidi kung'ata



• **Wagonjwa** wafikia watatu, Bakwata yatoa maagizo mazito, vyuo vikuu vyafungwa, Zanzibar yafunga shule na madrasa... *Uk. 2, 3,4,8, 24*



**BAA LA CORONA**

**Wakati uvaaji wa maski ukiendelea kupamba moto katika maeneo mbalimbali nchini kwa lengo la kujikinga na corona, Shirika la Afya Duniani (WHO) limesema anayetakiwa kuvaa vifaa hivyo ni yule mwenye maambukizo tayari au anayemhudumia mwenye virusi hivyo.**

- **Epuka mikusanyiko ya watu**
- **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
- **Epuka kusalimiana na kushika mikono na kukumbatiana**
- **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**





Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson na Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Freeman Mbowe, kwa nyakati tofauti, wakipimwa joto la mwili kabla ya kuingia katika Ofisi za Bunge, jijini Dodoma jana, kufuatia utaratibu uliowekwa ili kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa corona. Ofisi ya Bunge, pia imeweka vifaa vya kuosha mikono (sanitizers), katika maeneo mbalimbali ya Bunge. **PICHA: BUNGE**

## Lissu ataja vikwazo kurejea

UKURASA 4




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## Waziri aagiza idadi abiria wa kusimama mwendokasi

UKURASA 2

MICHEZO SVEN: KILICHOBAKI SIMBA NI REKODI TU UK.32 MAONI, KATUNI UK.6

## TISHIO CORONA

# Agizo abiria watakaosimama daladala, mabasi mwendokasi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, ameiagiza Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini (LATRA) kwa kushirikiana na wataalamu wa afya, kushauri idadi ya abiria wanaoruhusiwa kusimama kwenye daladala na mabasi ya mwendokasi ndani ya siku tatu.

Kadhalika, ameagiza kuwa ndani ya muda huo kukutana na Halmashauri za majiji na miji ili kuweka utaratibu utakaodhibiti wingi wa watu kwenye vituo vikuu vya mabasi ya masafa marefu.

Aidha, Kamwelwe amesema Serikali ipo katika hatua ya mwisho kukamilisha mfumo wa kukata tiketi kwa njia ya kielektroniki, ambao utapunguza kwa kiwango kikubwa mikusanyiko ya watu katika vituo vya kukata tiketi.

Maagizo hayo aliyatoa jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na wanahabari kuhusu hatua zinazopaswa kuchukuliwan katika huduma za usafiri wa umma ili kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona.

Kamwelwe alisema ni vyema tahadhari kubwa ikachukuliwa kwenye maeneo yenye mikusanyiko mikubwa ya watu ikiwamo daladala, mabasi yaendayo mikoani, treni, meli, vivuko na ndege.

Waziri huyo alisema makampuni ya mabasi yaangalie uwezekano wa kuwa na vituo vingi maeneo mbalimbali ya miji vya kukatia tiketi ili kupunguza msongamano katika vituo vya mabasi.

"Tunashauri abiria wanaosafiri kwa mabasi ya masafa marefu wasisindikizwe na watu wengi ili kupunguza msongamano kwenye vituo vya mabasi," alisema.

Aliwataka wamiliki, madereva na abiria wa mabasi kuhakikisha wanatumia vitakasa mikono mara kwa mara baada ya kushika nyaraka mbalimbali zikiwamo fedha, tiketi, mizigo na maeneo mengine.

"Kwenye suala la idadi ya abiria itakayoshauriwa na wataalamu wa afya, madereva na makondakta wazingatie kama itakavyoshauriwa," alisema.

Kuhusu usafiri wa treni, Waziri Kamwelwe aliagiza Shirika la Reli Tanzania (TRC) na Mamlaka ya Reli Tanzania na Zambia (Tazara), kuhakikisha wanakuwa na vitakasa mikono stesheni na ndani ya treni, na kutenga vyumba maalum kwa ajili ya kuwafanyia uchunguzi wa ziada wale watakaoshukiwa kuwa na dalili za ugonjwa huo.

Kadhalika, aliitaka Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) kutenga vyumba hivyo maalum na kuwa na vitakasa mikono.

"Ninaagiza Latra, Tasac, TPA, TAA na TCAA kushirikiana na wataalam wa afya kuandaa matangazo na kuweka utaratibu wa kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi," alisema.

Alisisitiza taasisi hizo pia zishirikiane na wataalam wa Wizara ya Afya na wamiliki wa vyombo vya usafiri kuweka utaratibu wa kupuliza dawa ya kuua wadudu katika vyombo vya usafiri.

Kuhusu kufunga mipaka, Kamwelwe aliagiza kuwapo na udhibiti wa wanaoingia nchini kwa njia za panya, huku akisema hatua za kufunga zitafikiwa endapo tatizo hilo litakuwa kubwa.



Mufti wa Tanzania na Mwenyekiti wa Baraza la Ulamaa Taifa, Sheikh Abubakar Zuberi, akizungumza na wanahabari jijini Dar es Salaam jana, wakati akitoa tamko la baraza hilo, kuhusu janga la ugonjwa wa corona (COVID 19). **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Makali ya corona yazidi kung'ata

**Na Romana Mallya**

MAKALI ya ugonjwa wa corona yameendelea kuleta athari zaidi katika jamii hatua ambayo imesababisha serikali na wadau mbalimbali kuchukua uamuzi mbalimbali katika kukabiliana na tatizo hilo.

Wakati serikali na washirika wakichukua hatua, imetangazwa kuwa wagonjwa wengine wawili wa corona wametambuliwa nchini, hivyo kufanya idadi kufika watatu baada ya mgonjwa wa kwanza kugundulika Jumatatu.

Katika kuchukua hatua stahiki, serikali pia imelazimika kusitisha masomo ya vyuo baada ya awali kufunga kwa siku 30 shule zote kuanzia za awali hadi kidato cha sita.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alitangaza hayo jana jijini Dar es Salaam na kubainisha kuwa wagonjwa walioongezeka ni raia wa kigeni. Alisema mmoja amepatikana visiwani Zanzibar na mwingine jijini Dar es Salaam.

Majaliwa alisema mgonjwa aliyebainika Zanzibar ni raia wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 24 na wa Dar es Salaam ni raia wa Marekani mwenye umri wa miaka 61.

"Sampuli za Mjerumani zililetwa maabara kuu na kuonekana amepata maambukizo na Dar es Salaam tuna Mmarekani ambaye amegundulika ana virusi vya corona," alisema.

Majaliwa alisema serikali inatambua vyuo vya ualimu vinatakiwa kufanya mitihani Mei mwaka huu, hivyo akamwagiza Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, kufanya marekebisho ya mihula ya mitihani yao kama alivyotakiwa kufanya kwa shule za sekondari.

"Watanzania tutaendelea kuwapa taarifa, lakini bado tunatoa wito kuwa makini na kutokuwa na taharuki, hatua zitaendelea kuchukulia na kadri siku zinavyokwenda, tunapochukua hatua tunaona umuhimu wa kusitisha baadhi ya shughuli kadri tunavyoendelea.

**MADRASA KUFUNGWA**

Mufti wa Tanzania, Sheikh Mkuu Abubakary Zubeiry bin Ally, ameagiza kufungwa kwa madrasa zote nchini kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Akitangaza uamuzi huo jana, Mufti alisema umetokana na kikao cha Baraza la Ulamaa kilichofanyika juzi na kuamua walimu wote wa madrasa kuzifunga mpaka serikali itakapotangaza vinginevyo.

Pia alisema baraza limewashauri waumini wa dini hiyo ambao wanaweza kwenda msikitini, waende na mikeka yao, wafanye hivyo ili kutoruhusu maambukizo.

"Wenye matatizo ya kiafya na wenye umri mkubwa, baraza linawashauri kuswali majumbani mwao kwa sababu sifa za ugonjwa huu wapo kwenye hatari zaidi kuambukizwa, kanuni za usafi misikitini maeneo yote uzingatiwe," alisema.

Kiongozi huyo alisema baraza limewataka waumini kuchukua udhu zao nyumbani badala ya msikitini.

"Ile dua Msikiti wa Mtoro iliyokuwa ifanyike Ijumaa ijayo na ilitarajiwa kuongozwa na Mufti, baraza limeamua isiwapo tena, kila imamu ajitahidi kuleta dua za qunuti (maalum) kwa sababu hatupendi watu wakusanyike," alisema.

**BIASHARA KUENDELEA**

Licha ya kuwapo kwa tishio na kusambaa kwa ugonjwa wa corona, Waziri Mkuu alisema shughuli za biashara katika maeneo mbalimbali zitaendelea.

"Bado shughuli za maduka, masoko zitaendelea, natamka hili kwa sababu tumeanza kuona mkanganyiko mkubwa kwenye maduka na masoko, hizo zitaendelea, huduma za usafirishaji zitaendelea, lakini wasafirishaji waendelee kuelimisha abiria," alisema.

Majaliwa alisisitiza hatari ya kujaza abiria kwenye vyombo vya usafiri, akiwataka wamiliki kuchukua hatua.

"Tuendelee kutoa huduma hizo za usafiri, maduka na masoko ili watu wapate chakula, tunaendelea kuwahifadhi hawa pale tutakapojiridhisha tatizo limekwisha ndipo tutawaondoa," alisema.

Waziri Mkuu Majaliwa alisema serikali imejizatiti na inaendelea kuwa makini na maeneo yote yenye mipaka ili kujiridhisha wote wanaoingia Tanzania hawana maambukizo.

UDSM YASITISHA USAILI

Wakati Majaliwa akitangaza hilo, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kimetangaza kuahirishwa kwa usaili kwa waombaji wa kazi wa nafasi mbalimbali ambao walitakiwa kufika leo.

Katika taarifa ilitolewa jana na Ofisi ya Naibu Makamu Mkuu wa Chuo hicho (Utawala), usaili huo umeahirishwa mpaka watakapofahamishwa tena. "Hii ni kutokana na kuepusha uwekezano wa kuendelea kusambaa kwa ugonjwa wa virusi vya corona, chuo kinaomba radhi waombaji wote wa kazi kwa usumbufu utakaojitokeza kutokana na kuahirishwa kwa usaili," ilisema taarifa hiyo.

Juzi, Majaliwa alitangaza kuzuia mikusanyiko ya ndani na nje isiyo ya lazima kama semina, mikutano, makongamano, shughuli za kisiasa na michezo ili kujikinga na ugonjwa huo.

# Waziri Mkuu ataka SADC kuungana dhidi ya corona

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amezitaka nchi wanachama wa Jumuiya ya Kusini mwa Afrika (SADC) kuungana katika mapambano ya kuutokomeza ugonjwa wa virusi vya corona pamoja na kufuata masharti yatolewayo na wataalamu wa afya, vinginevyo utaathiri uchumi wa nchi.

Amesema ugonjwa huo ni vita kubwa ya kidunia unaohitaji mshikamano wa pamoja katika kupambana, hivyo nchi wanachama wa SADC zinapaswa kushirikiana kuutokomeza.

Alitoa agizo hilo jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua mkutano wa Baraza la Mawaziri wa SADC, uliokuwa unafanyika kwa njia ya video ukiwajumuisha Mawaziri wa Fedha na Mipango, Viwanda na Biashara, Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

"Tunahitaji kupambana ili kuzuia maambukizi ya virusi vya ugonjwa huu, hii ni vita kubwa vinginevyo itaathiri uchumi wa nchi zetu," alisema Majaliwa.

Alisema ugonjwa wa virusi vya corona unasambaa kwa kasi katika nchi Jumuiya ya SADC hali iliyowalazimu Mawaziri wa SADC sekta ya afya kupendekeza mikutano ya jumuiya kufanyika kwa njia ya video.

Kadhalika, alisema katika miaka 40 tangu kuanzishwa kwa SADC mafanikio mbalimbali yamepatikana kama miradi mbalimbali ya miundombinu imeendelea kutekelezwa na kuiwekea kipaumbele sekta ya viwanda ambayo ni nguzo ya msingi katika kusaidia kukua kwa uchumi wa kanda na wa kila mwanachama.

"Vilevile tumefanikiwa kuboresha masuala ya kijamii kama afya, elimu, jinsia, mazingira yanaendelea kutekelezwa," alisema Majaliwa.

Naye Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri wa SADC, Prof. Palamagamba Kabudi, aliwataka mawaziri wa jumuiya hiyo kuendeleza ushirikiano, kubadilishana taarifa, utaalamu ili jumuiya hiyo iendelee kuwa imara.

Pia, alisema ushirikiano wa mawaziri utafanikisha mwenendo mzuri wa uchumi, biashara, uwekezajj na masoko ya fedha katika SADC kutokuyumba kutokana na hofu ya ugonjwa wa virusi vya corona.

Kadhalika kuna baadhi ya maeneo SADC imeonyesha mafanikio makubwa ambayo ni maendeleo ya viwanda na mtangamano wa soko, maendeleo ya miundombinu kwa ajili ya kuwezesha masuala ya mtangamano, ushirikiano katika ulinzi na usalama, demokrasia na utawala bora.

Alisema maeneo mengine ni utekelezaji wa programu mbalimbali za jumuiya ikiwa ni pamoja na masuala mtambuka kama huduma za pamoja na mabadiliko ya kitaasisi.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Waziri Kindamba alisema TTCL kufanikisha mkutano wa SADC kufanyika kwa njia ya video ni historia kwa Tanzania.




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akipunga mkono kuwaaga washiriki wa Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), baada ya kufungua mkutano huo kwa njia ya video, kwenye Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OWM**

# Mgonjwa wa kwanza wa corona azungumza na waziri kwa simu

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MGONJWA wa kwanza kutangazwa kuwa na ugonjwa wa corona, Isabella Mwampamba (46), jana alizungumza na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa njia ya simu na kueleza kuwa anaendelea vizuri.

Waziri alizungumza na mgonjwa huyo mbele ya waandishi wa habari waliokuwa katika mkutano uliofanyika jijini hapa, akiwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha ya Mount Meru.

Uamuzi wa waziri kufanya hivyo huku simu yake akiwa ameweka sauti ya juu, ulikuwa na lengo la kutaka waandishi pia wamsikie.

Isabella, katika mazungumzo hayo, alisema anamshukuru Mungu kwa kumlinda na serikali kupitia madaktari na wauguzi kupigania afya yake na kwamba kwa sasa anaendelea vizuri.

"Kweli nashukuru sana serikali kuniweka eneo maalum kwani sasa naendelea vizuri na naomba mshikamano kwa Watanzania, kwani mgonjwa wa kwanza Tanzania ni mimi na kuonekana kisababishi.

Naomba kubwa zaidi tumuombe Mungu atupiganie na ugonjwa huu sababu ni janga la dunia," alisema.

Alisema ni vyema kila mtu akatumia muda wake mwingi kuelimisha wenzake badala ya kukuza ugonjwa huo kwa kuwa ni tatizo la kidunia na si suala la kulaumiana.

Isabella alisema wizara imechukua hatua kubwa na madhubuti, hivyo hakuna haja ya Watanzania kuwa na hofu, kikubwa watu ni kuzingatia maelekezo yanayotolewa na serikali.

"Mimi hapa nimepewa kipimo najipima mwenyewe joto kila siku mara tatu kwani hiki ndicho kipimo kikubwa na wala sina homa, mafua wala kikohozi. Hata watumishi wa Mungu wananipigia simu na kuniombea, namshukuru sana Mungu," alisema.

Hii ni mara ya pili kwa Isabella kuzungumza tangu alipowekwa katika eneo maalum hospitalini hapo. Mara ya kwanza ilikuwa juzi alipozungumza na Nipashe kuelezea maendeleo ya afya yake.

"Naendelea vizuri, waambieni watu kwenye 'groups' (makundi) ya WhatsApp waondoe wasiwasi kwani naoga mwenyewe na kupaka mafuta. Kwa kweli naendelea vizuri," alikaririwa akisema.

Waziri Ummy Jumatatu iliyopita alithibitisha taarifa juu ya mgonjwa wa kwanza wa corona kubainika nchini huku akisema aliingia nchini Jumapili iliyopita kupitia Uwanja wa Kimataifa wa Ndege wa Kilimanjaro (KIA) akitokea Ubelgiji.

Kuhusu wagonjwa wapya, Waziri Ummy alisema jana Tanzania ilithibitisha kuwapo kwa wagonjwa wawili wa corona, baada ya kufanyiwa vipimo Maabara Kuu ya Taifa ya Afya ya Jamii.

# TIC yaahirisha mikutano yote

**Na Beatrice Shayo**

MKURUGENZI Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Geoffrey Mwambe, amesema mikutano mingi ya uwekezaji ya nje ya nchi wameiahirisha kwa sababu ya ugonjwa wa virusi vya Corona.

Mwambe ameyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akihojiwa na waandishi wa habari na kufafanua kuwa hilo ni tatizo la muda mfupi. Kutokana na tatizo hilo, Mwambe amesema kwa sasa hawawezi kuwavutia wawekezaji kuja nchini. "Hata mimi nawaogopa wawekezaji wakija hapa kwangu."

Alisema tatizo hilo limesababisha nchi nyingi kusimamisha safari na hata Rais John Magufuli, ametoa wito wa kuwalinda Watanzania kwa kukataza watu wasiende nje ya nchi kama hakuna sababu za msingi.

"Tulikuwa na mikutano mingi tumeahirisha hata juzi nilimwagiza Mkurugenzi wangu kwenda Zanzibar, kufika kule mkutano ilibidi uahirishwe tuna mikutano mingine Congo, Kigali, Misri na Israel tumeahirisha, unaweza kuona namna ambavyo hatuwezi kuvutia uwekezaji hii ni athari ya muda mfupi," Mwambe. "Kama mtu haijui Tanzania ni vigumu kuleta uwekezaji tujitahidi kuitangaza Tanzania ili ifahamike jambo ambalo litasaidia kuvutia wawekezaji kuja nchini hata wanamichezo wanariadha waitangaze vizuri Tanzania," alisema Mwambe.

Kadhalika alisema mamlaka za serikali zinatakiwa kuboresha huduma zake ikiwamo utaratibu wa ulipaji kodi kuwa wazi.

"Tusiwe ni watu wa kila siku unakuja na ufuatiliaji mpya wa kodi za juzi alizolipa mara kesho anaanza upya hajui kama ameshamaliza kulipa kodi au hajamaliza, je, anatakiwa kulipa kodi hii au anatakiwa kulipa zaidi? Huelewi kama umeshamaliza au atakuja mwingine mwakani kuambiwa ulipe nyingine, tunatakiwa kuwa na uhakika tunachokifanya," alisema. Alisema kila taasisi ina wajibu wa kumjali mwekezaji, hawatakiwi kuchelewesha huduma kwa mwekezaji bila sababu za msingi. "Wawekezaji hawajaja hapa kucheza tutoe vibali kwa wakati na kama kuna changamoto tuwasiliane ndani ya serikali ili kuwezesha mazingira ya uwekezaji kuwa mazuri na zile ambazo zinahitaji sera basi tuziboreshe," alisema. Kadhalika, alisema sheria inawataka kuwa na kituo kimoja chenye taasisi za serikali kwa lengo la kuharakisha uamuzi wa kutoa vibali kwa wawekezaji.

Alisema TIC wana taasisi 11 ambazo zinafanya hizo kazi ili kurahisishia mwekezaji kupata vibali vyake kwa wakati na kuwa na mtazamo mmoja wa serikali.

"Tukifanya ukaguzi wa pamoja na taasisi za serikali unasaidia kuepuka mazingira ya rushwa kila taasisi ikienda kivyake kwa mwekezaji na kujifungia wanamtisha mwekezaji na kujitengenezea mazingira ya rushwa," alisema.

# Maalim Seif: Lowassa kavunja moyo upinzani

**Na Romana Mallya**

MWENYEKITI wa ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, amesema kitendo cha Waziri Mkuu mstaafu, Edward Lowassa, kurudi Chama Cha Mapinduzi (CCM), kimeuvunja moyo upinzani.

Machi Mosi, 2019, Lowassa alitangaza kurejea CCM akitokea Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), alikokaa takribani miaka mitatu.

Lowassa alijiondoa CCM mwaka 2015, baada ya vikao vya juu vya chama hicho kukata jina lake katika mchakato wa uteuzi wa mgombea wake wa urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika uchaguzi wa mwaka 2015, Lowassa aliwania kiti cha urais kupitia Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa) akipambana na John Magufuli ambaye alimshinda kwa kupata kura 8,882,935 sawa na asilimia 58.46, huku Lowassa akijipatia kura 6,072,848 sawa na asilimia 39.97 ya kura zote.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Maalim Seif alisema: "Sisi upinzani tumevunjika moyo kwa kitendo chake cha kuhama Chadema na kwenda CCM, ambayo alikuwa akiipinga.

"Unaweza kufahamu Lowassa siyo kama Maalim Seif. Maalim Seif kazoea upinzani na mateso yake yote anavumilia, yeye alikuwa Waziri Mkuu na marupurupu yote kwa hiyo lile alilotegemea kulipata katika Ukawa hakulipata. Vile vile tunasikia Chadema haikumtendea vyema," alisema.

Hata hivyo, Maalim Seif alisema kuondoka kwa Lowassa Chadema ana sababu nyingi, hivyo hawezi kumhukumu.

**AFUNGUKA KIKWAZO NA LIPUMBA**

Maalim Seif ambaye kabla ya kuhamia ACT-Wazalendo, alikuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF), alikiri kuwa yeye ndiye aliyekataa kupatanishwa na aliyekuwa Mwenyekiti wa chama hicho, Prof. Ibrahim Lipumba, walipoingia katika mgogoro mkubwa baacha ya uchaguzi mkuu wa 2015.

"Sikumsusia, tukionana tunasalimia vizuri ila kufanya naye kazi haiwezekani, sina kinyongo naye, lakini siwezi kufanya kazi na mtu ambaye kanisaliti.

"Kama kanichoma mkuki mchana, usiku atafanya nini?" Alihoji Maalim Seif na kuongeza: "Simpi tena nafasi nyingine."



Dk. Ismail Gatalya (kushoto), akitoa elimu na mafunzo juu ya namna ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa corona, kwa wafanyakazi wa Vodacom Tanzania, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Lissu aanika kinachomkwamisha kurejea

**Na Enock Charles**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tundu Lissu, amezungumzia kurejea kwake nchini kuwa kutategemea majibu ya serikali kwa Kamati ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mabunge Duniani (IPU).

Kamati hiyo iliiandikia barua serikali ya Tanzania kuomba kuruhusiwa kumsindikiza Lissu kurejea nchini.

Awali, kamati hiyo ilitoa mapendekezo pamoja na mambo mengine kumsindikiza kiongozi huyo kurejea nchini kutokana na hofu ya usalama wake.

Akizungumza na Nipashe juzi, Lissu ambaye kwa sasa yuko Ubelgiji alikokwenda tangu mwaka 2017 kwa matibabu akitokea Kenya alikokuwa anatibiwa baada ya gari lake kumiminiwa risasi 32 kati yake tano zilimpata mwilini. Tukio lililotokea kwenye nyumba za serikali jijini Dodoma.

Kwa mujibu wa Lissu, mpango wake wa kurudi uko pale pale na sasa anachosubiri ni taarifa ya majibu kutoka Kamati ya Umoja wa Mabunge Duniani.

"Bado IPU hawajanipa taarifa yoyote ya majibu ya serikali nasubiri waniambie, ndipo nitajua lini narejea nyumbani," alisema Lissu.

Aidha, alisema amesikitishwa na kutolewa kwa vitu ndani ya nyumba ya bunge aliyokuwa akiishi kama Mnadhimu wa Kambi Rasmi ya Upinzani, huku akitoa lawama kwa mamlaka hizo kumzungusha aliyekwenda.

Hata hivyo, Bunge lilikanusha madai hayo kwa kueleza kuwa mtu huyo aliyetumwa na Lissu ndiye aliyekuwa hapatikani kuvitoa vitu hivyo kwenye nyumba hiyo ambayo Lissu alipangishiwa na bunge alipokuwa mnadhimu.

"Kuhusu vitu vyangu vilikwishatolewa kama wiki tatu zilizopita," alibainisha.

Lissu alipeleka malalamiko kwa kile anachodai kutotendewa haki na Bunge la Tanzania alipovuliwa ubunge wake.

Pia aliiomba kufanyika uchunguzi wa tukio lake la kupigwa risasi Septemba, 2017 na kamati hiyo kupendekeza pamoja na mambo mengine Lissu kusindikizwa kurejea nchini.

Pamoja na pendekezo hilo la kusindikizwa, kamati hiyo iméomba maelezo kutoka Bunge la Tanzania kuhusu sababu na hoja za uamuzi wa kuvuliwa ubunge kwa Lissu kuomba ruhusa ya kutembelea Tanzania kama ilivyopendekezwa huku ikieleza kusikitishwa na jaribio la mauaji ya mbunge huyo na suala la kuvuliwa kwake ubunge.

Lissu alivuliwa ubunge wa Singida Mashariki mwaka jana na Spika Job Ndugai kwa kile kinachodaiwa kuwa ni utoro wa shughuli za bunge baada ya Spika kudai kutokupata taarifa rasmi za mahali alipokuwa Lissu.

Sababu nyingine iliyotolewa ni kutokujazwa kwa fomu za maadili ya umma kwa miaka miwili mfululizo ambazo kikawaida hujazwa na wabunge kila mwaka.

## Wodi yatengwa watakaobainika na virusi corona

**Na Christina Haule,** MOROGORO

SERIKALI mkoani Morogoro imetenga moja ya wodi katika Hospitali ya Wilaya ya Morogoro iliyopo Mkundi kwa ajili ya kuwaweka wagonjwa wa corona kwenye karantini watakapohisi kupata maambukizi ya virusi hivyo.

Akizungumza jana kwenye kikao cha kamati ya afya ya msingi Manispaa ya Morogoro, kilichowakutanisha wadau mbalimbali wakiwamo watendaji wa halmashauri, viongozi wa dini, watu maarufu, wafanyabiashara na wanahabari, Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Regina Chonjo, alisema tahadhari iliyochukuliwa na manispaa ili kuhakikisha wananchi hawapati maambukizi.

Chonjo alisema kufuatia Tanzania kuwa na wagonjwa watatu hadi sasa, serikali ya wilaya haina budi kusisitiza mambo muhimu ya kufanya ili kujikinga na ugonjwa huo hatari.

Aliagiza kituo kikuu cha mabasi Msamvu, viwandani, hospitali, vituo vya mabasi na kwenye usafiri wa jumuiya kuwekwa huduma ya maji ya kunawa na kuhakikisha usafi unafanywa kwenye maeneo husika.

Aliitaka jamii kuacha kupuuza maelekezo wanayopewa ikiwamo matumizi ya dawa za kuosha mikono na kutambua namna ya kutengeneza dawa hizo hata majumbani.

Mganga Mkuu Manispaa ya Morogoro, Dk. Rashid Ikaji, alisema dalili za ugonjwa huo kuwa ni kukohoa, mafua, kuumwa viungo vya mwili, mwili kuchoka, homa kali na maumivu ya kichwa.

Dalili za mwisho ni vidonda kwenye koo, mafua mazito na yenye majimaji mengi, kutokwa na damu sehemu za wazi ikiwamo masikio, pua, mdomo na sehemu ya haja kubwa na ndogo kwa jinsia zote.

Naye Mkuu wa Mkoa mstaafu, Steven Mashishanga, ameiomba serikali kuweka bei elekezi ya vifaa vya kujikinga na ugonjwa huo ikiwamo maski na dawa za kudhibiti virusi hao kutokana na baadhi ya wafanyabiashara kupandisha bei maradufu kwa nia ya kutaka kujinufaisha kupitia ugonjwa huo.

Mkazi wa Manispaa ya Morogoro, George Lona, ambaye ameonyesha kuanza kuchukua tahadhari kwa kuvaa maski kujikinga na virusi hivyo, huku akiwashauri Watanzania wenzake kutopuuzia ugonjwa huo kwa kuwa ni hatari.

Ugonjwa wa corona unashambulia mapafu na kuleta shida katika upumuaji. Mgonjwa wa kwanza alibainika nchini China na kuenea nchi zingine ikiwamo Italia na kwa nchi za Afrika tayari watu wameshabainika kuambukizwa virusi hivyo katika nchi za Afrika Kusini, Rwanda, Ethiopia, Misri, Kenya, Tunia, Uganga, Congo na Tanzania.

HABARI KITAIFA



Msajili Msaidizi wa Vyama vya Siasa, Sisty Nyahoza (kushoto), akifafanua jambo mbele ya viongozi wa kitaifa wa Chama cha United Democratic Party (UDP), wakati wa zoezi la uhakiki wa vyama vya siasa katika makao makuu ya chama hicho, jijini Dar es Salaam jana. Wa pili kulia ni Mwenyekiti wa Taifa wa chama hicho, John Momose Cheyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Nida kufanya uhakiki upya vitambulisho vyenye utata

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Vitambulisho vya Taifa (Nida), imesema inafanya uhakiki upya kwa maombi ya vitambulisho vya taifa vyenye changamoto za uraia.

Taarifa ya mamlaka hiyo iliyotolewa juzi jijini Dar es Salaam na Ofisa Habari Mkuu wa Nida, Geofrey Tengeneza, ilisema hatua hiyo ni utekelezaji wa agizo la serikali la kuhakiki kwa kina maombi yote ya waombaji wa Vitambulisho vya Taifa yenye changamoto na upungufu.

"Upungufu ni wa aina mbalimbali ukiwamo uraia wa waombaji ili kuondoa mianya ya udanganyifu unaoweza kujipenyeza na hivyo kutoa vitambulisho vya raia kwa watu wasio raia wa Tanzania," ilisema taarifa hiyo.

Pia ilifafanua kuwa uhakiki huo unafanywa na Nida kwa kushirikiana na Idara ya Uhamiaji, Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya na Mikoa, Serikali za Mitaa, Idara ya Wakimbizi na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR).

"Uhakiki unakwenda sambamba na usajili wa raia, wageni wakaazi na wakimbizi, ugawaji wa NIN na vitambulisho kwa wakazi wa mikoa iliyoko Kanda ya Ziwa ambayo ni Kigoma, Kagera, Tabora, Geita, Mwanza Simiyu, Shinyanga na Mara," alisema.

Alisema wamejipanga kufanya uhakiki wa mara kwa mara kulingana na Sheria ya Usajili na Utambuzi wa Watu ambayo inaeleza kuwa mwombaji yeyote wa Kitambulisho cha Taifa atakayebainika kutoa taarifa za uongo kuhusu uraia wake, sheria itachukua mkondo wake.

"Niwasihi wote wenye nia ya kutaka kujipenyeza na kupata vitambulisho kinyume cha utaratibu, Nida haitawasaidia kwa kuwa uhakiki unaofanywa ni endelevu na utafikia mikoa yote, mwombaji yeyote aliyedanganya taarifa za uraia wake ni vyema akajisalimisha mapema," alisema.

Alisema uhakiki huo umeanza mikoa ya Kanda ya Ziwa kwa sababu ipo mipakani na ndiko kwenye mchanganyiko wa raia wa nchi za jirani.

"Zaidi ya watu 21,721,416 wamesajiliwa huku miongoni mwao 17,674,812 wameshatambuliwa kwa kupatiwa namba za utambulisho wa taifa na wengine Vitambulisho vya Taifa.

Alisema taarifa za waombaji wengine waliosajiliwa zinaendelea kuchakatwa ili namba zao za utambulisho na vitambulisho vyao vya Taifa vitolewe mapema iwezekanavyo. Pia alisema kutokana na kitambulisho cha taifa kuwa na kisilikoni (Chip) kinachoweza kutumika kama pochi ya fedha ya kielektroniki (E-Wallet), mtu anaweza kukitumia kuhifadhi fedha na kufanya malipo.

Kadhalika, alisema kitambulisho hicho kinaweza kutumika kama kadi ya ATM kwenye maingio ya milango ya kielektroniki (E-Entrace), Daftari la Mahudhurio la Kielektroniki na mwananchi kuondokana na adha ya kubeba utitiri wa vitambulisho.

# Wadhamini wa Lissu wakwama kortini

**Na Beatrice Shayo**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, imeshindwa kusikiliza maombi ya wadhamini wa Tundu Lissu, Ibrahim Ahmed na Robart Katula, kutokana na upande wa mashtaka kutokuwa na jalada la kesi ya uchochezi inayomkabili Mbunge huyo wa zamani wa Singida Mashariki na wenzake.

Ahmed na Robart wamefungua maombi mahakamani wakiomba itoe hati ya kumkamata Lissu kwa kuwa wameshindwa kumpata.

Wakili wa Serikali, Ester Martin, jana alidai hayo mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, kuwa wanaomba tarehe nyingine ya kusikilizwa kwa maombi hayo kwa sababu hawana jalada la kesi hiyo wakati kesi ya msingi ilipopangwa kwa ajili ya kutajwa.

Hakimu Simba alisema hawawezi kufanya jambo lolote kwa kuwa Upande wa Mashtaka hauna faili na kuahirisha shauri hilo hadi Aprili 23, mwaka huu.

Mbali na Lissu, washtakiwa wengine ni wahariri Simon Mkina, Jabir Idrisa na Mchapishaji wa Kampuni ya Jamana, Ismail Mehbooh.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao kwa pamoja wanakabiliwa na mashtaka matano, likiwamo la kuandika habari za uchochezi kinyume cha Sheria ya Magazeti ya Mwaka 2002.

Inadaiwa kuwa kati ya Januari 12 hadi 14, 2016, jijini Dar es Salaam, washtakiwa Jabir, Mkina na Lissu, waliandika na kuchapisha taarifa za uchochezi zenye kichwa cha habari 'Machafuko yaja Zanzibar'.

Katika shtaka la pili, inadaiwa kuwa Januari 14, 2016, walichapisha habari hizo ili kuleta chuki kwa wananchi wa Zanzibar.

Mshtakiwa Mehboob anadaiwa kuwa Januari 13, 2016, katika jengo la Jamana lililoko Manispaa ya Ilala, alichapisha gazeti la Mawio lililokuwa na taarifa za uchochezi.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa huyo pia alichapisha gazeti hilo bila ya kuwasilisha hati ya sheria ya kiapo kwa Msajili wa Magazeti.

# Zungu asema serikali haitafunga viwanda

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu, amesema wizara yake haitafunga kiwanda chochote kwa ukiukwaji wa mazingira.

Badala yake amesema busara zitatumika kuhakikisha kanuni, taratibu na sheria za mazingira zinafuatwa.

Akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya mkutano maalum uliowahusisha Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) pamoja na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Zungu alisema kuwa kufungia kiwanda ambacho kimekiuka kanuni na sheria za mazingira inapelekea serikali kukosa mapato na hata ajira kwa vijana wa kitanzania.

"Malengo ya Rais John Magufuli ni kufikia uchumi wa viwanda ifikapo 2025, hatuwezi kufikia malengo hayo kama tutafikiria kufunga kila kiwanda ambacho kitakiuka sheria na kanuni za mazingira.

Njia ya majadiliano, onyo na faini zinaweza kuleta suluhu bora zaidi bila kuathiri uzalishaji kiwandani na serikali kupata mapato," alisema Waziri Zungu.

Zungu alisema kuwa wizara yake itaendelea kukutana na wadau wa sekta binafsi ili kuendelea kutatua changamoto za kiuwekezaji na kuweka mazingira rafiki zaidi ya ufanyaji biashara hapa nchini.

"Kama wizara kupitia NEMC tutaendelea na utaratibu wa kukutana na wawekezaji na wafanyabiashara ili kuangazia changamoto zilizopo na kuzipatia ufumbuzi hali ambayo itachangia katika kuleta uwazi na uwajibikaji kwa idara zetu," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, aliwataka wadau wa sekta binafsi, wawekezaji na wataalamu elekezi kufanya kazi kwa ukaribu na baraza hilo ili kuondoa kero.

"Suala la utoaji vibali ni mchakato unaoanzia kwa mwekezaji kisha mtaalamu elekezi na mwisho ni NEMC. Matatizo huanza hapo kwa kuwa NEMC

lazima ijiridhishe kabla kibali hakijatolewe. Nitoe wito kwa wadau wote kushirikiana na NEMC kwa hatua zote muhimu ili kurahisisha upatikanaji wa huduma," alisema Dk. Gwamaka.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa TPSF, Godfrey Simbeye, alipongeza jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na serikali katika kuhakikisha mazingira ya biashara na uwekezaji yanakuwa rafiki.

"Utoaji wa vibali kwa njia ya mtandao utaharakisha upatikanaji wake na kupunguza urasimu, lakini hata ufungaji wa viwanda ambao ulikuwa ukifanyika huko nyuma ulionekana kuathiri wawekezaji, wafanyakazi pamoja na serikali, hivyo tunapongeza jitihada hizo na tunaomba majadiliano yawe ya mara kwa mara kati ya serikali na sekta binafsi," alisema.

Mkutano huo maalum kati ya Waziri Zungu na wadau wa TPSF ni mwendelezo wa majadiliano kati ya NEMC na wawekezaji katika kutafuta namna nzuri ya kuondoa changamoto za uwekezaji hapa nchini.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kutumia majanga kujinufaisha sawa na kufurahia vifo

**WAKATI** huu ambao dunia unakabiliwa na tishio kubwa la ugonjwa wa corona, kuna Watanzania kadhaa ambao wanafurahia, na kukitumia tishio hilo kuwa fursa kwao.

Watu hawa ambao ni wafanyabiashara, badala ya kutoa mchango wao na kushirikiana na Watanzania wenzao kuhakikisha kuwa tishio hilo halisababishi maafa nchini, wao wanapandisha bei ya vifaa ambavyo vinatumika kujikinga na maambukizi mara dufu.

Walianza kupandisha bei baada ya vifaa hivyo kama maji tiba (sanitizer) na 'mask' mara dufu baada ya kusikia wananchi wakihamasishwa na kuhimizwa kuvitumia kwa lengo la kukabiliana na kusambaa kwa ugonjwa huo ambao unasababishwa na virusi.

Kitendo hicho kimewaathiri watu wengi kutokana na kushindwa kumudu, huku wakiomba serikali kuchukua hatua za haraka dhidi ya ulanguzi unaofanywa na wauzaji wa vifaa hivyo.

Katika maduka kadhaa ambayo yalitembelewa na waandishi wetu jijini Dar es Salaam kwa mfano wilayani Ubungo, maski moja ilikuwa ikiuzwa kwa gharama ya Sh. 5,000 kutoka Sh. 500, huku maji-tiba (sanitizer) yakiwa yameadimika madukani.

Mmoja wa watoa huduma kwenye duka la dawa eneo la Kimara Baruti, alisema maski hizo zimeadimika dukani kwa sababu wafanyabiashara kutoka China hawajaleta nchini.

Alisema gharama imepanda sana kwa kuwa kabla hazijaadimika, walikuwa wanauza moja kwa Sh. 500, lakini sasa wanauziwa boksi zima kwa Sh. 80,000 badala ya Sh. 5,000 , huku ndani na ndani zinawekwa 50.

Katika duka lingine kwenye eneo hilo, mfanyabiashara wa duka la dawa alisema wananunua maski kutoka kwa watu binafsi ambao wanawauzia kuanzia Sh. 60,000 hadi Sh 100,000 kwa boksi moja.

Kuhusu maji-tiba alisema bidhaa hiyo imeadimika madukani kote, hivyo gharama zake nazo zitakuwa zimeongezeka kwa wauzaji ambao watakuwa nazo.

Alisema awali walikuwa wanauza maji-tiba yenye ujazo wa milimita 25 kwa 250, lakini kwa sasa yanauzwa kwa Sh 5,000.

Sisi Nipashe tunalaani vitendo hivi vya kihuni vya kupandisha bei vinavyofanywa na baadhi ya wauzaji wa vifaa hivyo, kwa kuwa ni kutothamini utu na thamani ya binadamu badala yake kujali fedha na maslahi binafsi.

Tunachokiona ni kuwa watu hao wanatumia majanga kama fursa ya kujinufaisha, huku wakifurahia kuona binadamu wenzao wakipoteza maisha ili waendelee kuuza vifaa hivyo kwa bei ya juu kutokana na kuongezeka mahitaji.

Kimsingi, misingi ya soko huria hairuhusu soko kuingiliwa, ikiwamo serikali kuweka bei elekezi za bidhaa na huduma kwa lengo la kuliacha lijiendeshe lenyewe.

Hata hivyo, katika mazingira yetu, baadhi ya wafanyabiashara wanakiuka misingi hiyo kwa kupandisha bei ovyo badala ya kuacha mahitaji (demand) kutegemeana na usambazaji (supply).

Kutokana na hali hiyo, tunaona kwamba ipo haja kwa sasa kwa serikali kuingilia kati kwa muda ili kuweka mambo sawa.

Ndio maana tunaunga mkono hatua ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu ya kuwataka wafamasia wote nchini kuchangamkia fursa ya kutengeneza vifaa vya kujikinga kama maji-tiba na maski za kuziba pua na mdomo ili kuvisambaza maeneo yote nchini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Salamu za kukumbatiana 'wauu!...' ziachwe kwa muda

Na Sabato Kasika

**KUGUSANA** mwili kwa namna mbalimbali, iwe kupeana mikono au vinginevyo, mara zote inabeba ishara ya 'yuko pamoja' kwa upendo.

Hivyo, zile salamu kwa mtindo wa kukumbatiana, inatajwa kuwa moja ya ishara ya furaha na upendo miongoni mwa watu wa jamii. Waafrika nao tumo. Hiyo ni kawaida kwetu Waafrika, tunapokutana nyumbani, barabarani au sehemu yoyote.

Kukumbatiana na kupeana mikono, ni salamu za jadi zinazoendelea kudumishwa kwenye baadhi ya makabila ya Kiafrika, kizazi kimoja hadi kingine, tukitakiana mema maishani. Watanzania nasi ni sehemu ya hilo.

Sasa imeibuka corona, ugonjwa wa kuambukiza, unaoilazimu jamii kuachana kwa muda mambo ya kugusana pasipo lazima.

Virusi vya corona, wataalamu wanatuambia ni tatizo kubwa linaloikabili dunia na tayari serikali imeshatangaza, Mtanzania mwenzetu mmoja tayari ana virusi vyake, hali inayotupa shaka, baadhi wanaangukika taharuki.

Kabla ya kugundulika mgonjwa mwenye virusi vya corona nchini, serikali ilishatahadharisha na kuwapa Watanzania maelekezo ya nini cha kufanya, ili kujikinga na ugonjwa huo.

Hapo kuna suala la kusalimiana pasipo kugusana. Pamoja na maelekezo hayo, bado wapo baadhi ya watu hawajaanza kuzingatia hilo.

Hii inatokana na ukweli kwamba kwenye mikusanyiko ya watu ikiwamo vitu vya mabasi, baadhi ya watu wamekuwa wakisalimiana kwa kukumbatiana na kushikana mikono kama kawaida.

Wanafanya hivyo huku kukiwa na maelekezo yaliyotolewa na serikali kana kwamba ni jambo la kawaida, wakati wakijiingiza kwenye hatari aidha kwa kujua ama kwa kutojua.

Lakini, pamoja na yote, jambo la msingi ni kuzingatia maelekezo, ingawa kuna baadhi waliozoea kusubiri hadi washuhudie ndipo wachukue hatua na kumbe tayari wamechelewa.

Kwa hali ilivyo sasa, salamu za kukumbatiana zikome kwa muda, kupisha udhibiti wa kuenea corona na ndipo mambo mengine yaendelee, kuliko kung'ang'ania hatari, kuliko kung'ang'ania mbwembwe za uhusiano, sakata likiwa sehemu yake. Viongozi wakuu wa nchi wameitikia maelekezo hayo na wameanza kuyafanyia kazi mara moja. Hivyo, sioni hivyo kwa nini wengine tubaki katika mzaha.

Mara tu baada ya maelekezo, Rais na Waziri Mkuu wametuonyesha mfano vitendo, kufuata maelekezo ya Wizara ya Afya, Meandeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kuhusu tunachopaswa kufuata kutetea uhai wetu.

Virusi vya corona vilikuwa vinatajwa katika nchi nyingine na sasa ni hapa hapa nyumbani. Ndipo swali langu la msingi linachukua nafasi yake, wale wasiotaka kuachana na salamu za kukumbatiana na kushikana mikono, wanatafuta nini?

Hadi juzi tumeona hatua zaidi za kiserikali, shule zimefungwa kwa muda. Ni jitihada za kuwanusuru wanafunzi na jamii zao dhidi ya ugonjwa huo.

Ndugu zangu, hatua hizi ziwazindue wale ambao ni wagumu kuzingatia maelekezo, walioyapa uzito maneno ya mitaani ama kwa kupuuzia au kutiana hofu bila sababu za msingi.

Mtindo wa kuchukua maneno ya vijiweni na kuyafanyia kazi bila kuchukua hatua zinazotakiwa, ni sawa na kujiangamiza. Hivyo, kwa kuwa ugonjwa umetajwa kuwapo nchini, tahadhari kubwa zinatakiwa kuchukuliwa.

Siyo wakati wa kuambiana kuwa 'kama Mungu amekupangia kufa kwa virusi vya corona utakufa tu', bali kufuata maelekezo, ikiwamo kuacha salamu za kukumbatiana na kupeana mikono.

Uzembe uachwe kwenye mambo ya hatari kama hayo. Kila mmoja wetu achukue hatua kwa nafasi yake, inagawa inawezekana kuwapo changamoto, katika sura mbalimbali, kulingana na maazingira ya kila mmoja wetu.

Maelekezo kwamba watu wasikumbatiane na wasipeane mikono yasipite bure, bali yazae matunda katika vita hii dhidi ya corona.

Pia, ni vyema kukumbuka kwamba dhana 'mazoea yana taabu' na yanaweza kukuingiza kwenye matatizo. Ni wakati wa kuishi kulingana na mazingira na jinsi dunia inavyokwenda, kama ambavyo sasa inapambana na virusi vya corona.

Kila mmoja kwa njia moja ama nyingine ana nafasi ya kushiriki katika vita dhidi ya virusi hivyo, madaktari wanafanya sehemu yao, na wananchi kwa upande wao, wanatakiwa kuzingatia maelekezo ya wataalamu hao wa afya.

## BARUA & MJADALA

# Tujipange kwa vita corona

**Mhariri,**

*HIVI sasa katika kila mahali nchini ni hekaheka iliyojaa hofu. Sababu kuu ni homa ya corona, ambayo imevuka mabara kadhaa, ikagonga hodi Afrika na sasa imetufikia.*

*Si jambo jema. Huwa tunakumbushana kwa kumwomba Mwenyezi atuepushe mbali na janga hilo, ambalo halina sura ya kuwa na dalili nzuri kwetu wanajamii nchini, kama tulivyoshuhudia kilichojiri huko ughaibuni inakotambaa, kuanzia safari yake kwa Wachina.*

*Kama ilivyo kanuni ya changamoto yoyote duniani, mara zote mtu unapambana na tatizo kadri ilivyo kiwango cha uhalisia wake.*

*Sasa tumeshathibitishiwa kitaifa kwamba maradhi yako kwetu na tunachopaswa kufanya, ni namna ya kuangalia tutayakabili vipi.*

*Namna ya kupewa mbinu stahiki, ni namna moja na utekelezaji wa mbinu hizo ni jambo la pili, kabla ya kusonga zaidi kwamba, ikiendana na mambo zaidi kama vile kutoa ushirikiano katika kufanikisha vita ya azma iliyo mbele yenu.*

*Ikiwa ni askari, basi wanatia jina la operesheni maalum katika ufanikishaji lengo tajwa, hadi kufikia mahali wanakokusudia, katika mpango walionuia kuufanikisha.*

*Ni katika mtazamo huo, basi una haja ya kuwapo kunuia na kufanikisha lengo tajwa katika vita ya kukomesha corona kabla ya kuathiri wengi kitaifa na inakuwa na manufaa katika sura ya kitaifa na kimataifa.*

**Sudi Mwameda,**
**Muheza.**

**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz




# Vyoo vya kukaa ni maendeleo, lakini...

**Na Sabato Kasika**

KUNA msemo wa lugha na kiafya 'nyumba ni choo,', maana hapo ni kwamba, ujenzi wa nyumba usiokuwa na choo, bado unakuwa haujakamilika.

Wanajamii wengi kutokana na sababu mbalimbali, iwe kiuchumi na kijamii, wamezoea vyoo vya kuchuchumaa, ingawa kuna ukweli kadri miaka yainavyosonga, kuna mageuzi ya kusogelea vyoo vya kukaa.

Ni vyoo vimekuwa vinaonekana kuwa ishara ya ustarabu na maendeleo katika jamii ya Kiafrika na zaidi viko mijini, kuanzia nyumbani, ofisini, hotelini na hata katika majengo mengine.

Hata nyumba na ofisi mbalimbali zinazoendelea kujengwa mijini kwa sasa, zinawekwa vyoo vya kukaa, kwa vile inaelezwa kuwa kukaa wakati wa kujisaidia ni sehemu ya ustaarabu na maendeleo.

Kwa ujumla, ni kwamba vyoo vya kukaa siyo vya kwanza, bali ni mwendelezo wa vile vya kuchuchumaa, kwa maana ya kuboresha huduma hiyo pasipo kuchoka.

Pamoja na ustaarabu huo, inaelezwa kitaalamu kujisaidia kwa kutumia choo cha kukaa, kuna madhara kiafya. Ni mkao unaoweza kusababisha magonjwa mbalimbali, iwapo kitatumiwa na watu wengi.

Mtaalamu bingwa wa Magonjwa ya Ndani kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili, Dk. Nzobendo Lucas anatahadharisha vyoo hivyo vinatumika kujisitiri na kulinda afya za watu wa eneo husika, pia kisigeuke chanzo cha madhara ya matumizi yasiyozingatia usafi.

Anadokeza kuwa matumizi yasiyozingatia usafi, yana madhara, ikiwamo kuambukiza ugonjwa homa ya ini, mkojo mchafu au UTI, Ukimwi na magonjwa kadhaa ya zinaa na ngozi, hasa maeneo ya makalio.

Homa ya ini inaambukiza kwa njia ya damu, hivyo umakini unahitajika katika matumizi ya vyoo vya kukaa, ili kuepuka magonjwa tajwa.

Dk. Lucas anafafanua kuwa, mtu mwenye homa ya ini akiwa na vidonda kwenye makalio na kwenda kujisaidia, anaacha damu ambayo ni rahisi kumuambukiza mwingine mtumiaji wa choo hicho.

Pia, anakumbusha kuwa bakteria hawapatikani tu kwenye eneo la kukalia, pia kwenye maji yanayobaki baada ya kutumia choo, hivyo cha muhimu ni kusafisha choo kabla ya kukitumia, kukwepa maambukizi hasa katika maeneo ya faragha ya mtumiaji.

Dk. Nzobendbo anasema hamaanishi kupinga hitaji la vyoo vya kukaa, bali ana ujumbe kwa umuhimu wa matumizi salama, kwa kuzingatia kanuni za usafi.

Kimsingi, kuna hatua kadhaa ambazo mtu anapaswa kuchukua kabla ya kujisaidia kwenye choo cha kukaa, ili kuwa asakama na maambukizi ya magonjwa, yakiwamo aliyoyataja.

"Kutokana na vyoo kutumiwa na watu wengi, ni vyema kufunua mfuniko kwa kutumia karatasi laini, ili kuzuia bakteria waliopo sehemu ya kukalia wasipenye kwenye mikono yako," anasema.

Anasema ni hatua muhimu kujikinga na UTI na kwamba, hatua inayofuata ni kusafisha eneo la kukaa kwa karatasi laini iliyolowekwa kwa dawa au sabuni ya maji ya kuua wadudu.

Hii inaitwa 'toilet seat sanitizer' inayoua bakteria walioachwa na wengine wakati wakijisaidia, ingawa bakteria hawapatikani tu katika eneo la kukalia, bali hata kwenye majimaji yanayobaki baada ya kutumia choo.

Kufunika eneo la kukaa kwa kitambaa au karatasi laini ni njia nyingine ya kuzuia bakteria kuingia mwilini kupitia njia ya mkojo na hutumika kama mtu hana dawa ya kusafisha eneo la kukaa au vyote kwa pamoja ili kujihakikishia ulinzi zaidi.

Elimu ya kitaalamu, ikiwamo toka kwa Dk. Lucas ni kwamba, choo bora kukitumika ipasavyo, ni hitaji muhimu kwa kila binadamu kwa afya yake na usafi wa mazingira, ili kuepuka maambukizi ya magonjwa ambayo wakati mwingine yanasababishwa na kinyesi.

"Kimsingi katika maisha ya kila siku, nyumba haiwezi kuwa kamili bila kuwa na huduma ya choo, na kwa kutambua umuhimu huo, ni vyema watu wakawa makini katika matumizi yake ili kupusha madhara," anasema mtalamu huyo.

Kwa kinamama, anasema uwezekano wa kupatwa maambukizi ya njia ya mkojo uko juu zaidi, kutokana na maumbile yao na wengine tatizo hilo huwa linawarudia kila mara.

Anasema, kuna wakati ugonjwa huo ukawa unajirudia kutokana na mtumiaji kutoelewa jinsi ya kujisafisha, mara baada ya kujisaidia, lakini ni muhimu kuzingatia maelekezo ya wataalamu.

Wataalamu wanadai si mijini tu, bali hata vijijini na kwa sasa maji wanayotumia zaidi, hivyo inahimiza jamii kutambua njia sahihi ya kuepuka maradhi hayo ya UTI, ambayo sasa yametapakaa kila sehemu nchini.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed





Wakazi wa Kijiji cha Isoliwaya, Kata ya Ihimbo, wilayani Kilolo, mkoani Iringa, wakiendelea na utamaduni wa kunywa pombe aina ya ulanzi kwa kupokezana kikombe cha lita maarufu kama "kilita" licha ya kuwapo kwa tishio la maambukizi ya virusi vya corona nchini.
**PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Zanzibar sasa yafunga vyuo, shule

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imezifunga shule zote, vyuo vikuu pamoja na madrasa ili kupunguza uwezekano wa maambukizi ya maradhi ya corona hadi hapo serikali itakapotoa tangazo lingine.

Hatua hiyo imetokana na kupatikana kwa mgonjwa mmoja mwenye maambukizi ya kirusi cha corona ambaye ni raia wa Ujerumani, mwanaume mwenye umri wa miaka 24.

Waziri wa Afya, Hamad Rashid Muhamed, alisema mtu huyo aliingia nchini kutokea Ujerumani kwa usafiri wa ndege ya Shirika la Ndege la Kenya Machi 13, mwaka huu.

Alieleza Machi 17, Zanzibar ilikuwa na washukiwa watatu wa ugonjwa huo ambao wawili wakiwa raia wa kigeni wa Ghana na Ujerumani na mwingine ni Mtanzania, lakini walifanyiwa uchunguzi na mmoja kugundulika kuwa na virusi vya ugonjwa huo. Alieleza kuwa kwa sasa mgonjwa huyo amelazwa katika kituo maalum kilichotengwa kwa ajili ya maradhi ya mlipuko eneo la Kidimni Wilaya ya Kati Unguja kwa ajili ya matibabu, na hali yake inaendelea vizuri.

Waziri huyo alieleza kuwa pia serikali inazuia mikusanyiko inayokutanisha watu wengi kwa wakati mmoja ikiwamo mikutano, makongamano, semina, warsha, michezo ya ligi kuu, ligi za kanda pamoja na burudani za ngoma na shughuli za harusi mpaka hali itakapotengemaa.

"Hata hivyo, shughuli za msiba zihusishe watu wachache kadri iwezekenavyo... pia serikali inawataka watu wote wanaoingia nchini kutoka nchi zilizoathirika na maradhi hayo kufuata utaratibu wa kujitenga kwa hiyari kwa muda wa siku 14 kwa gharama zao pamoja na kufuata masharti ya afya," alisema.

Aidha alisema serikali inakataza na kukemea utumiaji wa bandari zisizo rasmi kwa ajili ya kuchukua abiria na mizigo, hivyo watu wote wanatakiwa kutumia bandari rasmi na vyombo vitakavyotumika nje ya bandari zisizo rasmi vitataifishwa na serikali. Hamadi alieleza kuwa pia serikali inalaani vikali vitendo vya wafanyabiashara kutumia ugonjwa huo kwa maslahi yao binafsi kwa kupandisha bei vifaa vya kinga, bidhaa na huduma nyingine, na kwamba hatua kali zitachukuliwa dhidi ya watakaobainika kufanya hivyo.

"Serikali inazuia safari zote za nje ya nchi kwa watendaji wake, na pia kwa wale watakaokuwa na ulazima wa kusafiri wanapaswa kuchukua hatua za kujilinda na maradhi hayo... niwaombe wananchi kuepuka safari zisizo za lazima za nje ya Zanzibar," alisema.

Pia aliwataka wananchi wanaokwenda sokoni na maeneo mengine ya kutafuta huduma kuepuka mikusanyiko, na baada ya kupata huduma warudi majumbani.

# Zitto adai wakili kumfurahisha taarifa kifo mwandishi Azory

**Na Beatrice Shayo**

KIONGOZI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, amedai kufurahishwa na Wakili wa Serikali kukiri Mwandishi wa Habari, Azory Gwanda, amefariki dunia.

Suala hilo lilijitokeza jana wakati Zitto akijitetea kwenye Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam mbele Hakimu Mkazi, Huruma Shaidi.

Zitto akihojiwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Nassoro Katuga, kuhusu kauli yake inayodaiwa ya uchochezi aliyoitoa katika mkutano na vyombo vya habari.

Katuga alimuuliza Zitto kuhusu njia za kufikisha ujumbe kwa serikali na akajibiwa na mwanasiasa huyo kuwa miongoni mwake ni kupitia vyombo vya habari.

Katunga alimtaka Zitto kueleza kwa namna gani wananchi walihusika kwenye ujumbe huo ikiwa alilenga serikali na Jeshi la Polisi. Zitto alidai kwa mujibu wa Katiba, serikali ni ya wananchi, hivyo nao wana wajibu wa kupata taarifa.

Wakili huyo alimuuliza Zitto kwanini anashtakiwa kwa kutoa maneno ya uongo na mshtakiwa huyo akadai hakushtakiwa kwa kusema maneno ya uongo, bali kwa uchochezi.

Wakili Katuga akamuuliza kwanini asishtakiwe kwa kueleza habari za kifo cha Ben Saanane au Azory Gwanda.

Zitto alijibu: "Mheshimiwa Hakimu, nimefurahi kusikia Wakili wa Serikali amesema kuwa kweli Azory Gwanda amefariki dunia."

## DC Kinondoni apiga marufuku 'tuition'

**Na Elizabeth Zaya**

MKUU wa Wilaya ya Kinondoni, Daniel Chongolo, amepiga marufuku ya mikusanyiko ya wanafunzi kwa ajili ya masomo ya ziada (tuition) katika maeneo yote.

Akihojiwa kwenye kipindi cha Kumekucha cha ITV, alisema serikali tayari imeshatoa maelekezo ya kufunga shule zote nchini, hivyo kuanzisha tena masomo hayo ya ziada ni sawa na kuanzisha shule nyingine ambayo ni hatari zaidi na kwenda kinyume cha maelekezo yaliyotolewa.

"Niwaombe wazazi wasiruhusu watoto wao kutoka ndani kwenda nje, ni vyema wakabaki ndani, na yeyote atakayebainika kwamba amewakusanya wanafunzi kwenye masomo ya ziada hatutamvumilia, tutamchukulia hatua kali," alisema Chongolo.

"Serikali imeamua kufunga shule ili kuwaepusha wanafunzi na janga, halafu tena watu wengine waanzishe tena shule nyingine mtaani huko ambako tena ni hatari zaidi kwa sababu hakuna usimamizi, kwa kweli watu wa namna hii hatutawavumilia."

**WAFANYABIASHARA WAPEWA MAELEKEZO**

Chongolo aliwaagiza wamiliki wa maduka ya dawa yenye bidhaa za kutumika kusaidia kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huo ikiwamo maji tiba (sanitizer) na nyinginezo, kubandika bei ya bidhaa hizo mlangoni badala ya kuziuza kama za magendo.

"Baada ya kutangaza kuingia kwa ugonjwa huu nchini, wafanyabiashara wamependisha bei bidhaa za kusaidia kujingika ikiwamo vitakasa mikono. Niombe kwamba duka la dawa lenye bidhaa hizi zibandike mlangoni bei zake na mimi nitapita kukagua kote, hatuwezi kutumia mwanya huu kuwaumiza wananchi, na wasiziuze kama magendo," alisema Chongolo.

**VIKAO VYA HARUSI**

Alisema ni vyema wananchi wa wilaya hiyo wakajizuia kuweka mikusanyiko kupitia shughuli hizo. "Hivi kweli katika mazingira haya mnaenda kukaa kwa ajili ya vikao vya harusi, bahati mbaya sana tunajitengenezea utamaduni wa ajabu sana.

Kwa mfano ningekuwa mimi katika familia yangu ndiyo tunaoza au kijana anaoa, ningeshukuru Mungu kwamba tumepata fursa ya kufanya shughuli bila mbwembwe," alisema Chongolo.

**BAA**

Chongolo alisema si lazima mtu aende baa badala yake anaweza akafika hapo na kununua.

HABARI KITAIFA

# Viongozi wa dini wakutana kuliombea taifa

**Na Hamisi Nasiri, MASASI**

VIONGOZI wa dini wilayani Masasi, mkoani Mtwara wamekutana na kufanya maombi ya pamoja ya kumuomba Mwenyezi Mungu aweze kuliepusha taifa na virusi vya ugonjwa wa corona.

Wadau wengine ambao walialikwa katika kikao hicho cha dharura ni viongozi wa taasisi za umma, wafanyabiashara, wazee maarufu, mamwinyi, viongozi wa vyama vya siasa, watendaji wa Idara ya Afya na wakuu wa kamati ya ulinzi na usalama.

Viongozi hao walifanya maombi hayo jana wilayani hapa na baada ya kumalizika kikao cha dharura kilichoitishwa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Selemani Mzee, kwa ajili ya kujadili na kuweka mkakati wa kutoa elimu kwa jamii kuhusu kuzingatia njia za kujikinga na ugonjwa huo.

Sheikh Mnung'a Mohamed, Mwenyekiti wa Baraza la Waislamu Tanzania (Bakwata), Masasi alisema virusi vya ugonjwa wa corona ni janga la kidunia hivyo jambo kuu ni kila Mtanzania kumwomba Mungu aweze kuliepusha taifa dhidi ya ugonjwa huo.

Alisema serikali kupitia vyombo husika iendelee kutoa elimu kwa jamii kuhusu njia sahihi za kujinga na virusi vya corona kwa vile bado maeneo ya vijijini elimu hiyo haijatolewa.

Mchungaji wa Kanisa la Agape Mtandi Masasi, Monica Kasembe, alisema wakati huu jamii ina ulazima wa kupata uwelewa wa kutosha wa mara kwa mara ya ufahamu wa njia za kujikinga na ugonjwa huo hatari na kila mwananchi akifahamu vyema elimu ya kujikinga itasaidia kuepusha maambukizi mapya.

Mchungaji wa Kanisa la Morivian Masasi, Canon Doglaus, alisema iwapo elimu itatolewa kwa upana zaidi jamii itabadili mwenendo na kuona sasa kuna umuhimu wa kuchukua tahadhari dhidi ya virusi hivyo.

Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Mzee alisema viongozi wa dini wanayo nafasi kubwa katika jamii, hivyo watumie kutoa elimu kwa jamii kuzingatia kanuni za kujikinga na virusi vya ugonjwa huo.

"Nimewaita hapa leo ili kwa pamoja tupeane uelewa wa pamoja na tuone tunaifikiaje jamii katika kutoa elimu hii ya namna ya kujikinga na virusi vya corona viongozi wa dini na sisi wote kwa pamoja tushirikiane kuhakikisha tunafikisha elimu hii ya kujikinga na ugonjwa huu," alisema Mzee.

Naye Mganga Mkuu wa Hospitali wa Hamashauri ya mji wa Masasi Mkomaindo Salumu Gembe, alisema tayari kwa upande wa Wilaya ya Masasi wameshajiandaa kukabiliana na kudhibiti virusi vya ugonjwa huo.

Alisema moja ya mkakati ambao wamejiwekea kuhakikisha ugonjwa huo unadhibitiwa ni pamoja na kutoa elimu katika makundi yote katika jamii ikiwamo kufika kwenye maeneo ya ibada, taasisi mbalimbali ili kujikinga na maambukizi.



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Utawala Bora na Serikali za Mitaa, Dk. Jasson Rweikiza, akiangalia moja ya kazi anazofanya Edith Makalah, mkazi wa mtaa wa Sokoine mjini Singida, baada ya kujikomboa kwa kununua cherehani mbili kutokana na fedha za mpango wa kunusuru kaya maskini kupitia Tasaf. **PICHA: ELISANTE**

# Fisi avamia mgodi na kujeruhi walinzi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WALINZI wawili wa mgodi wa madini ya almasi Mwadui, unaomilikiwa na Kampuni ya Wiliamson Diamondu, wilayani Kishapu, mkoani Shinyanga, wamejeruhiwa na fisi ambaye aliingia ndani ya mgodi huo na kuanza kuwashambulia.

Tukio hilo limetokea juzi majira ya saa 5 usiku katika mtaa wa Line Polisi, wakati walinzi hao wakiwa doria pamoja na wenzao watano na fisi huyo kuvamia mgodini humo. Walinzi hao walipoanza kumpiga marungu, fisi huyo aliwageukia na kuwajeruhi walinzi wawili.

Akitoa taarifa hiyo jana, Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Deborah Magiligimba, aliwataja walinzi waliojeruhiwa kuwa ni Geofrey Zabron (23), ambaye amejeruhiwa mkono wa kushoto, pamoja na Modester Ngassa (30), aliyejeruhiwa paja la mguu wa kulia.

"Walinzi hawa wawili waliojeruhiwa na fisi, wamelazwa katika hospitali ya mgodi huo wa Mwadui kwa ajili ya kupatiwa na matibabu, na hali zao tumezifuatilia zinaendelea vizuri," alisema Magiligimba.

Alisema fisi huyo alikimbia baada ya kuzidiwa nguvu na walinzi, ambao waliongeza nguvu kwa kumpiga.

# Mapendekezo kutungwa sheria matumizi mitandao

**Na Mbaraka Kambona**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria imeiagiza Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) kwa kushirikiana na Taasisi ya Haki Maendeleo, kuandaa mapendekezo yatakayosaidia kuanzishwa kwa mchakato wa kutungwa kwa sheria ya kulinda haki za mtumiaji wa huduma za mifumo ya kimtandao na kuyawasilisha kwa kamati hiyo ili waweze kushawishi Bunge na mamlaka nyingine husika ili sheria hiyo iweze kutungwa.

Maelekezo hayo yalitolewa na Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Emmanuel Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini kufuatia mada kuhusu haki za binadamu na mitandao iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Haki Maendeleo, Dk. Abdallah Mrindoko, katika warsha ya siku moja iliyoandaliwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa kushirikiana na Taasisi ya Haki Maendeleo kwa wabunge wa kamati hiyo iliyofanyika mkoani Morogoro.

Mwakasaka alisema kuna haja ya kuwa na sheria itakayolinda usiri wa taarifa za mtumiaji wa huduma zinazotumia mifumo ya kimtandao kwa kuzingatia kuwa mifumo hiyo inachakata taarifa za mtumiaji na kuzisambaza jambo ambalo linaibua haja ya kutungwa kwa sheria hiyo.

Mapema wakati akitoa mada hiyo, Dk. Mrindoko alitaja changamoto kubwa inayowakumba watumiaji katika kipindi hiki cha maendeleo ya teknolojia ya mtandao ni uwapo wa taasisi nyingi zinazojihusisha na utunzaji na uchakataji wa taarifa katika mfumo wa kidijitali bila kuwapo na sheria ya kulinda haki hizo za mtumiaji.

Vile vile, Dk. Mrindoko alisema ili thamani ya matumizi ya mitandao iweze kutambulika vizuri ni muhimu kuwa na sera na sheria itakayosimamia ulinzi wa haki za mtumiaji nchini.

Alisisitiza mapinduzi ya huduma ya kifedha kwa njia ya mitandao ya simu imeibua changamoto nyingi zinazohusiana na ulinzi wa haki za mtumiaji, akisema kuwa jukwaa hilo limeleteleza mwingiliano kati ya kampuni za mawasiliano na taasisi za kifedha, mazingira ambayo yameibua hoja ya kuwapo sheria ya kusimamia masuala hayo.

"Mazingira yaliyopo sasa yametengeneza ombwe la kisheria kufuatia kuwapo kwa pande mbili ambazo ni kampuni za simu na taasisi za kifedha zinazosimamia masuala ya kifedha mitandaoni ambapo kila mmoja ana mipaka yake kiutendaji," alisema Dk. Mrindoko.

"Wakati matumizi ya simu katika kutuma na kupokea pesa kumesababisha ukuaji na urahisi wa mzunguko wa masuala ya kifedha, bado kuna changamoto nyingi zinazohusu mustakabali wa mtumiaji ambazo zinahitaji kupatiwa ufumbuzi," aliongeza Dk. Mrindoko.

Alisema maendeleo katika matibabu ya afya ya kimtandao na kitambulisho cha uraia vimeleta maswali mengi kuhusu ulinzi na usiri wa taarifa za mtumiaji, akipendekeza kuwa mambo yote hayo inabidi yawe katika mfumo mmoja ambao utalinda usiri na taarifa za mtumiaji.

Akichangia majadiliano katika warsha hiyo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Profesa Sifuni Mchome, alikiri kuwa ni muhimu kuwa na sheria zinazolinda usiri na taarifa za mtumiaji huku akisema kuwa mchakato wa kutungwa sheria hiyo hivi sasa ipo katika mchakato wa kutungwa ili iweze kutumika.

# Ewura yatakiwa kudhibiti wauza mafuta kinyemela

**Na Shaban Njia**, KAHAMA

WANANCHI wa kijiji na kata ya Ulowa, Halmashauri ya Ushetu, wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, wamesema wako hatarini kupata majanga ya moto kutokana na baadhi ya wafanyabiashara wa kata hiyo kuuza mafuta ya petroli na diseli, holela.

Walisema licha ya kuwapo kwa kituo cha mafuta, baadhi yao wanaendelea kununua na kuuza mafuta kinyemela huku wengine wakiwa na zaidi ya lita 400 za mafuta ya petroli na dizeli ndani ya nyumba wanazoishi na familia zao.

Wameiomba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Nishati na Maji (Ewura), kutoa elimu kwa wananchi wa kata hiyo ili kudhibiti majanga ya moto ambayo yanaweza kujitokeza wakati wowote.

Aloyce Jacobo, mkazi wa kata hiyo, alitoa tahadhari hiyo jana wakati alipokuwa akizungumza na vyombo vya habari muda mfupi baada ya uchangiaji wa ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa na bweni kwa ajili ya wanafunzi wa kike sekondari ya Ulowa, unaugharimu Sh. milioni 133 huku nguvu za wananchi ikiwa Sh. milioni 15.

Alisema, wapo wafanyabiashara wanaishi ndani na mafuta ya petroli na dizeli zaidi ya lita 140, pipa 40 pamoja na lita 80, huku wakijua linaweza likatokea janga la moto na kusababisha maafa kwa familia zao na watu wanaowazunguka.

Diwani wa kata hiyo, Paschal Mayengo, alikiri kuwapo kwa baadhi ya wafanyabiashara wa kata hiyo wanauza mafuta ya petroli na dizeli kinyemela.

"Tulikaa vikao na kukubaliana wakachukue maeneo nje ya mji na kufungua biashara zao huko, lakini walikwenda na kurudi na kudai wanakosa wateja na wanaweza kuvamiwa na waporaji na kunyang'anywa fedha zao za mauzo na sasa wapo tena kwenye makazi yao na biashara zinaendelea," alisema.

Naye Meneja Mawasiliano na Uhusiano wa Ewura, Titus Kaguo, alisema kuishi na mafuta ndani ni hatari na sheria inawataka wao kudhibiti kuanzia ngazi ya chini kwa kusaidiwa na Jeshi la Polisi.

Alitoa mfano wa tukio la Morogoro, na kuahidi kufika katika Kata ya Ulowa na kutoa elimu kwa wafanyabiashara hao, kwa kuwa kununua na kuuza mafuta kinyemela ni kesi ya uhujumu uchumi.



Mwekahazina wa Shirikisho la Vyama vya Magonjwa yasiyoambukiza, Dk. Tatizo Waane (kushoto), akizungumza na Wahariri Watendaji wa magazeti ya The Guardian, Wallace Maugo (kulia) na Nipashe, Beatrice Bandawe (wa pili kushoto), alipotembelea ofisi za kampuni ya The Guardian Ltd, Mikocheni, jijini Dar es Salaam juzi. Wa (pili kulia) ni Mwandishi wa Habari, Leon Bahati. **PICHA: ROMANA MALLYA**

# TANCDA kuelimisha jamii magonjwa yasiyoambukizwa

**Na Romana Mallya**

SHIRIKISHO la vyama vya magonjwa yasiyoambukiza (TANCDA), limesema kutokana na ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza, wameamua kutoa elimu kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kuwapima bure na wanaobainika huwaunganisha na vituo vya afya.

Kwa Tanzania, inakadiriwa magonjwa hayo yanasababisha asilimia 27 ya vifo vyote na utafiti wa mwaka 2012 ulionyesha, kila watu 100 wenye miaka 25 na kuendelea, tisa wana kisukari, 26 wana shinikizo la damu, 25 wana mafuta yaliyozidi kwenye damu na 34 wana uzito uliozidi. Mwekahazina wa Shirikisho hilo, Dk. Tatizo Waane, aliyasema hayo jana katika ofisi za The Guardian, zilizopo Mikocheni jijini Dar es Salaam baada ya kuzitembelea na kuzungumza na wahariri pamoja na waandishi wa habari.

Waane ni Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Moyo, alisema kuwa, shirikisho hilo limejikita kujenga uwezo kwa makundi mbalimbali kwenye jamii kuwa na uelewa wa magonjwa hayo.

"Kazi mbalimbali tunazofanya ni pamoja na kufanya upimaji bure na kuwajengea uelewa wananchi. Tunafanya haya katika mikoa mbalimbali ikiwamo ya Kanda ya Ziwa, Kaskazini na Mashariki.

"Tumefanya upimaji na kuwajengea uelewa wanafunzi kutoka vyuo mbalimbali na sasa tuna mradi wa kutoa mafunzo kwa wanafunzi wa kike ili wapate uelewa."

Pia Dk. Waane alisema wanafanya kazi pamoja na Chama cha Waandishi wa Habari wanaoandika habari za magonjwa yasiyoambukiza ili iwe rahisi kufikisha ujumbe kwenye jamii.

"Tumekuja hapa The Guardian kuwajulisha kuwa shirikisho hili lina wataalamu waliobobea kwenye magonjwa yote hivyo wakati mkiandika habari au makala, mnapotaka mtaalamu, mnaweza kuwasiliana nao ili kufikisha ujumbe sahihi na kubadilisha mfumo wa maisha kwenye jamii.

"Chanzo cha magonjwa yasiyoambuliza kuongezeka kinachangiwa na mfumo wa maisha tunaoishi hivi sasa, shirikisho limejikita pia kutoa elimu kwa wanafunzi ambao ndiyo kizazi kijacho ambacho kikielimika kitasaidia kupunguza kasi ya magonjwa haya Tanzania."

Mhariri Mtendaji wa Nipashe, Beatrice Bandawe, alilishukuru shirikisho hilo kwa kutambua mchango wa vyombo vya habari katika kuielimisha jamii na kutoa fursa kwa wataalamu hao wa afya kushiriki kwa kuandika makala za kuelimisha.

"Gazeti la Nipashe ni mdau mkubwa wa sekta ya afya kwa sababu zinagusa moja kwa moja jamii, tunawakaribisha wataalamu wa shirikisho lenu waweze kuchangia uelimishaji huo kwa kuandika makala mbalimbali za afya," alisema.

Naye, Mhariri Mtendaji wa gazeti la The Guardian, Wallace Maugo, alisema vyombo vya habari vina jukumu kubwa la kuielimisha jamii na elimu hiyo inahitaji wataalamu waliobobea sekta mbalimbali.

"Mnakaribishwa kuchangia mawazo katika sekta hii kupitia utaalamu mlionao, andikeni makala zenye kuelimisha jamii ambazo zitachapishwa kama habari nyingine, milango ipo wazi," alisema.

Kitabu cha TANCDA chenye kichwa 'Mtindo wa maisha na magonjwa yasiyoambukiza' kimefafanua magonjwa yasiyoambukiza ni yale yasiyo na vimelea vinavyoweza kusambazwa.

Kimeyataja baadhi ya magonjwa hayo kuwa ni moyo na mishipa ya damu, saratani, magonjwa sugu ya njia ya hewa, kisukari na selimundu.

Pia kitabu hicho ambacho kimetaja dalili, athari na kinga kina takwimu za mwaka 2016 ambazo zinaonyesha watu milioni 42 (sawa na asilimia 71 ya vifo vyote) walifariki duniani kutokana na magonjwa yasiyoambukiza.

Kadhalika, kinasema asilimia 75 ya vifo vyote vinavyohusu watu wenye miaka 30 hadi 70 husababishwa na magonjwa hayo.

Kinautaja utafiti wa miaka 1986/87 ambao unaonyesha kuwa ni mtu mmoja tu kwa kila 100 alikuwa na kisukari na watano kwa kila 100 alikuwa na shinikizo la damu.

## Walimu wahofu kushika madaftari kisa corona

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA UJIJI

BAADHI ya walimu wamesema wamekuwa na hofu ya kupata maambukizo ya virusi vya corona kupitia usahihishaji wa madaftari ya wanafunzi.

Hofu hiyo ilibainishwa wakati Manispaa ya Kigoma Ujiji ikiendelea na utoaji elimu kuhusu ugonjwa wa corona ulioanza Machi 15 mwaka huu.

Mwalimu wa Shule ya Sekondari Wakulima, Mubaraka Fumbo, alisema kutokana na elimu waliyopewa kuhusu namna virusi hivyo vinavyoweza kukaa kwa muda mrefu katika sehemu mbalimbali, anaona walimu wako katika hatari kubwa ya kupata maambukizo hayo.

"Tumeambiwa virusi hivyo vinakaa kwenye nguo, sasa tahadhari tumeshapewa, sisi kama walimu tutafanyaje kukabiliana na jambo hilo kama vinaweza kukaa hata kwenye madaftari?" Alihoji.

Mratibu wa Ukimwi Manispaa ya Kigoma Ujiji, Dk. Shabani Mgolwa, alisema katika kukabiliana na ugonjwa huo, wameandaa mazingira bora ya sehemu ya karantini katika Zahanati ya Bangwe na kuweka vipimo katika moja ya eneo la stendi ya mabasi.

Alisema katika utoaji elimu, wamebaini kuwa uelewa wa wananchi juu ya ugonjwa wa corona bado ni mdogo, hivyo kuna haja kuongeza jitihada za utoaji elimu hiyo katika maeneo yanayokusanya watu wengi na kuhamasisha kila anayeipata kuwa balozi kwa wengine.

"Tumeamua kuwekeza zaidi katika kutoa elimu kwa wanafunzi sababu kwanza ni wahanga wa jambo hilo na pia ni wajumbe wazuri katika kufikisha taarifa," alisema.

# Gambo ataka ubunifu matumizi mawasiliano

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, amesema kutokana na kukua kwa sekta ya mawasiliano wananchi wanatakiwa kuwa wabunifu wa kutumia mawasiliano kuhabarisha umma habari zitakazojenga maadili na kuwa na uzalendo ambao utajenga uchumi wa nchi.

Kauli hiyo, aliitoa jana jijini Arusha, wakati wa semina ya Kamati ya Amani ya mkoa huo, iliyoendeshwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

Lengo la semina hiyo, ni kukabiliana na uhalifu wa mawasiliano.

Gambo alisema TCRA kuwachagua viongozi wa dini kupata elimu ya mawasiliano ni kundi sahihi kwa kuwa wana nafasi kubwa ya kutoa elimu hiyo kwa waumini wao kuhusu kujikinga na uhalifu wa kimtandao na huduma za mawasiliano.

Alisema ana imani viongozi hao watawaelimisha waumini kutumia mawasiliano kwa maadili kujenga uchumi wa nchi.

"Watu watumie mawasiliano kwa kuzingatia uzalendo pamoja na kutumia mawasiliano katika kujenga uchumi wa nchi na si vinginevyo na kuwa wabunifu wa kutumia mawasiliano kwa kuhabarishana habari za kujenga maadili," alisema Gambo na kuongeza;

"Naamini viongozi wa dini mtafikisha elimu hii kwa ufasaha na kujenga taifa lenye maadili mema katika utumiaji wa mawasiliano," alisema.

Alisema kampeni hiyo iliyopewa jina la 'Sirubuniki Mjanja Haingizwi Chaka', imeanza kwa kundi la viongozi wa dini ikiwa ni kundi lenye watu wengi na ni rahisi kutoa elimu ya kujikinga na uhalifu unapotumia huduma za mawasiliano.

Mkuu wa Kanda ya Kaskazini TCRA, Mhandisi Emelda Salum, alisema wametoa elimu kwa viongozi wa dini, kwa kuwa wao ni ngazi katika kufikisha elimu kwa haraka kutokana na kuwa na kundi kubwa la waumini wa rika zote.

Alisema semina ya viongozi wa dini inatarajia italeta mafanikio kwa wananchi kuwa na uelewa namna ya kutumia mawasiliano na kwa Kanda ya Kaskazini wataendelea kutoa kwa ajili ya kujikinga na uhalifu wa huduma za mawasiliano. Ofisa Mawasiliano Mwandamizi wa TCRA, Mabel Masasi, alisema mikoa yote waliyozunguka kutoa elimu hiyo, wana imani elimu itawafikia wananchi wengi kwa kuwa wameyafikia makundi yote katika kampeni hiyo.

Alisema wakati umefika wananchi kutumia mawasiliano kwa kulinda usalama na amani ya nchi.

## Viongozi dini, mila wafundwa kupambana ukatili kijinsia

**Na Allan Isack,** ARUSHA

TATIZO la ukatili kwa wanawake na watoto katika jamii huenda likawa limepatiwa ufumbuzi wa kudumu baada ya Wizara ya Katiba na Sheria kuanza mchakato wa kutoa elimu kwa viongozi wa dini na kimila ili kuielimisha jamii kuhusu haki za wanamke na watoto.

Akizungumza jijini Arusha, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Amon Mpanju, alisema walitoa mafunzo ya siku mbili kwa viongozi hao.

Alisema lengo la kutoa mafunzo hayo ni kuielimisha jamii kutambua haki za wanamke, binadamu, watoto, wenye ulemavu na makundi yasiyojiweza kwenye jamii.

Alisema viongozi wa dini na wa kimila wanaushawishi mkubwa kwenye jamii na wanathaminiwa hivyo kutoa mafunzo hayo yatasaidia serikali katika harakati za kupambana na kutokomeza vitendo vya ukatili na unyanyasaji dhidi ya wanawake na watoto.

"Tumieni majukwaa yenu ya dini na ya kimila kuisaidia serikali kutokomeza vitendo vya ukatili na unyanyasaji dhidi ya wanawake, watoto na wenye ulemavu, tunatambua mna mchango mkubwa katika jamii, hivyo tumieni mafunzo haya kwenda kuielimisha jamii na kukemea vitendo vya ukatili hadharani," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya viongozi wa dini walioshiriki mafunzo hayo, Sheikh Hussein Junje, Mchungaji na Sadick Kinanga, walisema watayatumia mafunzo hayo, kutoa elimu kuhusu haki za sheria kwa wanawake na watoto na wanatarajia watapunguza matukio ya ukatili wa kijinsia.

Walisema, watatumia vizuri nafasi zao kuielimisha jamii kupiga vita matukio hayo ambayo yanaendelea kushamiri katika jamii inayotuzunguka.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Arusha, Blandina Nkini, alisema tatizo la unyanyasaji na ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto mkoani humo, bado linaendelea kushika kasi, kutolewa kwa mafunzo hayo kwa viongozi wa dini na wa kimila, itasaidia kuibadilisha jamii kutambua umuhimu wa kulinda na kuheshimu haki za wanawake, watoto na wenye ulemavu.

Mafunzo hayo ya siku mbili yametolewa na Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Mkoa wa Arusha, yaliwashirikisha viongozi wa dini na kimila kutoka mikoa ya Arusha na Manyara.



Mkazi wa Jiji la Arusha akichagua suruali za mtumba katika Barabara ya Idara ya Maji, jijini humo jana. Wananchi wengi wa kipato cha kati na chini hupendelea matumizi ya bidhaa za mitumba kutokana na unafuu wa bei. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

## Wadau wa kilimo watakiwa kubadilika

**Na Allan Isack,** KITETO

WADAU wa kilimo wilayani Kiteto mkoani Manyara, wametakiwa kubadilika na kuanza kutumia maofisa ugani ili kulima kilimo chenye tija ambacho kitawazalishia mavuno mengi.

Wadau hao walisema endapo wakulima watalima kilimo chenye tija kitawasaidia kuendesha maisha yao na kupata maendeleo ya kimaisha.

Mmoja kati ya wadau hao, Abasi Famau, alisema tatizo kubwa lililopo ni wakulima kuendelea kulima kilimo cha mazoea badala ya kubadilika kwa kulima kitaalamu.

Famau alisema wakulima wengi hawajabadili fikra ya kilimo cha kitaalamu na kutumia mbegu bora na zana za kisasa.

Alisema wakulima wa vijijini wanapaswa kubadilika kwa kutumia kilimo ambacho watawatumia maofisa ugani watakaowapa ushauri wa kitaalamu.

"Kuna wakulima bado hawajabadilika hata wakati wa palizi wa mazao shambani hawapalilii, ni vigumu kufikia malengo ya kilimo biashara endapo hatutabadilika," alisema Famau.

Alisema wanapaswa kubadilika kwa kujiunga na vyama vya msingi ambavyo vitawapatia elimu ya mauzo pamoja na kuwatafutia masoko ya uhakika.

"Pamoja na kuwa mazao machache, lakini tukijiunga na vyama vya msingi tutapiga hatua kwa namna moja au nyingine," aliongeza Famau.

Mkuu wa Wilaya ya Kiteto, Tumaini Magessa, aliwasisitiza wakulima wa eneo hilo, kuwatumia maofisa ugani ambao wapo kwenye kata zao.

Magessa alisema wakulima wanapaswa kuachana na kilimo cha mazoea na kufuata ushauri wa kitaalamu kutoka kwa maofisa ugani, ambao wanapatikana kwa urahisi.

Aliagiza madiwani na watumishi wa serikali wenye mashamba wilayani Kiteto, kumwonyesha mashamba yao ili aone kama elimu hiyo ya kitaalamu imewasaidia.

# Bonite Bottlers yakabidhi washindi zawadi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

HATIMAYE Kampuni ya Bonite Bottlers Limited (BBL), inayozalisha vinywaji baridi jamii ya Coca-Cola, imekabidhi zawadi ya pikipiki 25 na sanduku 1,350 kwa washindi wa Promosheni ya Shindano la V.I.P kwa wakazi wa mikoa ya Kanda ya Kaskazini.

Akizungumza jana mjini hapa kabla ya kukabidhi zawadi hizo, Meneja Mauzo na Masoko wa Bonite Bottlers Ltd, Christopher Loiruk, alisema zawadi hizo zinalenga kuimarisha biashara na kurejesha faida kwa wateja wake.

Alisema kuwa wateja hao ni wanaonunua bidhaa za soda jamii ya Coca-cola na kuuza bidhaa nyingi.

Alisema kiwanda hicho kimejipanga kuhakikisha kinawasaidia wateja wake kuboresha biashara zao.

Alisema washindi waliofanya vizuri zaidi watapewa zawadi za pikipiki kila mmoja, wengine watapewa sanduku 100 za soda kwa kila mmoja na wengine watapewa sanduku 50 kila mmoja.

"Washindi hao ni kutoka mikoa ya Kilimanjaro, Manyara, Arusha na Singinda. Washindi wanne kutoka Mkoa wa Manyara wamejishindia pikipiki kila mmoja, wawili kutoka Singida, 10 Mkoa wa Arusha wamejishindia pikipiki kila mmoja na Mkoa wa Kilimanjaro washindi tisa, hivyo mkoa uliongoza katika shindano letu ni Arusha na Kilimanjaro. Bado tunawatia moyo wateja wetu kuendelea kununua bidhaa zetu kwa wingi," alisema.

Washindi wengine 18 walijishindia zawadi za kreti za soda na washindi tisa walipata kreti 100 kila mmoja na wengine tisa kreti 50 kila mmoja.

Katika hatua nyingine alisema, kiwanda hicho kila mwaka kinashinda tuzo kwa kuzalisha bidhaa zenye ubora kimataifa.

Awali, Meneja wa Mauzo mkoa wa Arusha, Boniface Mwase, alisema kiwanda hicho kimeendelea kuchukua tahadhari ya maambukizi ya virusi vya corona kwa kuendelea kutoa elimu kwa wafanyakazi kazi ikiwa ni pamoja na kunawa mikono mara kwa mara waingiapo maeneo ya kazi na kutoka na kuepuka kushikana mikono.

# Ghasia asifu kukamilika maabara ya uchunguzi

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

WAZIRI wa zamani wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Hawa Ghasia, amesema kukamilika kwa maabara ya kisasa ya uchunguzi wa magonjwa ambukizi ya Hospitali ya Taifa ya Kibong'oto, kunaipa sifa Tanzania kimataifa kutokana na kukidhi vigezo vya Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO).

Alikuwa akizungumza jana wilayani hapa, baada ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, kutembelea na kukagua miradi mbalimbali inayoendelea kutekelezwa hospitalini hapo.

Ghasia ambaye ni Mbunge wa Mtwara Vijijini (CCM), alisema maabara hiyo itawezesha kutoa huduma bora zenye uhakika hususani kufanya uchunguzi wa kina wa magonjwa ambukizi na kutoa vipimo vinavyokubalika kimataifa. Alisema kamati hiyo imeridhishwa na kasi ya ujenzi wa maabara hiyo ambayo inajengwa kwa kufuata maelekezo ya Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) na kwamba hatua iliyofikiwa inaleta matumaini ya kukamilika kwa wakati. Akizungumza kabla ya kusoma taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya hospitali hiyo mbele ya Kamati ya Bunge, Mkurugenzi wa Hospitali hiyo, Dk. Riziki Kisonga, alisema hadi sasa maabara hiyo imemalizika awamu ya kwanza ya ujenzi ambao umegharimu Sh. bilioni 1.9.

"Awamu ya kwanza tayari na tumejenga kufuata viwango vya kimataifa na kuwa fedha zimetoka kwa wahisani na hivi sasa serikali ipo katika mazungumzo na wadau wengine ili kupata fedha za kuendelea na ujenzi," alisema. Dk. John Jingu ambaye ni Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Idara Kuu Maendeleo ya Jamii, alisema kukamilika kwa maabara kutaiwezesha hospitali hiyo kutoa huduma kwa wigo mpana zaidi tofauti na ilivyo sasa.

Alisema kukamilika kwa maabara hiyo kutaiwezesha hospitali hiyo kubadilika kimfumo na kuwa na vitengo badala ya idara, hali ambayo itaongeza idadi ya watumishi na ongezeko la huduma.

Naye Mwenyekiti wa Kamati hiyo ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Peter Serukamba, alisema serikali imewekeza katika hospitali hiyo na kuifanya ya taifa na kukamilika kwake kutatoa msaada na mataifa mengine.

"Maabara hii itakuwa na uwezo wa kufuatilia mwenendo wa vimelea vya ugonjwa wa kifua kikuu (TB) na vilevile itakuwa na itifaki ya kimataifa na hapa patakuwa kimbilio la wengi," alisema.



Mwanasheria wa Shirika lisilo la kiserikali la Haki Madini, Erick Luwongo, akizungumza na waandishi wa habari wa mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro kwenye mafunzo ya siku mbili ya kupambana na sheria kandamizi za habari yaliyohitimishwa juzi jijini Arusha. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mashindano ya insha shule 18 sekondari yasitishwa

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

UAMUZI mgumu wa serikali kuchukua hatua mbalimbali katika kukabiliana na ugonjwa wa corona ambao umetangazwa kuwa janga la dunia, umesitisha kwa muda usiojulikana mashindano ya insha kwa shule 18 za sekondari yaliyokuwa yaanze jana (Machi 18) Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro.

Taarifa iliyothibitishwa jana na Katibu wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), Bulugu Magege, inaeleza kuwa sasa mashindano hayo yatatangazwa baadaye.

"Kama ambavyo Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ametangaza kuzifunga shule zote nchini kwa siku 30, hatuna budi kusitisha shindano hilo ambalo lililenga kutafuta nguli wa insha inayoeleza maendeleo endelevu ya serikali ya Rais Dk. John Magufuli, kwenye sekta mbalimbali.

"Pamoja na mambo mengine, shindano hili lililenga pia kutoa elimu ya kujikinga na ugonjwa wa corona kwa kila shule. Sasa tutalitangaza baadaye."

Mchuano huo ulikuwa umepangwa kuanza Machi 18 na kufikia ukomo Machi 22, mwaka huu. Shule zilizokuwa zishiriki shindano hilo ni Suum Sekondari, Fuka, Oshara, Kishisha, Sanya Juu, Dahani, Kilingi, Kilasara na Karansi.

Nyingine ni Sekondari za Magnificant, Magadini, Namwai, Matadi, Visitation, Nuru, Orkolili, Sikirari na Faraja Siha Sekondari.

Mshindi wa kwanza katika shindano hilo angezawadiwa kompyuta mpakato, mshindi wa pili atapata kompyuta ndogo ya mkononi ya Ipad, mshindi wa tatu atapewa zawadi ya begi la kisasa la vifaa vya shule, wakati washindi 10 wa kwanza watapewa medali.

Uandishi wa insha, utawasaidia na kuwaongozea wanafunzi hao uwezo wao kukuza ujuzi wa lugha.

Ugonjwa huo unaosababishwa na kirusi jamii ya corona (Covid 19), ambacho ni tofauti na virusi vingine vya jamii hiyo ambavyo viliwahi kusababisha milipuko ya ugonjwa unaojulikana kama 'Sars-Cov' mwaka 2003 na Mers-Cov Corona Virus mwaka 2013.

Ugonjwa huo huambukizwa kwa njia ya hewa kwa kuingiwa na majimaji yenye virusi kutoka kwa mtu mmoja kwa njia ya kukohoa au kupiga chafya au kwa kugusa majimaji au makamasi kutoka kwa mgonjwa aliyethibitishwa kuwa na dalili za ugonjwa huo.

# ama

ALHAMISI MACHI 19, 2020

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 17

**Faida nane kunywa maji kabla ya chai**



Ukurasa 16

Janga la watoto wa Mkuranga wanatumbukia katika 'unga'



Ukurasa 14

**Wa vitambi hawapumui, wapoteza fahamu usingizini**



# FAHAMU KILA KINACHOHUSU MARADHI CORONA (COVID-19)

Ukurasa 18



Mgonjwa mwenye maradhi hayo, akitumia mashine ya kupumua. **PICHA: MTANDAO.**

## Wa vitambi hawapumui, wapoteza fahamu

**Na Mwandishi Wetu**

NI ugonjwa mpya aina yake sasa inawapa tabu Bara la Ulaya, kwa kuibuka maradhi ambayo mtu anapumua kwa tabu kwa shida usingizini, hali inayoweza kutokea mara nyingi, ikiendana na mgonjwa kupoteza kumbukumbu.

Wataalamu wanaitaja kwa jina la 'Obstructive Sleep Apnoea' (OSA), ambao ili mtu atibiwe kufika kiwango cha kupona ni mchakato unachukua wastani wa miaka miwili.

Utafiti wa awali unadokeza una uhusiano wa karibu kuwepo maradhi hayo na mgonjwa kuwa na kitambi, ingawaje haijawa bayana ni kwa namna gani.

Hadi sasa nchini Uingereza kunatajwa, kuna wastani wa wagonjwa milioni mbili wanaosumbuliwa na maradhi hayo.

Mtaalamu bingwa wa masuala ya kupumua, Dk. Annabel Nickol, katika Hospitali ya Oxford, anasema ni maradhi ya kipekee, pale inapotokea anahisi upumiaji usio wa kawaida, anapumua kwa kukoroma, kusinzia na kuwa na uchovu usioisha hata anapotoka kuamka.

Hiyo, inaendana na mgonjwa kuishi kwa masharti kama vile kutoendesha magari, hadi watapokuwa katika hali nzuri kiafya. **Kwa mujibu vyombo kimataifa.**

AFYA

# Mkemia Mkuu Kanda ya Ziwa majibu 'papo hapo' kama Dar

• Mitambo mipya yaja na mageuzi • Tegemeo la migodini na mahakamani • Yatoa ujuzi; madaktari, polisi, ustawi



Rais Dk. John Magufuli, alipotembelea na kukagua utendaji kazi wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), sasa inatanua wigo wa huduma zake kupitia kuongeza idadi ya mitambo walio nayo na hivi karibuni imenunua mitambo ya Sh. bilioni 6.5 kuhakikisha wanaboresha huduma nchini kote.

Mkemia Mkuu wa Serikali, Dk. Fidelice Mafumiko, anasema kuwapo mitambo hiyo ya kisasa, kutasaidia kupunguza siku za kupima vinasaba na kutoa majibu kutoka ndani ya siku 21 hadi siku moja

Ni ufafanuzi wa Dk. Mafumiko, katika kueleza mchango wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa lengo la kuangazia mafanikio, chini ya kivuli cha kampeni inayojulikana 'Tumeboresha sekta ya afya.'

> **Imetufanya tujisikie faraja zaidi kwa kuwa lengo letu ni kuhudumia wananchi kwa ukaribu zaidi.**

Mkemia Mkuu anafafanua: "Uwekezaji huu wa mitambo ya kisasa, umeongeza kasi na uwezo wa GCLA kufanya uchunguzi wa sampuli mbalimbali zikiwamo za dawa za kulevya, uchunguzi wa mazingira, vinasaba vya binadamu na wanyama na ubora wa chakula."

Anasema, kuwapo mitambo ya kisasa kumesaidia kutoa huduma kwa wingi na kasi kubwa, kulinganisha na miaka iliyopita.

Ni maboresho ya huduma, mbali na makao makao makuu jijini Dar es Salaam, pia katika Kanda za Ziwa, Kaskazini, Kusini na Nyanda za Juu Kusini.

Dk. Mafumiko anasema, mamlaka imefanikiwa kukarabati miundombinu ya ofisi za kanda zote nchini kwa gharama ya Sh. bilioni 1.3, uliosaidia kuboresha utendaji kazi.

Pia, katika kipindi hicho walifanikiwa kusajili wadau wa kemikali 2,426, kusajili vibali 21,336 na kutoa vibali 99,934 na kufanya kazi katika mipaka yote na katika bandari nchini kwa saa 24.

### KANDA ZIWA

Katika ziara hiyo pia, walifanikiwa kutembelea Kanda ya Ziwa inayojumuisha mikoa ya Mwanza, Mara, Shinyanga, Geita, Kagera na Kigoma, ambako Meneja wake, Bonaventure Masambu, anasema ilianzishwa ili kusogeza huduma karibu na wananchi.

Anasema, pia inaimarisha na kuongeza ufanisi katika utoaji huduma, kuongeza uhusiano na wadau wengine na kupunguza gharama kwa wananchi kufuata huduma jijini Dar es Salaam.

Masambu anasema tangu kuzinduliwa maabara hiyo, inafanya uchunguzi wa kimaabara, kusimamia na kudhibiti kemikali za viwandani na majumbani, ikitii masharti ya Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani ya Mwaka 2003.

Pia, anasema wana wajibu wa kuchunguza ubora wa bidhaa na kuchunguza uchafuzi wa mazingira, ili kulinda afya na mazingira na kutoa ushahidi wa kitaalamu mahakamani.

Masambu anasema, katika usimamizi wa kemikali, hivi sasa wanafanya ukaguzi wa maeneo yenye kemikali na kuyasajili na wadau wake.

Pia, lingine analotaja linaambatana na majukumu hayo ni kusimamia udhibiti wa kemikali katika mipaka iliyoko katika Kanda ya Ziwa na kutoa vibali vya usafirishaji na kuingiza na kuuza bidhaa nje ya nchi.

### MAFANIKIO YALIYOKO

Masambu anasema katika kipindi cha miaka minne iliyopita, mitambo yao mipya imewawezesha kufanya uchunguzi wa sampuli za uchafuzi wa mazingira.

Pia, mitambo mingine ya kisasa anayoiita GC ambayo inajukumu mahsusi ya kuchunguza sumu sumu mbalimbali kwenye sampuli zinazofikishwa katika maabara ya Kanda.

"Hii imesabisha kuboresha huduma zinazotolewa na mamlaka na hivyo kupunguza muda wa kuchunguza sampuli kwa kusaidia sampuli nyingi kufanyika katika maabara ya kanda, badala ya kupeleka makao makuu," anasema.

"Imetufanya tujisikie faraja zaidi kwa kuwa lengo letu ni kuhudumia wananchi kwa ukaribu zaidi," Masambu anaendelea.

Pia, anasema kuwapo kwa mitambo hiyo bora na ya kisasa , kumeongeza uchunguzi wa sampuli kutoka 1,085 kwa mwaka 2015 hadi sampuli 7,193 mwaka jana.

Anasema, ni hali inayoenda na kupungua muda wa kufanya uchunguzi kwa sampuli zinazoletwa maabara , kutoka siku 30 mwaka 2015 hadi siku 10 kwa kila sampuli, mwaka jana. Hizo ni sampuli zisizohitaji kupelekwa kuchunguzwa zaidi kwenye maabara nyingine.

Mkemia Masambu anafafanua

AFYA

# Mkemia Mkuu Kanda ya Ziwa majibu ‘papo hapo’ kama Dar

kuwa ni aina ya mafanikio yanayoendana na hali katika Kanda ya Ziwa kuwa na uwezo wa kutambua aina chache za sumu, huku zingine zilibidi wakati huo, zipelekwe makao makuu, jijini Dar es Salaam, kwa uchunguzi zaidi.

Anarejea kutoka kipindi cha mwaka 2017 hadi sasa, sampuli zote zilizohitaji uchunguzi, zimekuwa zikifanyiwa kazi katika maabara hiyo na inatokana na kuwepo vifaa vya kisasa, ikipunguza muda wa uchunguzi na majibu kutolewa kwa wakati.

**UWEZO ULIVYOTANUKA**

Mkemia Masambu, anasema hadi sasa maboresho yamewapa uwezo kufanya uchunguzi wa dawa za aina zote za kulevya katika kanda hiyo na kwamba, wameshafuta hitaji la kupelekwa Dar es Salaam.

“Hii imesaidia kuharakisha kesi za aina hii katika Mahakama zetu na mashauri mengi ya dawa za kulevya yanachukua muda mfupi kwa kuwa taarifa za uchunguzi hutolea baada ya muda mfupi,” anasema Masambu.

Masambu anasema, kupitia sampuli za mazingira zinafanyiwa uchunguzi katika kanda hiyo na kwamba jumla ya mitambo nane ya kusafisha na minne ya uchenjuaji wa dhahabu katika maeneo ya kilimo ya Serengeti, zilifanyiwa uchunguzi na maabara hiyo na serikali ilitumia matokeo kuchukua hatua za kisheria.

“Itakumbukwa kuwa katika kipindi hicho, kulikuwa na mgogoro mkubwa wa uchafuzi wa mazingira wa kampuni ya Accacia North Mara,” anadokeza na kuendelea:

“Ni maabara hii iliyohusika katika hatua za uchunguzi wa jumla ya sampuli 210 ambazo zilichukuliwa kwa vipindi tofauti na majibu yake ndiyo yaliyotumika katika maamuzi ya Serikali.”

Anasema kanda hiyo ni mdau mkubwa wa mashauri ya mahakama na kuanzia mwaka 2015, wamekuwa wakishiriki mashauri ya mahakamani, akitaja Mahakama Kuu Mkoa wa Mwanza na wilaya zake na vikao vya kuharakisha kesi 436 kwa ajili ya kutoa ushahidi.

Kwa mujibu wa Masambu, walitoa mafunzo ya namna ya kuchukuaji sampuli, utunzaji na usafirishaji wake, kabla ya kuvifikisha maabara, stadi ya ueledi uliowafikia wadau 184 katika mafunzo hayo.

Anaeleza kuwa, ni mafunzo yaliyolenga kuwapa ujuzi wadau, wakiwamo askari, madaktari na maofisa ustawi wa jamii, ili sampuli zinazopokewa ziwe katika ubora na kutoa matokeo yanayokidhi malengo tarajiwa.

Masambu anaenda mbali, akisema wanafanya ukaguzi wa maeneo yenye kemikali na yameongezeka kutoka maeneo 151 mwaka 2015 hadi 213 mwaka jana. Ni ongezeko la asilimia 70.



Rais Dk. John Magufuli akikagua maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali jijini Dar es Salaam. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

> **“ Ni maabara hii iliyohusika katika hatua za uchunguzi wa jumla ya sampuli 210 ambazo zilichukuliwa kwa vipindi tofauti na majibu yake ndiyo yaliyotumika katika maamuzi ya Serikali.**




Mkemia Mkuu wa Serikali, Dk. Fidelice Mafumiko

Ofisi ya Wakala wsa Mkemia Mkuu Mwanza, hasi sasa inaendelea kutoa vibali vya kuingiza na kutoa kemikali nchini, kupitia mipaka ya Kanda ya Ziwa na jumla ya vibali vyote vimeongezeka kutoka 1,350 hadi 2,246.

Masambu anasema kutokana na ongezeko hilo, wadau wengi walioptisha kemikali bila ya kuwa na vibali. Hivi sasa, wanafuata sheria kuzuia kemikali hatarishi zilizozuiliwa kuingia nchini.

“Hii inasaidia kuzuia matumizi yasiyofaa ya kemikali hasa ambayo yanaendana na uhalifu na maeneo yaliyosajiliwa yameongezeka kutoka 72 mwaka 2015 hadi maeneo 213 mwaka jana,” anasema Masambu.

**FAIDA KUU**

Anataja faida kuu wanayoachiwa ni kwamba, kutokana na elimu waliotoa, imewapa faida ya wa watumiaji wengi wa kemikali katika shughuli za uchenjuaji madini, wameongezeka maradufu akitoa mfano wa ongezeko kutoka 183 mwaka 2015 hadi 592 mwaka jana.

Masambu anasema, ni hatua ambayo imewavutia sana wauza madini, hata wakaongezeka katika kupidi cha miaka minne hadi kufikia mwaka jana na wamefikia wauzaji na wamefika 92 mwaka jana.

AFYA

JICHO KIMANZICHANA...

# Janga la watoto wa Mkuranga wanatumbukia katika 'unga'

**Na Elizabeth Zaya, aliyekuwa Kimanzichana**

***UKIWA ni mwendelezo wa makala kuhusu maisha ya vijana na watoto wa Kimanzichana, Mkuranga, ufuatao ni mwendelezo wa makala, safari hii ni namna walivyotumbukia katika matumizi ya dawa za kulevya.***

UNAPOFIKA eneo la Kimanzichana, Mkoa wa Pwani, katika barabara kuu kati ya Dar es Salaam na Lindi, linataka kuchukua sifa ya mji mdogo, japo yenyewe umaarufu unaishia barabarani.

Hata hivyo, kumeshamiri kwa mengi, mazuri kwa mabaya. Ni mahali kunakotawala ukanda wa viwanda wilayani Mkuranga, ambako sasa si haba, kwamba kasi ya uanzishaji inaendelea kila kukicha na kuna ugeni mkubwa.

Hapo watu ni wengi na hasa vijana, biashara ni nyingi, kuanzia lori zilizoegeshwa, mama lishe wasiohesabika na maduka lukuki.



Vijana wanaofanya biashara Kimanzichana. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

### DAWA KULEVYA

Vijana wengi kutoka vijiji jirani na jijini Dar es Salaam wanamiminika Mkuranga, baadhi wanafanya biashara zikiwamo nguo za mitumba, wengine wanasaka ajira na kuna sehemu kubwa ya waajiriwa, wanatoka Dar es Salaam. Moja ya vituo vyao vya usafiri ni Kimanzichana.

Umaarufu huo sasa una lake. Ni lipi hilo? Kuna kikundi cha watoto wanaokadiriwa kuwa na umri kati ya miaka 10 hadi 15, walioanzisha vijiwe vya matumizi ya dawa za kulevya, pia wanauza.

Uchunguzi wa Nipashe mahali hapo, ulibaini vilevi hivyo vinapatikana kutoka kwa wauzaji wa siri katika maduka mengi yaliyoko mahali hapo, wanaodaiwa kuanzisha vikudi vya utapeli, kupora na kutumia dawa za kulevya Kimanzichana, wilayani Mkuranga, mkoa Pwani.

Kikundi cha watoto hao kinadaiwa kushirikisha baadhi ya wanafunzi wa shule za msingi, sekondari na wengine wasiosoma kabisa.

Uchunguzi uliofanywa na Nipashe katika eneo hilo la Kimanzichana, ulibaini baadhi ya watoto wanaofanya hivyo, wamekuwa wakijikusanya katika maeneo maalum kwa ajili ya kuwategea wapita njia na kisha kuwapora vitu vyao.

Miongoni mwa vitu wanapora, ni pamoja na pesa, mikoba ya mikononi kwa kinamama, simu na vitu vingine vidogo.

Aidha, uchunguzi unabaini kwamba, kundi hilo la watoto linajikita kutumia dawa za kulevya, kama bangi na dawa ya usingizi aina ya 'volume' inayochanganywa na pombe inayoitwa 'kitoko' au konyagi.

Ni mambo yanayofanyika ili walewe na na kuopata ujasiri wa kutekeleza wanayonuia, hususani wanapokutana na wanaofahamiana nao.

> **Ukizoea kutumia dawa hiyo unaweza kuwa 'addicted' (kuathirika) au kuandaa mateja wa baadae ambao mwisho wa siku hatari yake ni kuangukia kwenye dawa za kulevya.**



Majengo, ambayo yamechorwa na vijana watumiaji wa dawa za kulevya.

### MADUKA NYEMELA

Nipashe ilielezwa na kuthibitisha namna vijana hao wamekuwa wakinunua dawa kwa bei Sh.50 kila kidonge katika maduka ya dawa ndani ya eneo hilo, bila ya kuwa na kibali kutoka mamlaka ya kitabibu, hali iliyothibitika mwandishi wa makala alipofanikisha kununua kwa ridhaa yake, pasipo baraka husika.

Katika maduka mengi ambayo gazeti hili lilifanya uchunguzi, ilibainika baadhi zilikuwa zinauza kwa kificho dawa hizo na zingine zinathubutu hadharani, kwa mtindo zinafichwa ndani na pindi mteja anapofika kuzihitaji ndio hutolewa.

### WENYEJI WAFUNGUKA

Mjumbe wa Serikali ya Mtaa wa Lisimalike katika Kata hiyo ya Kimanzichana, Sihota Mchonjo, anasema katika kundi la watoto hao, sasa wamekuwa tishio na kwamba mbali na kuiba vitu vidogo, pia wanachana madirishani na kuiba vitu.

"Wakichanganya hizo dawa na hivyo vidonge, wanakuwa kama 'mateja' kabisa. Unakuta vitoto vimelewa na vinaongea na kutukana maneno mazito, ambayo huwezi kutamani hata kuyasikia kama mzazi, inasikitisha sana!

"Kuna 'vijiwe' kama viwili ambavyo wanapenda kukaa. Mchana wanakuwa huku mtaani chini ya mti mmoja hivi mkubwa," anasema Machonjo na kuendelea:

"Jioni huwa wanahamia kwenye nyumba moja hivi ya kulala wageni, wanakaa kwa nje na wamechora huo ukuta mzima. Wakikaa hapo wanavuta bangi, na ndiyo wanakwenda kununua hivyo vidonge vya 'volume' wanachanganya kwenye pombe.

"Kwa hiyo, hapa mpaka tunaogopa watoto wetu kuharibikiwa, yaani hapa Kimanzichana ni vigumu sana kulea mtoto na akawa salama, tunaogopa. Hata sisi watu wazima huwa tunaogopa sana kukutana nao,"

Mjumbe huyo wa mtaa anasema, kundi hilo la watoto wamejipa jina linalofahamika kama 'Gank Star' na anasema tatizo kubwa linalochangia wengi kujiingiza katika makundi mabaya, ni wazazi kushindwa kuwajibika katika malezi bora.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Kimanzichana, Said Abdallah, baada ya kudadisiwa kuhusu mkasa huo, anasema alilazimika kutembelea eneo mojawapo linalotuhumiwa na akashuhudia kundi la vijana hao, akisema wengi wanakadiriwa umri kati ya miaka 13 hadi 15.

Anasema, vijana hao walikuwa zaidi ya 10 na wawili anawakadiria umri kati ya miaka 15 hadi 20 na alipowauliza sababu ya kuwapo mahali hapo kulikozungukwa na vichaka vikubwa, walimjibu "hakuna baya wanalofanya zaidi ya kukutana na kubadilishana mawazo."

Pale alipowadadisi kujua kama wanasoma shule, baadhi wasema tayari wameshamaliza masomo darasa la saba na hawakufanikiwa kuendelea na kidato cha kwanza.

Diwani wa Kata hiyo, Ally Kassim Ndipitipi, anasema alishapata taarifa za vijana hao na aliwashirikisha viongozi wenzake wa Kata kwa ajili ya kulifanyia kazi.

"Nilishapata hizo taarifa kuhusu hilo kundi la watoto, ni wadogo sana lakini ni tishio hadi sisi watu wazima tunawaogopa," anasema.

" Kwa kweli, kuna haja ya kulifanyia kazi haraka kwa maana bila hivyo hali itakuwa mbaya zaidi," anaendelea Diwani Ndipitipiti.

"Yapo mambo makubwa mabaya, ambayo watoto hawa wanafanya. Tukikuambia huwezi kuamini, ila itoshe tu kusema tupambane nao kabla mambo hayajaharibika zaidi na kuharibu kundi kubwa," anaeleza.

Diwani na mmiliki wa duka la dawa, Elizabeth Hokororo, anakana binafsi kuwa na taarifa za tabia hiyo na watoto hao kununua dawa za volume kwa ajili ya kuchanganya kwenye vilevi.

"Kwa kweli mimi bado sina taarifa hizo kwamba watoto wananunua dawa hizo katika maduka yetu ya dawa na kujiwekea kwenye vilevi, kwa lengo la kujilewesha, isipokuwa nitafuatilia," anasema Elizabeth, akiongeza:

"Mimi ni miongoni mwa wamiliki wa maduka ya dawa kwa muda mrefu ambao nachukizwa sana na watu wa namna hii wanaotuharibia sifa.

"Ninaomba tu wahusika wanaosajili hizi biashara waje wafanye msako maana katika eneo hili wengi sana wanafanya biashara bila kujisajili, watakuwa wametusaidia na sisi."

### USTAWI JAMII

Ofisa Ustawi wa ujamii katika Kata ya Kimanzichana, Neema Nyasulu, anasema tatizo kubwa linalochangia watoto wadogo kuingia katika uhalifu huo.

"Matokeo haya yote yanayoonekana kwa watoto hawa ni malezi mabovu kutoka kwa wazazi. Asilimia kubwa ya wazazi au walezi wa eneo hili, hawana mafunzo mazuri. Kwao, unakuta wanafanya mambo ambayo si ya kujenga kwa watoto.

"Tumekuwa tukizungumza nao mara kwa mara kwa ajili ya kuwapatia elimu, lakini hakuna kinachobadilika. Tunaomba hata hawa wanaowauzia dawa hizi waache, wazingatie masharti ya biashara zao," anasema Neema.

> **Tumekuwa tukizungumza nao mara kwa mara kwa ajili ya kuwapatia elimu, lakini hakuna kinachobadilika.**

Kamanda wa Polisi Wilaya ya Mkuranga (OCD), Andrew Ngassa, anakana kuwa na taarifa hizo na anaahidi kuifanyia kazi kiusalama.

Mfamasia Mkuu wa Serikali, Daudi Msasi, anaeleza matumizi ya dawa 'volume' kwamba ni kwa mgonjwa mwenye maumivu makali na inamsaidia kupata usingizi.

"Ukizoea kutumia dawa hiyo unaweza kuwa 'addicted' (kuathirika) au kuandaa mateja wa baadae ambao mwisho wa siku hatari yake ni kuangukia kwenye dawa za kulevya."

# Faida nane kunywa maji kabla ya chai



Mtu akinywa maji. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

MIILI ya binadamu inaundwa na asilimia 70 ya maji, hali inayowapa umuhimu wanadamu, katika suala la kunywa maji ya kutosha ili kuuwezesha mwili kufanya kazi vyema.

Iwapo mwili unakosa maji ya kutosha, unaangukia katika madhara mbalimbali ya muda mfupi na mrefu, kama vile magonjwa ya shinikizo la damu, saratani hata figo.

### KANUNI ZA AFYA

Mtu anaweza kutumia maji kama nyenzo ya kuboresha afya yake, kwa mfumo wa kuzingatia kanuni ifuatayo:

- Mtu anaweza kunywa maji takriban mililita 160 za maji, kabla ya kupiga mswaki au kula chochote mara tu unapoamka.
- Pia, unaweza kunywa maji angalau dakika 30 kabla ya kula, lakini si ndani ya dakika 45 baada ya kifungua kinywa, chakula cha mchana au jioni.
- Mtu anaelezwa kama hawezi kunywa angalau bilauri nne za maji, basi anaweza kuanza na moja kisha akaongeza kiwango taratibu, kadri mwili binafsi unavyomudu.

Orodha na faida kuu mtu kunywa maji kabla ya kula chochote pindi anapoamka asubuhi au muda wowote hajala chochote ni zifuatazo;

Mosi, inamuondolea sumu mwilini; unywaji wa maji mengi unasaidia kuwezesha viungo kama vile figo kufanya kazi yake vyema. Mtu anapokunywa maji kabla ya mlo asubuhi, utauwezesha mwili huo pia kujenga misuli na kuzalisha seli mpya za damu.

Pili, kunaboresha metaboli, ambao ni mchakato mwili unatumia vyakula (wanga, protini na mafuta) ili kupata nguvu na kujijenga. Hivyo, unywaji maji unawezesha mchakato huu kwenda vyema na kuufanya mwili kuwa na afya njema.

Kunywa maji kabla ya chochote, unaufanya utumbo kuwa tayari kufyonza virutubisho, ikizingatiwa maji ni muhimu kwa ajili ya watoto na watu wazima.

Tatu, inasaidia kupunguza uzito wa mwili, kwani uzito mkubwa si jambo zuri kiafya. Inapaswa kukumbukwa, mtu anapoamka na kuanza kutumia vinywaji kama vile soda na juisi vinachangia kuongeza uzito wa mwili.

Nne, maji yanaondoa kiungulia na matatizo ya umeng'enyaji chakula; inasaidia kuzimua krmikali tumboni inayochamngia kiungulia.

Sanjari na hayo, unywaji wa maji unarahisisha na kuhimiza mchakato mzima wa umeng'enywaji chakula tumboni.

Mtu anahimzwa anapopata shida ya namna hiyo, aanze kwa kuzingatia unywaji maji, kabla ya kutumia dawa mbalimbali zingine kwa mujibu wa mdaktari.

Tano, inaboresha na kuimarisha ngozi ya mwili; utafiti unadhihirisha unywaji maji takriban mililita 500 kwa siku unarahisisha mzunguko mzuri wa damu katika ngozi na kuchangia kuondoa sumu, ikiiacha ngozi katika hali nzuri zaidi.

Sita, upungufu wa maji mwilini una madhara makubwa kwa afya na kinyume ni sahihi. Utafiti unaonyesha robo ya uzito wa nywele ni maji. Hivyo, kutokunywa maji ya kutosha, kunaziweka nywele katika ukuaji duni na kuishia kuwa dhaifu.

Kwa kifupi, kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya ubora wa nywele, kuanzia mwonekano wake na unywaji maji ya kutosha mtu anapoamka asubuhi.

Nane, inazuia mawe kwenye figo; Unywaji maji unazimua tindikali inayosababisha mawe kwenye figo tumboni. Maji hayo yanaepusha kwa kiasi kikubwa matatizo ya figo. Utendaji wa figo unarahisishwa na maji, hasa uanayoywewa mapema baada ya kuamka.

Nane, kuongeza kinga mwilini; kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya mwili kuwa na kinga bora na unywa maji ya kutosha, hasa kabla ya kula kitu chochote.

Hapo ndipo, inamuacha mtu anayepigania kuwa na afya bora, ajiulize kila siku anakunywa maji kiasi gani na wakati gani?

- **Kwa mujibu wa taarifa za afya mtandaoni.**

AFYA

# Fahamu kila kinachohusu maradhi corona (covid-19)

• Maambukizi hadi dalili zake • Mzee hatarini, mtoto nafuu
• Siri ya chanjo, kinga, maski • Unavukaje vizuizi usijulikane?



Matibabu hospitali kwa wagonjwa wa corona.. **PICHA: MTANDAO**

**Na Jackson Paulo**

KUENEA kwa kasi kwa virusi vipya, kumesababisha mshituko mkubwa duniani. Shirika la Afya Duniani (WHO), limetangaza mlipuko wa virusi vya corona kuwa ni janga rasmi.

Tangu Jumatatu wiki hii, Tanzania imeingia katika orodha ya nchi zinazokabiliwa na kuongezeka mikasa ya ugonjwa huo.

Nchini Marekani, Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC), kinawashauri raia wake wajiandae kwa usumbufu wa maisha yao ya kila siku, ikiwa virusi vya corona vitaendelea kusambaa zaidi ndani ya jamii.

Fuatilia maswali yanayododosa undani wa maana ya maradhi corona:

**SWALI: Virusi vya corona ni nini?**

**JIBU:** Ni virusi vinavyosababisha mafua na matatizo mengine katika mfumo wa upumuaji wa binadamu.

**SWALI: Nini maana ya ugonjwa wa COVID-19, ambayo hutajwa sambamba na corona ?**

**JIBU:** COVID-19, ni kifupisho cha "Corona Virus Disease 2019" kwa kiswahili "Ugonjwa wa Virusi vya Corona 2019" na ndilo jina rasmi lililotolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO)kwa ugonjwa huu. Unaosababishwa na virusi vipya aina ya corona.

> **"Virusi vya Corona vinahisiwa kuenea hasa kutoka kwa mtu hadi mtu na hii inaweza kutokea, wakati watu wamekaribiana sana (ikiwa mmoja ana virusi).**

**SWALI: Watu wangapi wameathirika na ugonjwa wa COVID-19?**

**JIBU:** Idadi ya walioathirika inabadilika kwa haraka sana. Hata hivyo, kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Afya Duniani (WHO), mpaka kufikia tarehe 15 Machi 2020, idadi ya waliothibitika kuambukizwa virusi vya corona duniani kote ni watu 153,517 na vifo vilivyoripotiwa ni 5,735, kati ya mikasa yote. China pekee ina idadi ya mikasa 81,048 na vifo 3,204. Nje ya China, kumeripotiwa mikasa 72,469 na vifo 2,531.

Virusi vya corona vinaenea kwa kasi sana na katika nchi nyingi, hali iliyochangia kupelekea Shirika la Afya Duniani kuutangaza kuwa janga au 'pandemic' (neno linaloashiria kuwa ugonjwa umeathiri idadi kubwa ya watu, mikoa, nchi, au bara).

**SWALI: Dalili za COVID-19 ni zipi?**

**JIBU:** Baadhi ya walioambukizwa virusi vya corona, hawaonyeshi dalili. Hata hivyo, pale virusi vinaposababisha dalili za kawaida, huwa ni pamoja na homa ya kiwango cha chini, maumivu ya mwili, kukohoa, kupata makamasi puani pamoja na maumivu sehemu ya koo.

Hata hivyo, virusi vya corona vinaposababisha dalili kali zaidi, huwa ni pamoja na homa kali, kikohozi kikali na kubanwa pumzi, ambayo mara nyingi huashiria niumonia.

**SWALI: Ni muda gani hupita, kati ya mtu kuambukizwa virusi hadi kuanza kuonyesha dalili?**

**JIBU:** Kwakuwa virusi vya corona vimegundulika hivi karibuni tu, muda kati ya pale mtu anapoambukizwa virusi hadi anapoanza kuonyesha dalili (incubation period) bado haujabainika kwa uhakika kamili.

Kulingana na taarifa zilizopo, hadi sasa dalili zinaweza kuonekana haraka zaidi ndani ya siku tatu baada ya kuambukizwa virusi na wakati mwingine huweza kuchuka muda mrefu hadi siku 13.

Utafiti uliochapishwa hivi karibuni, uligundua kuwa kwa wastani, kipindi cha kupata ugonjwa hadi kuonyesha dalili ni kama siku tano.

**SWALI: Virusi vya Corona vinaenezwaje?**

**JIBU:** Virusi vya Corona vinahisiwa kuenea hasa kutoka kwa mtu hadi mtu na hii inaweza kutokea, wakati watu wamekaribiana sana (ikiwa mmoja ana virusi).

Hii inatokea pale matone madogo ambayo hutolewa wakati mtu aliyeambukizwa virusi hivi anapokohoa au anapopiga chafya, yanapoweza kuingia kwenye midomo au pua za mtu ambaye yupo karibu, au kuvutwa wakati wa kupumua na hivyo kuingia ndani ya mapafu.

Iwapo pia watu wamesalimiana kwa mikono na mmoja miongoni ni muathirika, virusi hivi huweza kuenea iwapo asiye na ugonjwa atajigusa sehemu za uso kwa mkono huohuo, kabla ya kunawa.

Virusi vya corona vinaweza pia kuenea kutoka kwenye sehemu au vitu vilivyoguswa na mtu mwenye virusi hivyo na kuacha vijidudu. Kwa mfano, anaweza kupata maambukizi ya virusi vya corona kwa kugusa sehemu au kitu ambacho kiliguswa na kuachiwa virusi, kisha akajigusa kinywa chake mwenyewe, pua, au pengine macho yake.

**SWALI: Ugonjwa wa COVID-19 una hatari kiasi gani?**

**JIBU:** Hapo inategemea iwapo mtu anaangalia kiwango cha vifo (hatari ya kifo kati ya walioambukizwa) au jumla ya idadi ya vifo.

Hadi sasa homa ya kawaida ya mafua imesababisha vifo vingi zaidi msimu uliopo sasa nchini Marekani na duniani kote, kuliko COVID-19. Hiyo ndio sababu unaweza kusikia ikisemwa kwamba mafua ni tishio kubwa zaidi.

Kuhusu kiwango cha vifo, imeonekana kwamba hatari ya kufa na maambukizi ya virusi vya corona (kawaida inakadiriwa kuwa asilimia tatu hadi nne) ni chini kuliko ilivyokuwa kwa Sars (takriban asilimia 11) na Mers (inakaribia asilimia 35), lakini inaweza kuwa juu kuliko hatari kutoka homa ya mafua, ambayo ina wastani wa asilimia 0.1.

Hata hivyo, takwimu zinazozunguka sasa kwa virusi vya corona zinaweza kubadilika kadri muda unavyokwenda, kwani watu zaidi wanapimwa na ripoti zinazidi kutolewa.

**SWALI: Nani yuko kwenye hatari kubwa zaidi ya kuathirika na ugonjwa wa COVID-19?**

**JIBU:** Watu wenye umri mkubwa - wazee na wale walio na shida za kimatibabu kama wenye magonjwa sugu ya mapafu, ugonjwa wa kubanwa pumzi, wenye matatizo ya moyo, ugonjwa wa kisukari, wote hao wana uwezekano mkubwa wa kuathirika zaidi iwapo wataambukizwa virusi vya corona.

**SWALI: Je, Watoto wana kinga dhidi ya virusi vinavyosababisha COVID-19?**

**JIBU:** Watoto wenye umri wa kati, pamoja na watoto wadogo sana, wanaweza kupata ugonjwa wa COVID-19 wanapokutana na mazingira ya maambukizi. Walakini, watoto huwa wanapata dalili za kiwango cha kawaida kama vile homa, kutokwa kamasi na kikohozi.

Hata hivyo, baadhi ya watoto walioambukizwa corona wamekuwa na dalili kali, lakini hii imetokea mara chache. Watoto walio na hali ya kiwango cha chini kiafya au we-

INAENDELEA UK.19

AFYA

# Fahamu kila kinachohusu maradhi corona (covid-19)

**INATOKA UK.18**



Hatua ya Hospitali ya Taifa Muhimbili, wageni wake wote wananawishwa mikono kila wanavyoingia. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

nye matatizo mengine ya afya, wanaweza kuwa katika hatari kubwa ya kuugua zaidi ugonjwa huu.

**SWALI: Je, hali ya hewa ya joto inaweza kuzuia ugonjwa wa COVID-19?**

**JIBU:** Virusi kadhaa kama vya mafua ya kawaida, huenea zaidi wakati kukiwa na hali ya hewa ya baridi japokuwa mtu huweza pia kupata ugonjwa wa mafua wakati wa majira ya joto. Hadi muda huo, bado haijajulikana ikiwa kuenea kwa ugonjwa wa COVID-19 kutapungua hali ya hewa itawakapokuwa ya joto.

**SWALI; Ni salama kupokea vifurushi kutoka China kwa sasa?**

**JIBU:** Hakuna sababu ya kuhisi kuwa vifurushi kutoka China vinaweza kuwa na virusi vya corona. Kumbuka, hivi ni virusi vya njia ya hewa kama ilivyo vya mafua. Kama ilivyo kawaida, huwa hakuna sababu ya kuacha kupokea vifurushi kutoka China wakati wa msimu wa mafua, vivyo hivyo tunapaswa kufuata mantiki hiyo hiyo kwa virusi ambayo husababisha COVID-19.

**SWALI: Ninaweza kupata virusi vya corona kwa kula chakula kinachoshikwa au kilichoandaliwa na wengine?**

**JIBU:** Kwa sasa bado dunia inajifunza kuhusu maambukizi ya virusi vya corona kwa kuwa ni vipya. Haijulikani wazi, ikiwa corona inaweza kusambazwa na mtu aliyeambukizwa kupitia chakula ambacho amebeba au amekiandaa.

Pamoja na kwamba virusi vya corona ni vya mfumo wa hewa ambavyo husambaa kwa njia ya kukohoa au kupiga chafya, virusi hivyo vimeonekana kwenye kinyesi cha baadhi ya watu.

Kwa hiyo, kwa sasa hatuwezi kusema kwa uhakika kuwa hakuna uwezekano wa maambukizi kupitia chakula kilichoshikwa au kutayarishwa na muathirika wa corona ambaye hajasafisha mikono yake.

**SWALI: Naweza kufanya nini kujikinga na wengine kutokana na Corona?**

**JIBU:** Vitendo vifuatavyo vinasaidia kuzuia kuenea kwa corona:

- Epuka kukaribiana sana na mtu ambaye ni mgonjwa.
- Epuka kugusa macho yako, pua au mdomo.
- Kaa nyumbani ikiwa unahisi wewe ni mgonjwa.
- Funika kinywa wakati wa kukohoa (kwa kutumia kiwiko)au piga chafya na tishu, kisha utupe tishu hizo kwenye chombo cha taka.
- Safisha na weka dawa ya kuua wadudu vitu vya kuguswa kila mara kwa kutumia dawa ya kawaida ya kusafisha.
- Osha mikono yako mara kwa mara kwa sabuni na maji.

**SWALI: Ninahitaji kujua nini kuhusu uoshaji mikono yangu vizuri?**

> **Katika hili, unapaswa kufuata mapendekezo ya afya ya umma yatolewayo mahali unapoishi. Hadi kufikia Februari 26 mwaka huu, vitambaa vya uso 'mask' havipendekezwi kwa umma kwa ujumla.**

**JIBU:** Osha mikono yako kila mara kwa sabuni na maji, angalau sekunde 20, mara baada ya kwenda bafuni, kabla ya kula na baada ya kupiga chafya, kutoa kamasi, kukohoa au kupiga chafya, kugusa sehemu zinazoguswa na watu wengi.

Ikiwa sabuni na maji hazipatikani kwa urahisi mahali ulipo, tumia dawa maalum 'sanitizer' iliyowekwa alcohol kwa kiwango cha angalau asilimia 60. Siku zote, osha mikono kwa sabuni na maji ikiwa inaonekana ni mchafu.

**SWALI: Je, napaswa kuvaa barakoa au 'mask' ya uso kujikinga na corona?**

**JIBU:** Katika hili, unapaswa kufuata mapendekezo ya afya ya umma yatolewayo mahali unapoishi. Hadi kufikia Februari 26 mwaka huu, vitambaa vya uso 'mask' havipendekezwi kwa umma kwa ujumla.

Ikiwa una dalili kama kukohoa au kupiga chafya, wataalamu wanapendekeza kuvaa mask ili kulinda wengine. Hii inaweza kusaidia kuzuia kusambaa kwa matone madogo ambayo yanaweza kuwa na virusi vya corona.

**SWALI: Je! Kuna chanjo ya corona iliyopatikana hadi sasa?**

**JIBU:** Hakuna chanjo inayopatikana mpaka sasa, ingawa wanasayansi watakuwa wanafanya uchunguzi. Hata hivyo, inaweza kuchukua muda wa mwaka au zaidi kabla hatujafahamu ikiwa tuna chanjo ambayo inafanya kazi.

**SWALI: Mtu ambaye amekwisha ugua ugonjwa wa corona akapona anaweza kuambukizwa tena?**

**JIBU:** Haijathibitika kinga ya mwili ya muda mfupi inaweza kujengeka kwa virusi vya aina fulani vinavyosababisha ugonjwa wa COVID-19. Hata hivyo, bado



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, akinena jambo kuhusu corona kutua nchini.

unaweza kuwa hatarini kushambuliwa na virusi vya aina tofauti vya corona.

Au, virusi hivi hivi vinaweza kubadilika, kama vile ambavyo virusi vya mafua hufanya kila mwaka. Mara nyingi mabadiliko haya hubadilisha virusi kwa kiwango cha kutosha kiasi cha kuufanya mfumo wako wa kinga ya mwili kufikiri ni maambukizi mapya kabisa.

**SWALI: Virusi vya corona vina uwezo wa kuishi sehemu ya nje au kwenye vitu kwa muda gani?**

**JIBU:** Bado haijajulikana ni kwa muda gani virusi vya corona vinaweza kuishi kwenye sehemu zilizoguswa na mgonjwa kama vile plastiki, mawe, mwamba, chuma, au shaba.

Kwa sasa, Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa CDC, kinapendekeza kusafisha kila mara sehemu au vitu vinavyoguswa kila mara na kila siku. Sehemu hizi ni pamoja na vibao, uso wa meza, vitasa vya milango, vifaa vya bafuni na chooni, simu, keyboard ya kompyuta, meza, pembeni na mwa kitanda.

**SWALI: Kwa nini ni vigumu kupata matibabu ya magonjwa ya virusi?**

**JIBU:** Dawa ya virusi ni lazima iweze kulenga sehemu maalum ya maisha ya virusi, ambayo ni muhimu kwake kuzaliana.

Dawa ya kuzuia virusi lazima iweze kuua virusi bila kuua seli ya mwanadamu ambayo ndiko virusi vinaishi. Pia, vina uwezo mkubwa wa kustahimili mazingira tofauti, kwa kuwa virusi huzaliana kwa kasi sana, vina nafasi kubwa ya kubadilika mara kwa mara kiasili (kubadilisha taarifa zao za maumbile kiasili 'genetic information') na kwa kila kizazi kipya wakizaliwa virusi wenye uwezo wa kuhimili dawa au chanjo.

***• Makala hii ni kwa mujibu wa taarifa rasmi za afya. Mwandishi anapatikana kwa baruapepe: jacpole@gmail.com***

MAZINGIRA

UKWEPAJI PETROLI...

# Mageuzi yanayotetea mazingira, jitihada kupata usafiri mbadala

•Magari ya nishati hewa, umeme




Gari inayotumia nguvu za nishati umeme, ikijaziwa nishati hiyo katika kituo maalum. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Nimi Mweta**

JITIHADA za kutafuta jawabu janga la mabadiliko ya tabianchi, zimepiga hatua katika nchi kadhaa duniani.

Kuna mfano, suala la kuondoa nishati ya mafuta na kutumia ambako hata utengenezaji magari binafsi unaanza kubadilika.

Miradi ya kutengeneza injini tofauti za ndege zinazotumia hewa ya haidrojeni, ambako wataalamu wanasema hewa hiyo inaweza kutumiwa moja kwa moja kwa kuchomwa katika injini ya ndege.


Inaweza pia kutumiwa kama chanzo cha umeme wa kuendesha betri nzito zinazowezesha mapanga au propela za ndege kuzunguka.

Ngazi hizo za kupambana na uzalishaji hewa chafu ya uchomaji mafuta ya taa au mafuta mazito yanayotokana na viumbe hai vya kale vilivyoyeyushwa na joto ardhini katika miamba, zinafikiriwa katika nchi zilizoendelea.

Kutokana na kuwepo utandawazi, wakishafikia viwango vinavyohitajiwa vya teknolojia ya kuanza kuzalisha vifaa husika, siyo lazima utengenezaji ubakie katika nchi tajiri, kwani nyingi zina matawi ya ushirikiano nchi za nje.

Licha ya ukinzani mkubwa kuhusu sera nzima ya uhamishaji viwanda, bado hali hiyo itaendelea kwa kiwango fulani kwa miaka mingi ijayo kutumia vyema zaidi rasilimali, nguvukazi na utaalamu bei poa.

> **Kuna wakati zilianza sera nchini Ufaransa, kutumia gari binafsi siku tatu kwa wiki na siku tatu na nyingine zilizobaki kwa wiki, inaachwa nyumbani.**




Gari inayotumia nishati ya mafuta.

Baadhi ya nchi tajiri zimeingia katika mikakati endelevu ya kubadili mfumo wa usafiri kwenda kazini kupunguza nguvu zote za matumizi ya magari binafsi.

Kuna wakati zilianza sera nchini Ufaransa, kutumia gari binafsi siku tatu kwa wiki na siku tatu na nyingine zilizobaki kwa wiki, inaachwa nyumbani.

Ni sehemu ya mapendekezo ya wasomi wa mazingira barani Ulaya, ambayo bado inaungwa mkono na sehemu ndogo ya jamii hizo.

Sera hiyo inaelekea kupata nafasi kubwa endelevu katika mkakati wa kupunguza magari binafsi barabarani na hata kuyaondoa kabisa, kwa ngazi ya safari za ndani ya mtaa au inayofanana nayo. Ni namna ya kubadili usafiri wa pamoja uwe huria.

Taarifa za nchi za Ulaya ambako mpango huo umeanza, zinaonyesha kuwa ni hali iliyowezesha idadi ya watu wanaosafiri kwa treni kuongezeka kwa kasi, tofauti na wachache katika zama zilizopita, katika safari ya kwenda kazini.

India, nchi inayoendelea kujitanua kuwa na idadi kubwa ya viwanda, kutaka kufikia zile ambazo zimeshasonga kikamilifu, nayo imeanza kutekeleza mkakati huo wa mfumo usafiri unaokabili athari ya kimazingira.

Kimsingi, maendeleo makubwa ya viwanda, yanaendana na kasi ya uchafuzi wa mazingira.

Ni mabadiliko yanayohitaji kukidhi matakwa ya mageuzi hayo ya kukabiliana na hali ya mazingira. Hapo kuna masuala kama kukidhi mageuzi na haja ya watu wapate viti kwa urahisi wanapoingia ndani ya basi.

Vinginevyo, inaelaezwa wale wanaojimudu hawataona ubora wa madhala wa kuacha magari mtu anapoangalia mikakati na mahali waliko, bado wako mbali na hatua ya kufikia vita vya kudhibiti matumizi ya mafuta ya taa, petroli, dizeli na mafuta mazito.

Kunahitajika mipango thabiti ya kushirikisha sekta binafsi kwa namna endelevu, huku hatua za kiserikali zinachukuliwa kama vile ujenzi wa reli katika njia zote kuu za miji, kuunganisha wilaya na mikoa kwa njia za reli

Hiyo, haina maana kuwapo reli kunaweza kuwatosheleza watu kuacha magari yao, au mabasi na kuhamia reli kwenye treni pekee. Kuna mazingira ya kutumia usafiri binafsi katika baadhi ya maeneo.

Licha ya kwamba, watu wamezoea kwenda katika kituo cha basi muda wowote na kupanda, treni zinapokuwa mbadala mkuu hata ikiwa mathalan kila baada ya saa moja, umma unapaswa kujipnga upya.

Tatizo ni pale panapokuwapo treni ambazo zinasafiri jijini kwa mara kadhaa tu, wakati abiria wa usafiri wa jumla katika umma, wanahitaji kuzungukia kila mara.

Mathalan, katika jijini la Dar es Salaam, kuna usafiri wa treni kuelekea nje ya jiji, Usafiri huo, uko wa eneo la makao makuu ya stesheni, jirani na Buguruni hadi Majohe, ambako ni stesheni ya kwanza kwa safari kuu ya treni.

Pia, kuna usafiri (kwa sasa) kati ya Kariakoo na Pugu, ambako nako ni safari kuu ya jiji na nyingine hadi Ubungo. Safari hizo huenda na eneo la Buguruni. Wakazi wa jiji, wameipa 'Treni ya Mwakyembe' kwa sababu Waziri Dk. Harrison Mwakyembe, ndiye aliisimamia, wakati huo akiwa na dhamana yake.

Kumekuwapo hisia tangu awali, nchi za dunia ya tatu, ikiwamo Afrika, ziletewe fedha kuziunga mkono, ili ziwekeze miundombinu ya reli, zifanane na kwingineko duniani, huku malengo ya mazingira yakiwa yanafikiwa.

Ina maana, miradi ya reli na treni inakuwa katika sura ya ruzuku, ingawaje haviwezi kutolewa katika sura ya zawadi, bali uwekezaji endelevu.

Hiyo inakuwa faida kwa taifa hata pale uendeshajii unapokuwa ni wa binafsi.






Wanafunzi wa shule mbalimbali za sekondari katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wakihangaikia usafiri wa kurejea majumbani kwao kwenye kituo cha daladala katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, jana asubuhi, baada ya shule zote nchini kufungwa na Serikali kufuatia tishio la corona. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# DC aiagiza Polisi katazo la mikutano

**Na Grace Mwakalinga,**
MBARALI

MKUU wa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, Reuben Mfune, amemwagiza Mkuu wa Polisi wilayani humo, kutotoa vibali vya kuruhusu mikutano ya aina yoyote ili kujiepusha na maambukizi ya virusi vya corona. Mfune alitoa agizo hilo jana, alipokuwa akizungumza na watumishi na viongozi wa dini wilayani humo, kwa lengo la kutoa tahadhari juu ya maambukizi ya ugonjwa huo ambao tayari umeripotiwa nchini.

Alisema kuanzia sasa mikutano ya aina yoyote hairuhusiwi na upande wa makanisa na misikiti wataandaa utaratibu ili kuepukana na hatari ya ugonjwa huo. "Kutokana na hali hiyo namwagiza mkurugenzi wa fedha zote ambazo zilitengwa kwa ajili ya shughuli za Mwenge sasa zielekezwe kununulia vifaa mbalimbali vya kujikinga na maambukizi ya corona," alisema Mfune. Alisema vifaa vitakavyonunuliwa vielekezwe kwenye maeneo mbalimbali zikiwamo ofisi za vijiji na kata huku akisisitiza kuwa dawa zote na vifaa lazima vipatikane kwenye duka la serikali lililopo hospitali ya wilaya na kwa bei nafuu.

Aliwaomba viongozi wa dini kuendelea kuomba kwa Mungu na kutoa elimu juu ya kujikinga katika kila ibada watakayokuwa wakiifanya.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Dk. Godfrey Mwakalila, alisema tayari maeneo yametengwa kwa ajili ya watu kuwaweka kwenye uangalizi washukiwa wa maambukizi ya corona wakati taratibu za kusafirisha sampuli kwa ajili ya vipimo zikiendelea. Aidha, Dk. Mwakalila alisisitiza umuhimu wa kuchukua tahadhari ya maambukizi kwa kuhakikisha wanawatenga walioambukizwa hata kama ni ndugu zao wanaowapenda.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi wilayani humo, Hashim Mwalihawa, alisema kuwa elimu ya kujikinga na maambukizi inapaswa kufika maeneo yote hususani ya starehe kwani wengi wao baada ya kutumia pombe hujisahau na kudharau maelekezo wanayopewa ya kujikinga na maradhi.

# Mashauri 1,564 ya ardhi, ndoa yapatiwa ufumbuzi

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

JUMLA ya mashauri 1,564 ambayo yanahusisha masuala ya ardhi na ndoa yameripotiwa na kutatuliwa katika kipindi cha mwaka 2019, huku mashauri mengine 514 yakikatiwa rufani kwenda Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS). Hayo yalisemwa juzi na Mratibu wa Shirika lisilokuwa la kiserikali linalotoa huduma ya msaada wa kisheria mkoani Mbeya (Mbepace), Laiki Ndagile, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake. Alisema kuripotiwa kwa mashauri hayo imesaidia wananchi kupata huduma za kisheria kwa urahisi kupitia kwa wasaidizi wa kisheria ukilinganisha na miaka ya nyuma, ambapo ni wanasheria pekee ndio walikuwa watoa huduma za msaada wa kisheria.

Ndagile alisema shirika hilo ambalo lengo lake ni kutoa huduma ya kisheria pamoja na mafunzo kwa wananchi, limekuwa chachu ya kuleta mabadiliko kupitia elimu wanayoitoa kwenye jamii kuhusiana na masuala mbalimbali ikiwamo, ndoa, ardhi na unyanyasaji wa kijinsia.

"Tumeweka utaratibu wa kuwafundisha wananchi masuala ya kisheria kutoka kila kata na wakihitimu siku 15 wanakuwa na sifa ya kutoa huduma ya msaada wa kisheria, lengo likiwa ni kupunguza gharama na usumbufu kwa wananchi wasio na uwezo kuwafikia mawakili wa kijitegemea," alisema Ndagile.

Alisema idadi ya mashauri 1,564 ambayo yalitatuliwa kabla ya kufika ngazi za juu za mahakama inatoa picha kuwa wasaidizi wa kisheria wamekuwa na mchango mkubwa kwenye utoaji wa huduma ya kisheria licha ya kuwa bado zipo changamoto zinazowakabili katika kutekeleza majukumu yao. Alisema hadi sasa Mkoa wa Mbeya una jumla ya wasaidizi wa kisheria 81 hitaji likiwa ni zaidia ya 150 ili kutoa huduma bora kwenye kila kata, na kwamba wananchi 21 waliohitimu wataenda kupunguza changamoto ya uhaba huo. Mmoja wa wanafaika wa elimu ya msaada wa kisheria kutoka Kata ya Kongoro Mswisi iliyopo wilayani Mbarali, Rehema Mwapasi, alisema elimu hiyo amemsaidia kuwahudumia vizuri wananchi huku akisimamia haki.

Alisema elimu hiyo imetoa dira kwake namna ya kuwahudumia wananchi kuwapatia msaada wa kisheria ukilinganisha na ilivyokuwa awali ambapo alitamani lakini hakuwa na elimu hiyo. Isabela Kapufi kutoka Kata ya Igawilo jijini Mbeya, alisema elimu hiyo imemsaidia kushughulikia migogoro mingi kwenye mabaraza ya ardhi ya kata ambako wanawake wengi hunyimwa haki zao.

# Waomba wataalamu udhibiti wa mchwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAKAZI wa Kijiji cha Chang'ombe, Kata ya Mjele, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameomba wataalamu kudhibiti utitiri wa wadudu aina ya mchwa, ambao wanatafuna nguzo za umeme na kuanguka, hali inayohatarisha usalama wao.

Wakizungumza na Nipashe jana kijijini hapo, wananchi walisema kutokana na wadudu hao kuongezeka na kuharibu nguzo za umeme, waliamua kuwaua kwa kutumia mafuta ya taa, lakini hawajafanikiwa kuwadhibiti.

Kutokana na kushindwa kuwaua mchwa hao, wananchi wamewaomba wataalamu kuwasaidia kuwadhibiti ili wasiendelea kuharibu nguzo za umeme.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Chang'ombe, Masaka Sukula, alilishauri Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco), mkoani Mbeya kusimika nguzo ambazo haziwezi kushambuliwa na wadudu hao.

Aliongeza kuwa wananchi wanaendelea na zoezi la kufukia mashimo yaliyochimbwa na mchwa hao kwenye nguzo ili kuzua athari zaidi ikiwamo kukatika kwa umeme.

"Wananchi wangu wanalazimika kufanya kazi ambayo ilitakiwa kufanywa na Tanesco na wakati huo huo wanafanya hivyo bila kuchukua tahadhari yoyote," alisema Sukula.

Kwa upande wake, Ofisa Uhusiano Msaidizi wa Tanesco, Shami Lameck, alisema baada ya kupata taarifa ya mchwa kushambulia nguzo za umeme na kuzua taharuki kwa wakazi wa Chang'ombe, walifanya mkutano kutoa elimu ya tahadhari dhidi ya umeme.





# Serikali yawamwagia pikipiki 448 maofisa tarafa nchini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imegawa pikipiki 448 kwa ajili ya kurahisisha utendaji kazi kwa maofisa tarafa nchini, huku ikipiga marufuku kutotumika kama kitega uchumi kwa kubeba abiria.

Uamuzi huo ulitangazwa jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaab (Tamisemi), Selemani Jafo, alipokuwa akikabidhi pikipiki hizo kwa baadhi ya wakuu wa mikoa.

Alisema pikipiki hizo zina thamani ya Sh. bilioni moja na zimetolewa kwa maofisa hao kwenye mikoa 24 nchini.

"Pikipiki hizi zimenunuliwa na serikali ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya Rais John Magufuli, aliyoitoa katika kikao chake na maofisa hao Juni 4, mwaka huu jijini Dar es Salaam," alisema.

Alieleza hatua hiyo itaondoa kero ya vitendea kazi na serikali imeendelea kuzipatia ufumbuzi kero zingine kadri mapato ya serikali yanavyoimarika.

Aliagiza wakuu wa mikoa kuhakikisha pikipiki hizo pamoja na magari ya viongozi wa Mikoa, Wilaya na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutumika kwa shughuli za serikali na si vinginevyo.

"Hapa tuelewane, pikipiki hizi zina namba za serikali ni marufuku kugeuza pikipiki hizi kuwa kitega uchumi na kuanza kusafirisha abiria, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na dhamira ya Mheshimiwa Rais kutoa pikipiki hizi," alisema.

Alitaka zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa na kutunzwa kwa kufanya matengenezo kwa wakati.

"Wakuu wa mikoa hakikisheni pikipiki hizi zinawafikia walengwa ambao ni maofisa tarafa kwa kuzingatia mgawanyo wa tarafa mlioziwasilisha, kwa mikoa ya Songwe na Pwani wao hawapo kwenye mgao huu kwa kuwa tulitangulia kuwapatia," alisema.

Jafo aliwahimiza kuhakikisha vyombo hivyo vinadumu kwa muda mrefu na kutoa huduma kwa wananchi kwa urahisi.

"Ifahamike kuwa serikali imetumia fedha nyingi kwa ajili ya kununua vyombo vya usafiri hivyo ni lazima vitunzwe vizuri ili vitumike kwa muda mrefu na kurahisisha utendaji kazi, sitarajii kusikia kuwa kuna changamoto ya ukosefu wa vyombo vya usafiri," alisema.

Alisisitiza vipaumbele vya serikali ni vingi na kuwataka kuyatunza magari mapya waliyopata viongozi kutokana na baadhi yao kuwa na utunzaji mbaya unaosababisha kuharibika kwa muda mfupi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Mkuchika, alisema pikipiki hizo zitarahisisha utendaji kazi kwa maofisa hao hususan kipindi cha uchaguzi mkuu.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Uhuru, jijini Dodoma, wakimsikiliza Mwalimu Hadija Salumu kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania kuhusu vifaa vya ufundishaji vinavyotumika na wanafunzi wenye ulemavu wa macho kwenye maonyesho ya mashindano ya kitaifa yaliyofanyika jijini Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# TAEC yabuni teknolojia ya mazao

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TUME ya Nguvu ya Atomiki Tanzania (TAEC), imebuni teknolojia ya kuhifadhi chakula kwa njia ya nyuklia ambayo inasaidia mazao kutoharibika haraka.

Akizungumza katika maonesho ya mashindano ya kitaifa ya Sayansi Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU), Mtafiti Mwandamizi wa TAEC, Simon Mdoe, alisema teknolojia hiyo itazuia uharibifu wa mazao pindi yanaposubiri kupelekwa sokoni.

"Teknolojia hii imebuniwa na watafiti wazalendo ambao wametengeneza mashine hiyo yenye uwezo wa kuhifadhi mazao, vyakula, matunda visiharibike hata baada ya miezi sita," alisema Mdoe.

Aidha, Mdoe alisema teknolojia hiyo pia inatumika kuboresha bidhaa za viwandani na vya matibabu ili kuviweka katika hali ya ubora na usafi.

Kadhalika, Mdoe alisema tume hiyo imeandika andiko kwa ajili ya kupata wahisani wa kujenga kiwanda hapa nchini ambacho kitasaidia kuendesha shughuli za kupiga mionzi mazao hayo.

"Endapo kiwanda hicho kitajengwa hapa nchini, kitasaidia kuzuia upotevu wa mazao, kwani wafanyabiashara wataweza kukaa na bidhaa zao kwa muda mrefu bila kuharibika," alisema mtafiti huyo.

Mdoe alisema hivi sasa wafanyabiashara wa matunda, mboga wanakabiliwa na upotevu wa bidhaa zao, pindi wanaposubiria kupata soko na hivyo kuharibika.

Aidha, mtafiti huyo alisema, uanzishwaji wa matumizi ya teknolojia ya mionzi katika uhifadhi inatarajia kuongeza mbinu za uhifadhi wa mazao na kuongeza mnyororo wa thamani kwa masoko ya nje.

## Vifurushi maalum vya simu vyanukia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Atashasta Nditiye, amesema serikali ipo kwenye mchakato wa kutengeneza vifurushi maalum ambavyo watu waliopo nchini watawasiliana na waliopo nje ya nchi kawaida bila kutumia mtandao wa 'Whatsapp'.

Nditiye alitoa kauli hiyo jana wakati akifunga mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Sekta ya Mawasiliano.

Alisema kifurushi hicho maalum kitasaidia watu kuwasiliana kawaida na kumudu gharama za mawasiliano.

"Tupo kwenye mchakato wa kutengeneza mtandao maalum wa kupiga simu nje ya nchi na tutatafuta utaratibu ili watu watumie bando/vifurushi kupiga simu nje na si kutumia mtandao, tutazifanyia kazi changamoto bila kumuumiza mtu yeyote maana kazi yetu ni kuhakikisha sekta inaendelea na watu wanufaika nayo," alisema.

Aidha, alivitaka vitengo na idara katika sekta ya mawasiliano kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa kuzingatia mikataba ya kazi na ufanisi ili ishike nafasi ya kwanza kwenye uchangiaji pato la taifa.

"Nchi inajua umuhimu wa sekta hii hata kwenye pato la taifa hatujazidi nafasi ya tano mwaka 2017/18 tulichangia asilimia 13.4 baada ya Wizara ya Maliasili na Utalii tukazidi uchukuzi na Madini, lakini tumeshika nafasi nzuri na tukifanya kazi kwa bidii zaidi tutachukua nafasi ya kwanza hivyo kuwakuwa hakuna mtanzania asiyependa mawasiliano tumewekaza fedha na tutawafikia waliobaki," alisema.

Alisema serikali kupitia wizara, inapimwa kutokana na namna inavyotekeza majukumu yake kwa wananchi kwa ufanisi, ni vyema wafanyakazi wakaonesha mfano katika kazi ili kuhamasisha wengine kufanya kazi kwa bidii. Akizungumzia mafanikio yaliyopatikana kwenye sekta hiyo katika kipindi cha mwaka 2019/20, alisema kuwa ujenzi wa vituo vipya 10 vya kutolea huduma za Mkongo wa Taifa kwenye ofisi za serikali katika halmashauri mbalimbali nchini umekamilika.

Alizitaja halmashauri zilizojengwa vituo hivyo kuwa ni pamoja na Siha, Nyang'wale, Bukombe, Ngorongoro, Nsimbo, Kalambo, Buhigwe, Busekelo, Buchosa na Mbogwe.

Aidha, alisema kazi za uboreshaji vituo 72 vya kutolea huduma za mkongo nchini ipo kwenye hatua za mwisho kukamilika ambapo takribani Sh.bilioni 1.6 zimetumika kwa kazi hiyo.

Akizungumzia matumizi ya Tehama, Nditiye alisema kuwa taasisi 87 zimefanyiwa maunganisho kwenye mikoa 16 nchini na kazi hiyo inatarajiwa kukamilika ifikapo Juni mwaka huu.



**HABARI ZANZIBAR**

# Tamwa yataka jamii kulinda watoto dhidi udhalilishaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Chama cha Wanahabari Wanawake (Tamwa) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, ameitaka jamii kuwa na umoja wa kumlinda mtoto wa kike ili aweze kuepukana na udhalilishaji wa kijinsia.

Aliyasema hayo katika ofisi za chama hicho zilizopo Tunguu, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja, wakati alipokuwa akizungumza na wanamtandao wa kupinga vitendo vya udhalilishaji kutoka wilaya tatu za Unguja.

Alisema kwa kiasi kikubwa wanamtandao hao wanaendelea kutoa mchango wao kupunguza vitendo vya udhalilishaji kwa wanawake na watoto na kwamba ipo haja jamii ikawaunga mkono.

Aliwakata wanamtandao hao kushirikiana kikamilifu kufichua matendo yote wakiamini kuwa wana wajibu wa kufanya hivyo kwa lengo la kujenga jamii bora.

"Matendo haya ya udhalilishaji kwa wanawake na watoto hayana mmoja kila mtu aguswe na kero hii na awe tayari kuwafichua wote wenye kufanya mambo haya," alisema.

Aliwataka wanamtandao hao kufanya kazi kwa ushirikiano wakiamini kuwa umoja wao ndio chachu ya kuleta mabadiliko katika jamii.

Mkufunzi katika mafunzo hayo, Hawra Shamte, kutoka Tamwa, akiwasilisha mada alisema kila mtu anapaswa kutunzwa na kuenziwa kwa mujibu wa haki ya kikatiba.

Alisema anapotokea mtu ama kikundi cha watu kumfanyia udhalilishaji mtoto wa kike au kiume anakwenda kinyume kwa mujibu wa Katiba, hivyo anapaswa kuchukuliwa hatua kali.

Washiriki wa mafunzo hayo walisema, wamekua wakipambana na matendo hayo ya udhalilishaji, lakini changamoto ni kitendo cha kutolewa dhamana kwa watuhumiwa wa kesi hizo jambo linalowavunja moyo kuendeleza harakati hizo.

# Serikali yaombwa kufunga shule, hoteli za kitalii

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANANCHI wameiomba Serikali ya Zanzibar kufunga shule na hoteli za kitalii katika kipindi hiki cha hofu ya mlipuko wa virusi vya corona, ili kukiweka kisiwa hicho katika hali salama. Walisema kisiwa hicho kimebahatika kuwa na vivutio na hoteli nyingi za kitalii hali inayowafanya watoto wao kukimbilia wageni ambao huwapa zawadi ndogo ndogo kitendo kinachoweza kuwafanya wapate maambukizi.

Pia kutokana na tahadhari ya ugonjwa huo, baadhi ya wafanyabiashara wamechukua fursa hiyo kujinufaisha kwa kuwaibia wananchi wanaofika kununua maski na maji tiba (sanitizer) katika maduka ya dawa mjini hapa.

Akizungumza na Nipashe mmoja ya watoa huduma kwenye duka la dawa lililopo Darajani Mjini Zanzibar alisema, juzi watu wengi walifurika dukani hapo kwa ajili ya kununua visaidizi hivyo na mmoja kati ya wateja wake aliibiwa simu akiwa dukani hapo.

"Majira ya mchana Jumatatu kulikuwa na kundi kubwa la watu dukani hapa na hafla ikazuka tafrani baada ya mteja wetu mmoja kuibiwa simu akiwa dukani hapa," alisema.

Mtoa huduma huyo ambaye hakutaka kutajwa jina lake aliwataka wananchi kuwa waangalifu na mali zao hasa katika mwingiliano wa watu kwa sababu baadhi yao huwa sio waminifu. Alisema vifaa hivyo visaidizi vimemalizika dukani hapo hivyo wanatarajia kuagiza kutoka Tanzania Bara.

Naye Ofisa Afya Kitengo cha Elimu ya Afya kutoka Wizara ya Afya Zanzibar, Mwanaisha Abdulrahman, aliwataka wananchi kuchukua tahadhari katika matumizi ya maski ambazo hivi sasa zimekua zikitumika kwa ajili ya kujikinga na maradhi ya corona.

Alisema matumizi sahihi ya maski ni muda wa saa sita endapo mtumiaji atakuwa yupo katika sehemu salama. Aliwataka wananchi kuhakikisha kuwa wanazitumia vizuri maski ili zisiweze kuwaletea madhara na kuwa makini katika suala la usafi. Katika hatua nyingine baadhi ya wananchi waliozungumza na Nipashe wameiomba Serikali ya Zanzibar kuzifunga shule zote na madrasa kama ilivyoamua Tanzania Bara kutokana kuwa na hofu ya ugonjwa huo.

"Mimi mwanangu leo nimemzua asiende shule maana wazazi tumeshakuwa na hofu kubwa kuhusu janga hili hivyo tunaiomba Serikali ya Zanzibar kuzifungia shule," alisema Mwaka Kassim Khatib, mkazi wa Marumbi, Mkoa wa Kusini Unguja.

Pia, aliomba serikali kuzifungia hoteli zote za kitalii ili wageni wasiweze kuingia nchini.

Alisema Kijiji cha Marumbi kimebahatika kuwa na hoteli nyingi za kitalii na watoto wao wanapowaona watalii huwafuata na hupewa vitu mbalimbali ikiwamo peremende kama zawadi.



Ofisa Afya Dhamana wa Bandari ya Zanzibar, Ali Ahmada Ali (wa pili kulia), akielezea kuhusu utoaji wa huduma kwa wasafiri wanaoingia na kutoka bandarini kwa Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi, jana. Kulia kwake ni Waziri wa Afya wa Zanzibar, Hamad Rashid. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wananchi waondolewa hofu ugonjwa corona

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya Zanzibar, Hamad Rashid, amesema wizara yake haitaficha taarifa yoyote ya mtu atakayebainika na virusi vya corona visiwani humo na kuwataka wananchi kutulia na kutoingia hofu.

Alisema, serikali iko makini na tayari imeshaweka maandalizi ya kutosha ili kudhibiti ugonjwa huo.

Alisema hayo wakati wa ziara ya kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kuangalia maeneo maalumu ya yaliyotengwa kwa ajili watu watakaobainika kuwa na dalili za virusi vya corona.

"Serikali iko makini na tayari imeweka maandalizi ya kutosha ili kudhibiti ugonjwa huo, lolote litakalotea serikali itatoa tamko," alisema Waziri Hamad.

Kamati hiyo ilifanya ziara ya kutembelea Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, Bandarini na kituo cha dharura cha matibabu ya ugonjwa wa corona, kilichopo Kidimni, kuona jinsi vituo hivyo vilivyojipanga kudhibiti virusi vya ugonjwa huo.

Naye Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mwanaasha Khamis Haji, amesema kamati imeridhishwa na maandilizi yaliyofanywa na serikali kutokana na kuwapo kwa vifaa vinatakavvohitajika kutoa huduma katika vituo hivyo.

Aliutaka uongozi wa Bandari na Mamalaka ya Viwanja vya Ndege kutoa ushirikiano na Wizara ya Afya ili kuzuia na kudhiditi ugonjwa huo nchini.

Kwa upande wake Msaidizi Mkuu wa Kituo cha Afya Uwanja wa Ndege, Mohamed Khamis Ali, alisema Mamlaka imeweka utaratibu maalumu kwa wageni wanaoingia nchini, kuwapima kwa kutumia vifaa maalum ili kutambua afya zao.

"Tumeweka utaratibu maalumu kwa wageni wanaoingia nchini ikiwa ni pamoja na kuhakikisha anavua vidhibiti vya ugonjwa huo alivyotumia safarini ikiwamo 'gloves' na maski, kunawa mikono kwa dawa maalumu na kupimwa kwa kutumia mashine malumu ya kutambua ugonjwa huo," alisema.

Katika hatua nyingine Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, kimewataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari ya kujikinga na ugonjwa huo.

Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar Dk. Abdulla Juma Saadalla, alisema ugonjwa huo ni janga la kiafya dunia nzima hivyo ni vyema kuwa na tahadhari.

Alisema Zanzibar ni miongoni mwa nchi zinazopokea raia wengi wa kigeni kupitia sekta ya utalii, hivyo ni lazima mamlaka husika kufanya kazi ya ziada ya kuhakikisha maeneo yote yanayotumika kama njia za kuingia visiwani humo wanakuwapo wataalamu wa afya kwa ajili ya kufanya vipimo vya ugonjwa huo.

Alisema ni wajibu wa kila mwananchi bila kujali tofauti za kisiasa, kidini, kikabila na rangi kuanza kuchukua hatua stahiki za kujikinga.

Alivitaka vyombo vya ulinzi na usalama kudhibiti bandari bubu na njia mbalimbali zisizo rasmi za kuingia katika visiwa vya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla ili kuzuia baadhi wa watu wanaotumia njia hizo kuingia nchini wasilete ugonjwa huo.

Alitoa wito kwa waumini wa dini mbalimbali nchini, kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya wanapokusanyika kwa ajili ya ibada ikiwamo makanisani na misikitini.

# Corona yasitisha ziara wafanyabiashara DRC

**Na Mwandishi Wetu**

ZIARA ya wafanyabiashara kwenda Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kati ya Aprili 6 na 9 kwa ajili ya kutafuta soko la uhakika la bidhaa zinazozalishwa na viwanda Tanzania imeahirishwa kutokana na corona.

Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Angelina Ngalula, amesema ziara hiyo imesitishwa kufuatia kuripotiwa kuwapo wagonjwa wa corona katika nchi hizo mbili.

"Ziara yetu itafanyika baada ya mamlaka husika kutangaza hali ya usalama juu ya ugonjwa wa corona katika nchi zetu," alisema.

Ngalula na kuongezea kuwa hali hiyo imetoa nafasi pia ya kujipanga zaidi katika kufanikisha lengo la ziara. Alisema lengo la ziara hiyo ni kuhamasisha na kutafuta masoko ya bidhaa zinazozalishwa nchini hivyo kuahirishwa kwake kunatoa nafasi kwa wafanyabiashara na wajasiriamali wengine kujiandisha ili waende kujionea fursa na kuunganishwa na masoko.

"TPSF ndiyo kiungo wa wafanyabiashara nchini hivyo ziara hii imelenga kutengeneza soko la uhakika la bidhaa zinazozalishwa wajasiriamali wadogo na wafanyabiashara ili kukuza biashara zao na kufikia maendeleo yaliyokusudiwa," alisema Ngalula. Alisema Tanzania ndiyo lango kuu la biashara kwa DRC, hivyo ni lazima kuchangamkia fursa hiyo na kuongeza masoko ya bidhaa zinazozalishwa Tanzania ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za serikali katika kutekeleza azma ya ujenzi wa uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025.

Mwakilishi wa Balozi wa DRC nchini, Moma Kampinga, alisema ziara ya wafanyabiashara wa Tanzania kwenda nchini kwake ilikuwa na maana kubwa sana katika ushirikiano na kuongezea kuwa wataendelea kushirikiana na Tanzania katika sekta ya biashara ili kukuza uchumi wa nchi zote mbili.




Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Benki ya CRDB, Tully Esther Mwambapa (kushoto), akionyesha namna ya kutumia mpango maalumu wa kuwasilisha maoni ya mteja kwa njia ya QR Code, wakati wa uzinduzi wa mpango huo, uliofanyika kwenye Tawi la benki hiyo, Mlimani City jijini Dar es Salaam, juzi. Katikati ni Mkuu wa Kitengo cha Huduma kwa Wateja, Yolanda Urio na wafanyakazi wengine. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Aonya uchochezi taharuki corona

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KAIMU Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Nuru Mpuya, amewataka waandishi wa habari kujiepusha na habari zenye kuleta taharuki kwa wananchi juu ya mlipuko na maambukizo ya virusi vya corona.

Alitoa rai hiyo jana alipozungumza na waandishi wa habari mjini Shinyanga, akisema vyombo vya habari vinapaswa kutoa elimu kwa wananchi juu ya kujikinga na maambukizo ya virusi hivyo na siyo kuandika habari zenye kuleta taharuki.

Alisema waandishi wa habari wana fursa kubwa ya kuelimisha jamii juu ya kujikinga na maambukizo ya ugonjwa huo kupitia kalamu zao, hivyo ni vyema wakajikita zaidi kuandika habari chanya na siyo zenye kuleta taharuki kwa wananchi.

"Nawaombeni sana waandishi wa habari mkoani Shinyanga, msiandike habari zenye kuleta taharuki kwa wananchi juu ya virusi hivi vya corona, bali mjikite zaidi kuandika habari zenye kuelimisha wananchi kujikinga na virusi hivyo, ili jamii ibaki kuwa salama.

"Natoa wito pia kwa wananchi wa Mkoa wa Shinyanga, wafuate maelekezo ambayo yametolewa na serikali juu ya kujikinga na virusi vya corona, kwa kutoshikana mikono, kunawa mara kwa mara mikono, kupiga chafya kwa kufunika pua na kitambaa pamoja na kuepuka mikusanyiko," alishauri.

Alisema wameshatenga maeneo kwa ajili ya kukabiliana na wagonjwa wa virusi vya corona katika halmashauri zote za mkoa huo.

Ofisa Afya wa Mkoa wa Shinyanga, Neema Simba, alisema wameshajipanga vyema kukabiliana kuzuia maambukizo ya virusi hivyo kwa kufanya ukaguzi kwenye nyumba za kufikia wageni kutokana na mkoa huo kuwa na mwingiliano mkubwa wa wageni unaochagizwa na viwanda na migodi ya madini.

# Gereza lapigwa jeki ujenzi wa zahanati

**Na Mwandishi Wetu**

GEREZA la Tukuyu lililopo Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya lililojengwa miaka1957, limepewa msaada wa bati 100 kujengea jengo jipya la zahanati kwa ajili ya askari na wananchi walio jirani na gereza hilo.

Akizungumza baada ya kuupokea msaada huo uliotolewa na Benki ya NMB, Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Chalya Julius ambaye alikuwa mgeni rasmi, alisema kuwa msaada huo ni zawadi kubwa ndani ya gereza na wananchi ambao wengi hupata huduma za afya ndani ya eneo hilo ambalo kituo cha kwanza cha zahanati kitapata uwezo wakuhudumiwa watu wengi zaidi.

Msaada huo uliotolewa wa mabati yenye thamani ya shilingi milioni tano ambazo zitakwenda kwenye ujenzi wa jengo jipya pembeni ya zahanati hiyo.

Mkuu wa Gereza la Tukuyu, Anganile Mwakalobo, alisema kuwa msaada huo uliotolewa na bati 100 kutolewa na benki hiyo ya NMB ndio nguvu iliyoweza kujenga juu ya jengo na kudai kuwa kiasi cha Sh. milioni 15 ni kiasi kilichobaki kumalizia jengo zima la zahanati hiyo.

Diwani Emmy Masseta, Mwenyekiti wa Huduma za Jamii kwa niaba ya Mwenyekiti wa Halmashauri ya Rungwe, alisema kuwa kazi kubwa imefanyika kuwezesha ujenzi wa kituo kikubwa kipya cha zahanati tofauti na eneo dogo lililopo kwa muda wa miaka 25.

Meneja wa Kanda ya Nyanda za Juu ya NMB, Straton Chilongola, alisema kuwa msaada huo umeweza kufika kwenye gereza hilo ili kufikisha faida njema inayotolewa na benki hiyo ili kuzisaidia jamii na kwamba huduma za afya ndio uhai wa watu na afya njema ndani ya gereza hilo lenye watumishi wa umma na wananchi wengi ambao ni jirani.

## HABARI KIMATAIFA

# Joe Biden ashinda dhidi ya Bernie Sanders

**WASHINGTON,** Marekani

MAKAMU wa zamani wa Rais wa Marekani, Joe Biden (pichani chini), ameimarisha nafasi yake ya uongozi katika kinyanganyiro cha uteuzi wa mgombea wa Chama cha Democratic baada ya kushinda kura za mchujo katika majimbo ya Florida na Illinois jana.

Majimbo hayo mawili pamoja na Arizona yaliendelea na mchakato wa uchaguzi wa mchujo licha ya wasiwasi kuhusu afya ya umma kuhusiana na kitisho cha virusi vya corona, ambacho kimeyalazimu majimbo mengine kadhaa kuahirisha kura hiyo.

Kwa mujibu wa matokeo ya awali, Biden anatarajiwa pia kushinda jimbo la Arizona.

Katika majimbo ya Florida na Illinois, Biden alishinda kwa asilimia 61.9 dhidi ya 22.8 na asilimia 59.4 dhidi ya 35.8 mtawalia dhidi ya Bernie Sanders.

Likiwa na wajumbe 219 jimbo la Florida ndiyo lilikuwa ushindi mkubwa usiku wa kuamkia jana huku Illinois na Arizona zikiwa na wajumbe 155 na 67 mtawalia. **DW**



# Iraq yateua Waziri Mkuu licha mkwamo wa kisiasa

**TEHRAN,** Iraq

BAADA ya mkwamo wa kisiasa uliodumu kwa wiki kadhaa, Rais wa Iraq, Barham Saleh, jana amemteua Adnan al-Zurfi kuwa Waziri Mkuu mpya wa taifa hilo.

Gavana huyo wa zamani wa mkoa wa Najaf sasa ana siku 30 za kuunda baraza ambalo hatimaye litapigiwa kura ya imani bungeni.

Kufuatia uteuzi wake, Al-Zurfi alisema ataandaa uchaguzi wa mapema na wa haki katika kipindi cha mwaka mmoja iwapo serikali yake itaridhiwa na Bunge.

Aidha, ameahidi kuyashughulikia madai ya waandamanaji walioandamana kwa miezi kadhaa kupinga ufisadi na kushindwa kwa serikali.

Uteuzi wake umekuja wakati maroketi kadhaa yakishambulia eneo lenye ulinzi mkali, karibu na ubalozi wa Marekani jana jioni.

Shambulizi hilo lilikuwa la nne la roketi katika kipindi cha wiki moja baada ya maroketi kadhaa kupiga vituo vya kijeshi vinavyowahifadhi wanajeshi wa kigeni. **DW**

# Majimbo 50 ya Marekani yakumbwa na corona

**WASHINGTON,** Marekani

VIRUSI vya corona sasa vimeyakumba majimbo yote 50 nchini Marekani huku jimbo la West Virginia likiripoti kisa cha kwanza cha maambukizi Jumanne.

Akitangaza kisa cha kwanza cha Covid-19 katika jimbo la West Virginia, Governor Jim alisema kuwa: "Tulifahamu kuwa hii inakuja."

Jiji la New York City limesema linaangalia uwezekano wa kufunga shughuli zote za umma sawa na ile iliyowekwa katika eneo la San Francisco Bay.

Kumekuwa na vifo 108 nchini Marekani vilivyotokana na corona na zaidi ya visa 6,300 vimethibitishwa kote nchini humo.

**Hatujawahi kuwa katika hali hii kabla. Sijawahi kusikia kitu kama hiki katika historia ya jiji la New York.**

Takriban visa 200,000 kote duniani na karibu watu 8,000 wamekufa kutokana na virusi vya corona.

Huku utawala wa Rais Donald Trump ukiangalia jinsi ya kutoa fedha za kuchochea ukuaji wa uchumi zilizoripotiwa kuwa sawa na Dola za Marekani bilioni 850, Waziri wa Fedha, Steve Mnuchin alisema kuwa utawala, "Unaangalia jinsi ya kuwatumia hundi wamarekani mara moja".

Kiwango cha ukosefu wa ajira kimefikia hadi asilimia 20 kikiwa kimeongezeka mara dufu ikilinganishwa na wakati wa msukosuko mkubwa wa kiuchumi wa mwaka 2008.

Meya Bill de Blasio alisema ataamua katika kipindi cha siku mbili ikiwa atawaagiza wakazi wa jiji hilo wapatao milioni 8.5 "kupata makazi".

Hatua hiyo inaweza kuwafanya watu walie nyumbani kwao tu, huku wakiruhusiwa kufanya matembezi ya lazima kununua bidhaa za nyumbani au dawa, kutembeza mbwa au kufanya mazoezi ili mradi waepuke mikusanyiko ya umma.

"Ni uamuzi mgumu, mgumu sana vigumu,"Bwana de Blasio alisema.

"Hatujawahi kuwa katika hali hii kabla. Sijawahi kusikia kitu kama hiki katika historia ya jiji la New York."

Maofisa katika eneo la San Francisco Bay wamekwishatoa amri kwa wakazi milioni 6.7 kubakia nyumbani isipokuwa inapokuwa lazima hadi Aprili saba. **BBC**



Shughuli zimeanza kurudi kama kawaida nchini China ikiwa ni ishara kuwa, imefanikiwa kwa kiwango kikubwa kudhibiti kuenea kwa Corona licha ya kuwa kiini cha mlipuko vya virusi hivyo. **PICHA: NA MTANDAO**

# China kuwafukuza waandishi wa habari wa Marekani

**BEIJING,** China

NCHI ya China imetangaza jana kuwa itawafukuza waandishi wa habari wa Kimarekani kutoka magazeti matatu makubwa ya Marekani.

Hiyo ni moja ya hatua za ukandamizaji wa taifa hilo la kikomunisti dhidi ya vyombo vya habari vya kigeni na kuchochea mzozo mkali kuhusu uhuru wa vyombo vya habari.

Hatua hiyo dhidi ya waandishi wa magazeti ya New York Times, The Washington Post na Wall Street Journal inakuja katika wakati ambapo mataifa hayo mawili yenye nguvu kiuchumi yakivutana kuhusu janga la virusi vya corona.

Mvutano huo umekuja baada ya Rais Donald Trump wa Marekani kuviita kichokozi virusi vya corona kuwa "virusi vya China".

Beijing ilisema hatua yake ya kuwafukuza waandishi hao wa habari ni ya kisasi dhidi ya uamuzi wa Washington kupunguza idadi ya raia wa China wanaoruhusiwa kufanya kazi kwenye vyombo vya habari ya serikali yake vilivyoko nchini Marekani.

Beijing imewataka waandishi hao kurudisha hati za utambulisho wao katika kipindi cha siku 10 na kusema hawataruhusiwa pia kufanya kazi kwenye maeneo yenye utawala wake wa ndani ya Hong Kong na Macau. **DW**

# Raia wake waliokwama kuwarejesha

**BERLIN,** Ujerumani

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Ujerumani, Heiko Maas, amesema nchi hiyo imeanza mchakato wa kuwarejesha nyumbani maelfu ya raia wake waliokwama nje kutokana na janga la virusi vya corona.

Maas alisema katika mahojiano maalumu na DW hapo juzi, kuwa ndege kati ya 30 na 40 ziliondoka na kwenda maeneo mbalimbali duniani kuwarejesha watalii katika operesheni itakayochukua siku chache. **DW**

# Waziri aahidi kuingilia kati wawekezaji kunyimwa vibali

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, ameahidi kushughulikia tatizo la vibali kwa wawekezaji wa Kampuni ya Mountain Birds and Trophies, inayojihusisha na ufugaji wa wanyamapori hai watambao.

Pia Kanyasu ameahidi kushughulikia suala la kampuni hiyo kuruhusiwa kuanzisha bustani ya wanyamapori hai inayotembea (mobile zoo) baada ya kushindwa kujibiwa barua ya maombi yao kwa takribani miaka miwili sasa.

Wawekezaji hao walinyimwa vibali kwa ajili ya kusafirisha sampuli ya sumu za nyoka kwenda nje ya nchi kwa ajili ya utafiti. Pia waliiandikia Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (Tawa) kwa ajili ya kuanzisha bustani ya wanyama hai.

Akizungumza jana jijini hapa baada ya kutembelea bustani hiyo inayofuga nyoka, vyura, ng'e na vinyonga, Kanyasu aliwaahidi wawekezaji kuzifanyia kazi changamoto hizo haraka, hivyo wasikate tamaa ya kuwekeza zaidi nchini.

Kanyasu alisema wizara itaangalia uwezekano wa kushusha bei ya nyoka kutokana na malalamiko ya wawekezaji hao kuwa bei zimekuwa kubwa hali inayowafanya kushindwa kuendelea na mradi wa kukamua sumu za nyoka.

Alisema zilizokuwa zilizoandaliwa na wizara kuhusiana na bei ya wanyamapori hai hasa nyoka, zililenga watu walioanzisha bustani za wanyamapori hai na si wanaohitaji nyoka kwa ajili ya kuwakamua sumu.

Kwa mujibu wa kanuni za bei ya nyoka kwa sasa, nyoka mmoja anauzwa Sh. 800 ilhali hampuni hiyo inahitaji nyoka 3,600 kwa ajili ya kutafiti sumu halisi inayohitajika nchi za nje, hivyo kuwafanya washindwe kumudu gharama hiyo.

"Nataka nitakaporudi kesho (leo) Dodoma, Mkurugenzi wa Idara Wanyamapori, anieleze kitu gani kinachofanya wawekezaji hawa waliobadilika baada ya katazo la serikali la kusafirisha wanyamapori hai nje ya nchi na kuamua kusafirisha sampuli ya sumu ya nyoka kuzuiwa kupata vibali vyao," alisema.

Kanyasu amesema tangu katazo la serikali la mwaka 2016 la kusafirishwa wanyamapori hai, Wizara imekuwa ikiwataka wadau wa uhifadhi nchini kuja na mbinu mbadala ili kuendana nalo, kuanzisha bustani ya wanyamapori hai kwa ajili ya kuhamasisha utalii wa ndani.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni hiyo, Paul Madinda, amesema tangu serikali ilipositisha kusafirisha wanyamapori hai licha ya kuyumba kiuchumi, waliamua kubadilisha biashara kwa kuanza kuuza sumu ya nyoka na wadudu wengine lakini wanakosa ushirikiano kutoka mamlaka husika.

Amesema licha ya kupewa kibali na Tawa cha kukamua sumu za nyoka, wamenyimwa vibali vya kusafirisha sampuli ya sumu hizo kwenda nje ya nchi kwa ajili ya kufanyiwa utafiti ili kujua sumu za nyoka zipi ndizo zinahitajika katika soko la dunia.




Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Selemani Mzee (wa nne kushoto), akipiga makofi, wakati wa uzinduzi wa Klabu ya Biashara ya NBC, kwa wilaya hiyo, mkoani Mtwara juzi. Wengine ni Meneja wa tawi la NBC Masasi, Erick Mbeyale (kulia) na Meneja wa Bidhaa na Huduma za Kifedha, Jonathan Wilson (wa pili kulia) pamoja na baadhi ya wafanyakazi wa benki hiyo. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Dar yakusanya 95% mauzo ya madini

**Na Elizabeth Zaya**

SOKO la Madini la Mkoa wa Dar es Salaam limekusanya Sh. bilioni 7.616 sawa na asilimia 95.2 ya makadirio ya makusanyo ya Sh. bilioni nane kwa mwaka wa fedha 2019/2020 unaoishia Juni 30.

Akizungumza mbele ya Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, Ofisa Madini wa Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani, Ally Maganga, alisema makusanyo hayo ni ada ya ukaguzi wa madini, mrabaha, ada ya pango ya leseni na faini.

Maganga alisema Tume ya Madini iliyataka masoko ya madini kwa mikoa hiyo miwili kukusanya Sh. bilioni 13.157 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na kwamba hadi Februari 2020 masoko hayo yalikuwa yamekusanya Sh. 7,883,886,475.28.

Alisema katika kipindi hicho wamepima madini ya vito yenye uzito wa karati 4,887.44 yenye thamani ya Sh. 1,853,514,789.05 na dhahabu kilogramu 46.7 ya thamani ya Sh. 5,064,825,539.54 huku Tume ya Madini ikikusanya Sh. 382,620,947.38 ambazo ni mrabaha, tozo za madini na ada ya ukaguzi.

Naibu Waziri wa Madini, Stanslaus Nyongo alisema Serikali ipo kwenye mchakato wa kutengeneza sera na sheria kwa ajili ya kusimamia shughuli za kisonara.

Alisema lengo ni kuweka mazingira bora kwa wote wanaojihusisha na shughuli hizo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, Dastan Kitandula, aliipongeza Serikali kwa kuboresha sheria ya madini na kuanzisha masoko hayo ambayo alisema yamekuwa mkombozi kwa wachimbaji wadodgo na wakati ambao awali walikuwa wanafanya biashara zao katika mazingira magumu.

# 'Andikeni habari za Mahakama kama zilivyo'

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WAANDISHI wa habari nchini wametakiwa kuandika habari za mahakama kama zinavyotolewa ili kuepuka upotoshaji.

Rais iliyotolewa jana na Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Dk. Paul Kihwelo, wakati akifungua mafunzo ya waandishi wa habari kuhusu uandishi wa habari za mahakama, yaliyoandaliwa na Mahakama ya Tanzania kupitia mpango mkakati wa miaka mitano unaotekelezwa na mradi wa maboresho wa Benki ya Dunia kwa kutoa mafunzo hayo miaka miwili mfululizo.

Jaji Kihwelo ambaye pia ni Mkuu wa Chuo cha Uongozi wa mahakama Lushoto, alisema kumekuwa na utaratibu wa kihabari wa kuandika kichwa cha habari tofauti na inavyozungumzwa hali inayoleta maana tofauti.

"Sisi huwa tunakwazika sana, lakini tunaamini ni taaluma yenu, pale inapoandikwa na kuleta sintofahamu na inawakwaza watu, lakini tunapenda sana mahakama iandikwe kwa namna ambavyo hata kama unakosoa basi kuna namna ya ukosoaji," alisema Jaji Dk. Kihwelo.

Alisema watu wengi huwa hawaelewi kesi zao, mahakama gani zilipo, shauri linakwenda mahakama gani, na kesi ikiisha mtu akishindwa, haki yake ni kukata rufani, mambo ambayo yanapaswa kuandikwa vizuri ili mtu asipate tabu.

Jaji Dk. Kihwelo alisema, katika mafunzo hayo watawapitisha kuifahamu mahakama, taratibu za mahakama muundo wa mahakama pamoja na nafasi na jukumu la watendaji wa mahakama.

Alisema mafunzo hayo yamendaliwa na mahakama kwa sababu inatambua umuhimu wa habari na wanahabari na kuwa na maofisa habari wa mahakama kuwa na fursa kubwa katika jamii kuielezea mahakama kwa usahihi.

Alifafanua nguzo ya tatu ya mpango mkakati, inasisitiza ushirikishaji wa wadau na kama inavyoeleweka wanahabari na vyombo vya habari ni nguzo muhimu na kuiita dola ya nne katika nchi.

Alisema Mahakama inazungumza kwa kupitia kalamu na mtu hawezi kutoka mbele tena kuzungumzia uamuzi ulioutoa na wakati mwingine mahakama hupitia lawama si Tanzania tu bali hata dunia nzima.

Alisema Mahakama nyingi duniani zimekwepa hazipendi kuingia kwenye mijadala na ingekuwa wanakwenda wanasema tena baada ya kuandika hukumu wangetoa stori nyingine.

Jaji Dk. Kihwelo alisema Mahakama imebadilika sana na inaendelea kubadilika siku hadi siku ikiwamo kufungua milango wazi kwa wanahabari na ndio maana kuna maofisa habari wa mahakama wanaojaribu kutoa ufafanuzi wa kutoa taarifa.

Naye Ofisa Habari Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Lydia Churi, alisema mafunzo hayo yameandaliwa na Mahakama ya Tanzania kwa kushirikiana na Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto yakihusisha makundi mawili tofauti wakiwamo wahariri wa habari kutoka vyombo mbalimbali nchini na maofisa wa mahakama ambao ni wawakilishi wa maofisa habari wa mahakama kutoka mikoa mbalimbali nchini.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kufanya utekelezaji wa nguzo ya tatu ya mpango mkakati wa miaka mitano kwa kujenga taswira chanya ya mahakama kwa wananchi na kushirikiana na wadau wa mahakama kwenye shughuli za mahakama kutoka na wanahabari kuwa ni wadau muhimu wa mahakama katika kuhakikisha wananchi wanafahamu shughuli na huduma zinazotolewa.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**VIWANJA VINAUZWA,** Headline block ya viwanja vine inauzwa, Viko mbweni mpiji karibu na Shule ya Sekondari Mpiji . Eneo zaidi ya heka moja ) 4220 Sq mt . Viwanja Surveyed. Simu: 0711 506758 0787 445506, 0679 041220


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**


### KUPOTEA KWA HATI

**SAIDA SAID RUBANZA** anatangaza kupotea kwa hati ya nyumba namba **65332** Plot No. **137 Block 4 Bunju B** Kinondoni yenye jina la **Yunus Ismail Rubanza na Saida Saida Rubanza** . Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **KW/RB/1483/2020**

115672302

### NAFASI YA KAZI

Anahitajika **Secretary/Accountant..**

**Qualification:** certificate or Diploma.

**Age:** Below 28

**Location:** Kimara and Kibaha

Send your CV and contacts to:

**kegesambi@yahoo.com**

115672502

### KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**ARNOLD THEOBALD KISAKA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 271 AFH TOYOTA HIACE. Chassis namba LH71V0003475. Kadi ya gari yenye namba za usajili **T 525 ACQ TOYOTA HIACE.** Chassis namba LH71B0002290.

Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/224353/2020.**

115672602

Jamhuri ya muungano Wa tanzania
Baraza LA ardhi nyumba wilaya ya morogoro.
Maombi na.458 ya mwaka 2019.
EDNA MAFURU NDALLO.....MLETA MAOMBI
DHIDI YA
SALEHE ISLAM..............WAJIB MAOMBI

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA SALEHE ISLAM.**

Popote ulipo unaarifiwa ufike ktk baraza la ardhi na Nyumba la wilaya ya Morogoro tarehe 02/04/2020.Wewe mwenyewe binafsi au mtume mwakilishi wako bila kukosa ambapo MAOMBI yamepangwa kutajwa. Endapo hautaudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.

Imetolewa kwa mkono wangu Leo tarehe 10 mwezi 03 mwaka 2020.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MOROGORO.

215672802


**Uza,**

**Chenye**

**Thamani**

**Kubwa**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# REAL MADRID YAMCHOKA BALE




**MADRID,** Hispania

KLABU ya Real Madrid imeanza kujiandaa kuelekea dirisha la usajili ya kipindi cha majira ya joto wakati wakifikiria kumuachia Gareth Bale huru.

Kwa mujibu wa ripoti kutoka Madrid, kocha, Zinedine Zidane hana mpango wa kuendelea kuwa na Bale kwa msimu mwingine.

Bale anataka kumaliza mkataba wake hapo, lakini klabu hiyo ya Bernabeu kwa sasa inajiandaa kumuachia aondoke, limedai gazeti la Marca.

Raia huyo wa Wales ameshindwa 'kuvaa' viatu vya Cristiano Ronaldo na mwaka 2018 alikaribia kuondoka na kwenda nchini China kabla ya dili hilo kukwama. Bale hajafunga bao lolote la Ligi tangu Septemba na amecheza mechi tatu kwa mwaka huu 2020.

Zidane alijiandaa kumpa nafasi msimu huu, lakini alishindwa kuonesha kiwango na hivyo kutokuwemo kwenye kikosi cha kwanza.

Madrid sasa imeongeza nia ya kutokuendelea kumbakiza Bale ambaye mshahara wake ni pauni milioni 15.4 kwa mwaka, na wakati Brexit itahalalishwa rasmi Januari mwakani, mchezaji huyo hatakuwa kwenye wachezaji wanaotoka Jumuiya ya Ulaya.

Wakala wa Bale, Jonathan Barnett, amebainisha wazi kwamba, mteja wake anajisikia vizuri na maisha hapo kwenye mji mkuu wa Hispania na hana mpango wa kutaka kuondoka.

Lakini Real kwa sasa wameweka wazi hawawezi kumudu mshahara wa Bale.

# Obi Mikel aitema Trabzonspor kisa corona

**ANKARA,** Uturuki

KIUNGO wa Chelsea, John Obi Mikel ameachana na klabu yake ya Trabzonspor ikiwa ni siku chache baada ya kuishutumu mamlaka ya soka ya Uturuki kwa kutosimamisha msimu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Nigeria, alijiunga na klabu hiyo akiwa mchezaji huru kipindi cha majira ya joto kilichopita, akiwa ametia saini mkataba wa miaka miwili, lakini sasa ameondoka kwa miamba hao wa Super Lig baada ya kufikia makubaliano.

Mikel alisema kwamba, hakujisikia poa kuendelea kucheza wakati kuna mlipuko wa ugonjwa hatari, na watampa mishahara yake iliyobaki ili abakie kuwa mchezaji huru.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, ambaye alifurahia misimu 11 yenye mafanikio kwenye Ligi Kuu ya England, alikuwa nguvu muhimu kwa kikosi hicho cha Trabzonspor msimu huu.

Jumamosi iliyopita, nyota huyo alilaumu maamuzi ya kuendelea kwa Ligi kuu ya nyumbani wakati ligi nyingine za Ulaya zikiwa zimesimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Katika taarifa yake alisema: "Kuna maisha zaidi kuliko mpira wa miguu. Sijisikii vizuri na sitaki kucheza kwa hali hii.

"Kila mmoja alitakiwa awe nyumbani na familia yake pamoja na wapenzi wao wakati huu wa hali mbaya.

"Msimu unatakiwa kusimamishwa wakati duniani ikiwa kwenye hekaheka ya mlipuko wa vizuri vya corona."






# *Young kuongezewa mwaka mmoja Inter*

**MILAN,** Italia

ASHLEY Young anatarajiwa kupewa mwaka mmoja zaidi katika mkataba wake ili kuendelea kubakia Inter Milan baada ya kuonesha kiwango cha kuvutia tangu atue hapo Januari akitokea Manchester United.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 alihamia kwa Nerazzurri hapo Januari na amecheza mechi tano za Serie A, akichangia bao moja na asisti mbili kwa klabu yake hiyo mpya.

Young alijiunga na miamba hao wa Serie A kwa mkataba wa awali wa miezi sita, lakini amemshawishi kocha Antonio Conte kupewa mkataba mpya.

Kwa mujibu wa gazeti la michezo la Italia, Gazzetta dello Sport, Young ataongeza muda wake wa kukaa huko Italia.

Young pale Inter ameungana na wachezaji wenzake wa zamani wa Manchester United, Romelu Lukaku na Alexis Sanchez kwenye dimba la San Siro.

Lakini Lukaku amekuwa na wakati mzuri zaidi kwa kufunga mabao 23 kwenye mechi 35, lakini Sanchez raia wa Chile hajawa na wakati wa kuvutia tangu atea hapo kwa mkopo.

Fowadi huyo wa zamani wa Arsenal amefunga bao moja tu katika mechi 15, na sasa inaonekana wazi kwamba atarudi tena kule Old Trafford.

# Euro 2021 yamchelewesha Koeman kuichukua Barcelona

**AMSTERDAM,** Uholanzi

KOCHA wa timu ya taifa ya Uholanzi, Ronald Koeman, amesema kipengele chake cha kujiunga na Barcelona kitachelewa hadi mwaka 2021 baada ya kuahirishwa kwa michuano ya eruo 2020 kwa mwaka mmoja kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Mlinzi huyo wa zamani wa Barca, Koeman alikuwa kwenye mstari kumrithi Ernesto Valverde, ambaye alitimuliwa na nafasi yake kuchukuliwa na Quique Setien Januari mwaka huu.

Koeman awali alibainisha kwamba mkataba wake na Uholanzi una kipengele kinachomruhusu yeye kuondoka na kwenda Camp Nou baada ya Euro 2020.

Huku michuno ya Euros ikiwa imezogezwa mbele kwa miezi 12 kutokana na mlipuko wa virusi vya COVID-19, Mholanzi huyo ameelezea hali ya mkataba wake ulivyo.

"Kipengele kwenye mkataba wangu kwenda Barcelona ni baada ya michuano ya Ulaya," alisema Koeman akinukuliwa na gazeti la Marca.

"Hakuna tarehe iliyotajwa, sasa ni baada ya mashindano ya Ulaya mwaka 2021.

"Lakini sijawaza hilo hata kwa sekunde moja."

Shirikisho la vyama vya soka vya Ulaya, Uefa, liliahirisha michuano ya Euro 2020 Jumanne, na sasa mashindano hayo yatafanyika kati ya Juni na Julai mwaka 2021.



# MARTINEZ ATABAKI INTER - ZANETTI



**MILAN,** Italia

MAKAMU Rais wa Inter Milan, Javier Zanetti anaona kwamba, majaliwa ya Lautaro Martinez yako kwenye soka la Ligi Kuu ya Italia, Serie A, huku mabingwa wa Ligi ya Hispania, La Liga, Barcelona wakiripotiwa kumnyatia.

Barca imekuwa ikihusishwa mno na mpango wa kutaka kumsajili Martinez baada ya Lionel Messi na Luis Suarez kumsifia nyota huyo wa Inter.

Martinez – ambaye amezivutia klabu nyingi Ulaya kama vile Real Madrid, Manchester United na Manchester City – anaonekana kama mrithi wa muda mrefu wa Suarez pale Camp Nou.

Hata hivyo, nahodha wa zamani wa Nerazzurri hao, Zanetti haoni kama raia mwenzake huyo wa Argentinaa, Martinez anaondoka Inter.

"Kwa kipaji alichokionesha, Lautaro ni miongoni mwa wachezaji bora," amesema Zanetti akiiambia Radio Continental. "Leo naona majaliwa yake yapo kwenye soka la Italia.

"Ni mmoja wa wachezaji wanaofurahisha katika soka la Argentina."

Kabla ya kusimamishwa kwa ligi ya Serie A kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, Martinez amekuwa patina mzuri zaidi na mchezaji mwenzake, Romelu Lukaku pale Inter.

Martinez amefunga mabao 11 kwenye Ligi katika mechi 22 msimu huu na mabao 16 kwenye mashindano yote kwa kikosi hicho kinachonolewa na Antonio Conte.

# *Shabiki ashtakiwa kwa ubaguzi*

**MANCHESTER,** England

MTU mmoja ameshtakiwa kwa tabia za kibaguzi wakati wa mchezo wa nyumbani wa Manchester City dhidi ya Manchester United wa Ligi Kuu ya England.

Polisi wamemfungulia mashitaka shabiki huyo baada ya kuonesha vitendo hivyo vya kibaguzi wakati wa mchezo uliopigwa Desemba 7 kwenye uwanja wa Etihad, ambapo United ilishinda 2-1 dhidi ya majirani zao hao.

Ameshitakiwa kwa kuonesha ishara za kibaguzi na kelele dhidi ya wachezaji.

Kituo kikuu cha Polisi cha Manchester (GMP) kimemtaja Anthony Burke mwenye umri wa miaka 41 kuwa atafikishwa mahakama ya Salford mjini hapa Aprili 15 mwaka huu.

Polisi imesema "Anthony Burke wa Wythenshawe ameshitakiwa kwa ubaguzi wa rangi michezo kutoka kifungu cha 5 cha sharia ya michezo kilichowekwa."

Taarifa ya polisi iliongeza: "majira ya 12.55 jioni Jumamosi ya Desemba 7 mwaka 2019 aliitwa kumzuia shabiki aliyekuwa akionesha ishara za kibaguzi na kelele kwa wachezaji wakati wa mchezo wa dabi ya Manchester kwenye uwanja wa Etihad."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ICARDI AIKATAA PSG ATAKA KURUDI ITALIA

●●●Sijui kama mwakani tutaishi Milan au Paris, kwenye soka huwezi kujua..

**PARIS,** Ufaransa

MAURO Icardi amebainisha kupanga kurudi nchini Italia mara tu baada ya kumaliza kucheza kwa mkopo pale Paris Saint-Germain kipindi cha majira ya joto kinachokuja.

**Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Argentina aliruhusiwa kuondoka Inter Milan na kocha, Antonio Conte kipindi cha majira ya joto kilichopita na kujiunga na miamba hao wa Ufaransa kwa mkopo wa muda mredu.**

Amekuwa na kiwango cha kuvutia pale kwenye jiji la Paris, akifunga mabao 20 katika mechi 31 na kuisaidia kutinga robo fainali ya Ligi ya mabingwa Ulaya na kuwaweka kwenye nafasi nzuri ya kutwaa taji la Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1.

Lakini gazeti la Italia la Calciomercato limedai kwamba Icardi haoni majaliwa ya kucheza muda mrefu kwa kikosi hicho kinachonolewa na kocha, Thomas Tuchel na anataka kurudi kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, kipindi cha majira ya joto.

Mkataba wake na Inter Milan unamalizika Juni 2021, lakini Conte aliweka wazi kipindi cha majira ya joto kilichopita kwamba, Icardi hayupo kwenye mipango yake ya baadae.

Imedaiwa kwamba kama Nerazzurri hao watashindwa kufikia makubaliano ya kumuuza Icardi kwenda Juventus au Napoli, Icardi atafikiria kurudi Inter.

Mwezi uliopita pia iliripotiwa kwamba Real Madrid wanajiandaa kutoa fedha na mchezaji mmoja kwa ajili ya fowadi huyo.

Lakini inaeleweka kwamba mke na wakala wake, Wanda Nara, hataka uhamisho wa kwenda pale Bernabeu na angependa ajiunge na Juve.

Hata hivyo, alibainisha kwamba, chaguo lipo chini ya mume wake mwenyewe.

Alisema: "Kama Mauro hatakwenda Juve? Hilo silijui. Sijui kama mwakani kama tutaishi Milan au Paris, kwenye soka kamwe huwezi kujua. Atachagua na sisi tutamfuata."

## ZISIKUPITE

### EPL KUCHEZA BILA MASHABIKI

MABOSI wa Ligi Kuu ya England wanapanga mechi zilizobaki za Ligi Kuu ya England zitakwenda huku milango ya viwanja ikiwa imefungwa.***(Sun)***

### MADRID KUMUACHIA BALE

KLABU ya Real Madrid tayari inafanya mipango yake ya usajili ya kipindi kinachokuja cha majira ya joto na wanaweza kumuacchia fowadi wao, Gareth Bale, mwenye umri wa miaka 30 raia wa Wales, kuondoka akiwa huru. ***(Marca)***

### CITY YATAJA BEI YA MAHREZ

KLABU ya Manchester City imepanga bei ya pauni milioni 80 kwa winga wake, Riyad Mahrez, mwenye umri wa miaka 29 raia wa Algeria, ambaye amekuwa akihusishwa na mpango wa kwenda Paris St-Germain. ***(Sun)***

### SANE APEWA OFA MBILI

WINGA wa Manchester City, Leroy Sane mwenye umri wa miaka 24 raia wa Ujerumani amepewa ofa na klabu mbili ili aondoke pale kwenye uwanja wa Etihad. ***(Goal)***

### ZAMWANIA KIUNGO WA JUVE

KLABU ya Paris St-Germain na Chelsea zinapanga kutuma ofa zao kipindi cha majira ya joto kwa ajili ya kumsajili kiungo wa Juventus na timu ya taifa ya Bosnia-Herzegovina, Miralem Pjanic mwenye umri wa miaka 29. ***(Calciomercato)***

### YAKASIRISHWA NA BARCA

KLABU ya Arsenal imegazibishwa na namna Barcelona inavyoendesha zoezi lao la kutaka kumsajili mshambuliaji wa kimataifa wa Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang mwenye umri wa miaka 30. ***(Star)***

### TRIPPIER KUSTAAFIA BURNLEY

MLINZI wa kulia wa Atletico Madrid na timu ya taifa ya England, Kieran Trippier, mwenye umri wa miaka 29, amebainisha kwamba anataka kustaafika soka akiwa na klabu yake ya zamani ya Burnley na ndio timu pekee inayoweza kumfanya arudi kwenye ligi Kuu ya England kucheza pale kwenye dimba la Turf Moor chini ya kocha, Sean Dyche. ***(Burnley Express)***

### ARTETA KUMUUZA MKHITARYAN

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, anataka kumuuza kiungo wa Armenia, Henrikh Mkhitaryan, mwenye umri wa miaka 31, kipindi cha majira ya joto na Roma wapo tayari kumpa mkataba wa kudumu. ***(Express)***

### UTAJIRI WA ROMAN WASHUKA

MMILIKI wa klabu ya Chelsea, Roman Abramovich mwenye umri wa miaka 53, ameripotiwa kwamba utajiri wake umeshuka kwa pauni milioni 2.4 mwaka huu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, ingawa bado ana utajiri wa zaidi ya pauni bilioni 10. ***(Star)***

### NYOTA WA NEWCASTLE NJE

MLINZI wa kushoto wa Uholanzi, Jetro Willems mwenye umri wa miaka 25, ambaye anacheza kwa mkopo pale Newcastle akitokea Eintracht Frankfurt ya Ujerumani, hatacheza tena mwaka huu 2020 baada majeruhi yake ya goti ni makubwa zaidi tofauti ni ilivyozaniwa. ***(Bild)***

HABARI MICHEZO

## Banda arejea mazoezini Sauzi

**Na Saada Akida**

HALI ya beki wa timu ya Taifa (Taifa Stars) na klabu ya Highlands Park ya Afrika Kusini Mtanzania, Abdi Banda imeimarika na sasa ameruhusiwa kujiunga na wachezaji wenzake baada ya vipimo kuonyesha hajapata maambukizi ya virusi ya corona (COVID-19).

Banda (pichani) alisimamishwa kuendelea na mazoezi ya pamoja na wachezaji wenzake baada ya kuhisiwa huenda ameathirika na virusi vya corona.



Banda aliliambia Nipashe kuwa ameruhusiwa kurejea mazoezini baada ya vipimo kutoka na kungundulika kwamba hana ugonjwa huo ambao sasa unasumbua duniani.

"Napenda kutoa shukrani zangu kwa wote mlioguswa au kushtushwa na habari juu yangu, kikubwa kila kitu kimeenda sawa na kwa baraka za Mungu imegundulika haukuwa ugonjwa huo unaosumbua kwa sasa duniani," alisema Banda.

Uongozi wa Highlands Park ulilazimika kumweka chini ya uangalizi maalum baada beki huyo kupatwa na mafua makali na kikohozi wakati wa mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Supersport hali ambayo ilimsababishia kushindwa kumaliza mechi hiyo na kwenda kupimwa corona.

## Z'bar yajivunia chipukizi wake

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limesema mafanikio yanayoonekana katika timu zake za vijana za umri chini ya miaka 15 (U-15), U-17 na U-20 yanatokana na kuundwa na wachezaji wenye vipaji na viwango.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaimu Katibu wa Kamati ya Soka la Vijana wa ZFF, Seif Mohamed "King" alisema wanatarajia watafanya vizuri katika mashindano watakayoshiriki kutokana na uteuzi wa makini uliofanywa tofauti na ilivyokuwa hapo awali.

King alisema timu hizo zitakuwa endelevu na wachezaji watalelewa vema ili waweze kupeperusha vizuri bendera ya Zanzibar katika mashindano mbalimbali watakayoshiriki.

"Timu hizi zinafundishwa na makocha tofauti, lakini kubwa tunalojivunia ni namna vijana wanavyojituma mazoezini, kila siku wanaimarika na tunaamini vipaji walivyonavyo wakivitumia vema, watakuwa wachezaji wazuri Zanzibar," alisema King.

Aliongeza kuwa kamati hiyo inaendelea na ziara ya kusaka wachezaji wenye vipaji katika Wilaya za Unguja na baadaye itaelekea Wilaya ya Kaskazini A, B na kisha Kisiwani Pemba.

Kiongozi huyo aliwataka viongozi wa ngazi za wilaya kuhakikisha wanawaendeleza wachezaji wao ambao wanazichezea timu za kombaini za wilaya kwa sababu hao ndio nyota wa baadaye wa timu ya Taifa ya Zanzibar (Zanzibar Heroes).

# MAPRO AZAM WARUDISHWA KWAO, NDANDA YAATHIRIKA

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Azam FC umewapa ruhusa wachezaji wake wote wa ndani na nje ya nchi kuondoka kwenye kambi ya klabu hiyo kutokana na kujiepusha na maambukizi ya virusi vya corona, imeelezwa.

**Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat' alisema wamefunga kituo cha klabu hiyo chenye wachezaji wakubwa na wa timu za vijana wenye umri mbalimbali kwa muda wa siku 30.**

Popat alisema wameamua kufikia uamuzi huo ili kuwakinga na virusi vya corona mpaka pale serikali itakavyotoa maelekezo mengine.

"Tumewaruhusu wachezaji wetu kuanzia leo (jana), wale wakigeni watarudi nchini kwao, na wa timu ya wakubwa na vijana pia, hadi muda ambao ulitolewa katika tamko la serikali utakapomalizika," alisema Popat.

Kiongozi huyo alisema licha ya mlipuko wa virusi vya corona kukatisha programu yao ya mazoezi, bado wataendelea kujipanga kuhakikisha wanafanya vizuri katika mashindano ya Kombe la FA ili kufikia malengo yao ya kukata tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa.

Wakati huo huo, uongozi wa Ndanda FC unatarajia kuwapa wachezaji wake likizo fupi kufuatia kuwapo kwa janga la virusi vya corona.

Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Selemani Kachele, alisema timu yake imeathirika kwa kiasi kikubwa kwa kusimama kwa Ligi Kuu kutokana na kutumia kiasi kikubwa cha fedha kuandaa timu yao ili ifanye vizuri katika michezo inayokuja.

"Sisi kama uongozi kwa pamoja tumeamua kuwapa likizo fupi wachezaji wetu, lakini hivi karibuni tutaendelea na mazoezi mpaka hapo itakapotangazwa rasmi tarehe ya kuanza tena kwa ligi," alisema Kachele.

Katibu huyo alisema ugonjwa huo 'umevunja' mipango mingi ikiwamo ya uchumi wa soka kutokana na maandalizi ambayo tayari walikuwa wamefanya katika mechi hizi za lala salama.

Hata hivyo, Kachele alisema wanaungana na serikali kwa pamoja kuhakikisha wanatekeleza maagizo yote yaliyotolewa na Wizara ya Afya katika kipindi hiki kigumu cha kujikinga na ugonjwa huo.

MTIFUANO...




Mshambuliaji wa DTB FC, Iddi Simba (katikati), akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa The Mighty Elephants ya Songea, Jafari Mwarami, katika mchezo wa Ligi Daraja la Pili uliopigwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. DTB FC ilishinda 3-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## *DTB FC yatamba itapanda daraja*

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya DTB ya jijini Dar es Salaam ambayo inashiriki Ligi Daraja la Pili imetamba imejipanga vizuri kuhakikisha inafuzu kucheza Ligi Daraja la Kwanza msimu ujao.

DTB ambayo ipo Kundi C inashika nafasi ya pili katika msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 21, huku ikibakiza mchezo mmoja mkononi dhidi ya Tukuyu United.

Akizungumza baada ya mchezo wa ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya The Mighty Elephants ya Songea kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam Jumatatu wiki hii, Kocha Mkuu, Edward Lazaro alisema malengo yao ni kupanda daraja na wanaamini mipango yao itafanikiwa.

Lazaro alisema timu yake ina kikosi imara na wachezaji wenye uwezo wa kucheza katika ligi ya ngazi yoyote hapa nchini.

"Malengo yetu ni kucheza Ligi Daraja la Kwanza, na najiamini tutafanikiwa hilo, nasema hivyo kwa sababu ya sapoti nzuri tunayoipata kutoka kwa wadhamini wetu, benki ya DTB na wao wanataka kuona timu inafanya vizuri ili iweze kupanda daraja," alisema Lazaro.

Katika mchezo huo wa Jumatatu, DTB ilianza mchezo huo kwa kasi kali, huku bao lake la kwanza likifungwa na Robert Kobelo dakika ya saba, la pili likifungwa na Juma Madeba dakika ya 53 na Edwin Baluha akafunga la tatu dakika ya 75.

Kocha huyo pia aliwasifia wadhamini wao benki ya DTB kwa kusema kuwa, kupitia wao timu yake inafanya vizuri katika mechi zake.

Michezo
Alhamisi Machi 19, 2020
Nipashe



Icardi aikataa PSG ataka kurudi Italia UKURASA 30

WANACHEEEKA...



Wachezaji wa Simba wakitoka katika uwanja wao wa mazoezi wa Mo Simba Arena uliopo Bunju nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam, juzi. Simba inaongoza msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 71 baada ya mechi 28. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Sven: Kilichobaki Simba ni rekodi tu

## ●●● Wamaliza hesabu za ubingwa, TFF yasema Ligi Kuu sasa kuchezwa bila mashabiki...

**Na Somoe Ng'itu**

HUKU timu yake ikiwa katika nafasi kubwa ya kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, amesema kikosi chake kimejiandaa kuweka historia kwenye ligi hiyo kwa kumaliza na idadi kubwa ya pointi msimu huu.

**Hata hivyo, Simba ambayo imekuwa ikipata sapoti kubwa kutoka kwa mashabiki wake, sasa italazimika kusaka rekodi hiyo dimbani bila uwapo wao uwanjani kufuatia Kamati ya Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB), kupitisha azimio la mechi zote kuchezwa bila mashabiki baada ya kipindi cha mwezi mmoja cha zuio la serikali endapo hali ya maambukizi ya virusi vya corona (COVID-19) haijakaa sawa.**

Akitangaza uamuzi wa kikao cha kamati hiyo jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa TPLB, Almasi Kasongo, alisema baada ya kumalizika siku 30 za serikali ilizotangaza kusimamisha michezo yote, wachezaji watapimwa na wakijiridhisha kuwa hawana maambukizi ligi hiyo itachezwa bila mashabiki.

Simba ambao pia ni vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo imesimama kwa muda kutokana na kujiepusha kwa maambukizi ya virusi vya corona, imecheza mechi 28 na imejikusanyia pointi 71 ikifuatiwa na Azam FC yenye pointi 54 na Yanga pointi 51, lakini ikiwa na mchezo mmoja pungufu.

Wekundu wa Msimbazi wamebakisha mechi 10 na endapo watashinda zote watafikisha pointi 101, lakini ili kujihakikisha ubingwa kwa mara ya tatu mfululizo, kikosi hicho kinahitaji pointi 14 na kufikisha pointi 85, ambazo hazitafikiwa na klabu nyingine yoyote kwenye ligi hiyo msimu huu.

Hata hivyo, Sven ameweka wazi kupoteza mechi dhidi ya Yanga ni sehemu ya matokeo ya mchezo wa soka, na kuwataka mashabiki wa klabu hiyo kutoendelea kuumia.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Sven alisema wanahitaji kupata ushindi katika mechi hizo 10 zilizosalia ili kutimiza malengo yao.

Sven alisema anafahamu mechi zote zilizobaki zitakuwa na ushindani mkubwa kwa sababu kila upande utaingia uwanjani ukiwa na malengo yake na hali hiyo huongeza ugumu.

"Nina furaha kuona tuko katika nafasi nzuri, lakini bado hatujamaliza kazi, mechi zilizobaki ni nyingi na tunatakiwa kushinda, muhimu ni kuendelea kujipanga ili kuweka rekodi na historia, tunaweza kufanya hivyo kama tutakuwa imara zaidi," alisema Sven.

Naye Kocha Msaidizi, Selemani Matola, alisema kikosi chao hakitapunguza kasi na mara ligi itakaporejea, watahitaji kushinda kila mchezo ulioko mbele yao.

"Tunataka kutetea ubingwa kwa heshima, pia tunataka kumaliza msimu kwa kishindo, hatutabweteka, tunajua msimu huu timu zitakazoteremka daraja zimeongezeka, hivyo ushindani utakuwa hadi siku ya mwisho," alisema Matola.

Kiungo na nahodha huyo wa zamani wa Simba, alisema kikosi chao kilifanya mazoezi jana asubuhi kama kawaida, lakini mchana walitarajia kukutana na uongozi wa klabu hiyo ili kujadili hatima ya kusimamisha programu kutokana na taharuki ya virusi vya corona ambavyo vimeshaingia nchini.

# Ndayiragije: Corona imetibua mipango Stars

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, Etienne Ndayiragije, amesema mlipuko wa ugonjwa wa maambukizo ya virusi vya corona (COVID-19), umeathiri program ya timu yake katika mazoezi yao ya kujiandaa na michuano ya fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) na kuwania kufuzu Afcon 2021.

Ndayiragije alisema kusogezwa mbele kwa michuano hiyo kutokana na mlipuko wa ugonjwa huo ambao unasumbua duniani umeathiti mipango yake yote ya maandalizi ya timu hiyo.

Alisema licha ya kuharibu mipango yake, lakini pia anaungana na serikali na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kusitisha kambi pamoja na kusimamisha mashindano yote ambayo yalikuwa yakitarajiwa kufanyika hapa nchini.

"Hili ni janga la dunia nzima, hivyo hatuna budi kuungana na serikali pamoja na taasisi zote za michezo kuahirisha, ila ugonjwa huo umeharibu mipango yangu ambayo tayari nilikuwa nimeipanga,".

"Hatujui ni lini ugonjwa huu utakwisha au kupungua, hivyo hata huo muda ukifika itanilazimu kubadili kikosi kutegemeana na kiwango cha wachezaji wakati huo na muda wa maandalizi kwani ni wazi yatakuwa ya zimamoto," alisema Ndayiragije.

Alisema itakapofika muda huo, atalazimika kufanya mabadiliko ya kuita wachezaji ambao wataendana na kasi anayoihitaji kutokana na ratiba ambayo atakuwa nayo.

"Kama nilivyosema awali hatujui lini tena tutaendelea na maandalizi, ila tutakaporudi tena, mchezaji anatakiwa kuendana na kasi ya maandalizi ya michuano ambayo itakuwa mfululizo na hatutakuwa na muda," alisema kocha huyo.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042